ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.

12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Sita - Tarehe 29 Januari, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba kuweka mezani hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwaka 2012/13. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa idhini ya Waziri wa Kilimo na Maliasili, napenda kuweka hati mezani hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwaka 2012/13. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka mezani hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwaka 2012/13. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwaka 2013/14. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

TAARIFA ZA SERIKALI

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya mwaka 2012/13

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii, lakini kabla sijafanya hivyo, naomba nimshukuru Mwenyezi

Mungu kwa kutujaalia tukawa wazima sote na kufika hapa ili kuendelea na shughuli zetu hizi muhimu.

Mhe. Spika, napenda kwanza niishukuru sana Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa uono wao mkubwa na upeo wao mzuri ambao kwa kweli sisi Wizarani umetusaidia sana na utatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu. Taarifa yao Mhe. Spika, kwa kweli imetupa sisi kichocheo cha kufanya shughuli zetu kwa uwazi kabisa na naahidi kwamba ripoti hii tutaichukua kama ni moja katika shughuli muhimu ambazo zitatusaidia katika kufanya na kukamilisha shughuli zetu za Wizara.

Mhe. Spika, pili napenda niwashukuru wachangiaji wote ambao wamechangia katika Wizara yetu. Wachangiaji wote walikuwa ni 15. Na ukimuacha Mhe. Mwenyekiti, basi waliochangia ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Suleiman Hemed Khamis, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Abdalla Moh'd Ali, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, Mhe. Marina Joel Thomas na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

Mhe. Spika, wachangiaji wote hao walizungumzia masuala karibu manne au matano kwa ujumla. Lakini na suala la sita lilichangiwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin peke yake. Lakini zaidi katika michango yote hiyo, mchango mkubwa ulikuwa unakwenda katika Mahakama. Mahakama zetu zililaumiwa sana na mimi nakubali lawama hizo. Mengi takriban yote ambayo wameyasema Waheshimiwa Wajumbe ni ya kweli, na sisi tunachopenda kuwahakikishia ni kwamba yote ambayo wameelekeza humu waliyoyachangia sisi tumeyachukua na tutayafanyia kazi kikamilifu.

Mhe. Spika, sitopenda kuwataja mmoja mmoja katika mambo ambayo yalichangiwa, lakini nitaeleza kwa ujumla mambo yote ambayo yamechangiwa. Katika Mahakama Mhe. Spika, kulikuwa kuna mambo mengi. Kwanza ni ucheleweshaji wa kesi, ni kweli kesi zinachelewa sana Mahakamani hili tunalijua. Na kwa sababu hiyo ndio hata tukaunda Kamati ya kusukuma mbele masuala haya ya kesi. Kamati hizo zimeshaanza kufanya kazi, lakini ninachowaahidi Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba tutaziharakisha zaidi ili shughuli zao ziweze kwenda kwa haraka zaidi kuliko hivi sasa ambavyo tunafanya.

Napenda niseme tu kwamba ucheleweshaji wa kesi wakati mwengine unahusiana na mambo mengi, pengine uchunguzi haujakamilika, lakini zaidi na jamii. Mhe. Spika, jamii nayo ina mchango mkubwa katika ucheleweshaji

wa kesi. Kuna kesi nyengine ambayo jamii hawataki kabisa kuwa mashahidi, na unapokuwa huna shahidi, basi kesi ama itachelewa au kesi itafutwa. Kwa hivyo, ombi langu kwa jamii ni kwamba tujitahidi jamii pale ambapo tunatakiwa tutoe ushahidi katika Mahakama zetu, basi jamii wajitokeze kwa wingi ili tuweze kukamilisha suala hili.

La pili Mhe. Spika, lililozungumzwa ni suala la ubovu wa majengo ya Mahakama. Ni kweli Mahakama zetu nyingi ni za zamani na ni mbovu. Lakini kutokana na ubovu huo na hali tuliyonayo tumeanza kufanya ukarabati wa baadhi ya majengo na tutaendelea hivi hivi kwa kadri ambapo tutapata fedha. Hivi sasa tunashukuru jengo la Mahakama Kuu tumeshalikamilisha. Tumeanza na jengo la Mahakama ya Chake Chake, la Makunduchi, la Mkoani na la Chwaka.

Haya yote yanahitaji fedha na fedha zinazogaiwa tunazijua sisi wenyewe. Lakini kila tutakapopata fedha tunawahakikishia kwamba tutajaribu kuyakarabati majengo haya.

Pia tuna nia ya kujenga majengo mapya pale ambapo nafasi ya fedha tutapata. Tuna kiwanja kwa mfano Mwanakwerekwe, Makunduchi na Pemba, vyote hivi ni vya majengo ya Mahakama. Kwa hivyo, pale ambapo tutapata uwezo, basi nawahakikishia kwamba masuala ya ujenzi wa Mahakama mpya hilo lipo mbele katika shughuli zetu za Wizara.

Mhe. Spika, lilizungumzwa suala la rushwa na udhaifu wa Mahakimu, nakubaliana nalo kwamba matatizo haya yapo, tunajaribu kuyapiga vita sana, tumeanza kufanikiwa. Lakini Mhe. Spika, hapa pia ningelipenda niombe kwamba pale ambapo mwenye kesi mdai au mdaiwa anapodaiwa rushwa, basi asiwe mgumu kwa kutupa taarifa. Kuna wengine wanatupa taarifa kwamba mimi nilikwenda nikakabidhi kiasi hichi, lakini ukimwita kutaka kutoa ushahidi sasa hawezi anakwambia mimi namwachia Mungu.

Sasa kama unamwachia Mungu, sisi tutakuwa hatuwezi kuchukua hatua. Kwa hivyo, tatizo moja ambalo tunalipata hapa Waheshimiwa ni suala la jamii wenyewe haipo shirikishi na sisi. Kwa hivyo, hapa tunashindwa kuchukua hatua kwa sababu ya ile jamii. Lakini ingelikuwa jamii wapo tayari kutwambia kwamba mimi nilimpa au nilifanya hivi na hivi, hapo kesi yetu itakuwa ni nzuri na hatua tunaweza tukachukua haraka haraka. Kwa hivyo, mimi naomba sana jamii ishirikiane na sisi pale ambapo wanakuja kutupa taarifa.

Hivi juzi Mhe. Spika, kuna watu walikuja na wakasema makarani wale walitaka shilingi 40,000/= kupigiwa *proceedings*, yaani kupigiwa zile chapa.

Mimi nikamuuliza maswali mengi na mwisho nikamwambia sasa je, upo tayari kutoa ushahidi, akasema hapana mimi namwachia Mungu. Kwa hivyo, hatufanikiwi Mhe. Spika, tusimuachie Mungu peke yake, lakini na sisi tuanze huku halafu Mungu atahukumu mbele. Sasa naomba sana jamii itusaidie katika masuala haya.

Mhe. Spika, ni kweli kuna ukosefu wa usafiri na uhaba wa vifaa na haya yamechangiwa sana katika hata kuahirisha kesi. Kwa sababu ni kweli baadhi ya Mahakama wanaahirisha kesi kutokana na kukosekana kwa vifaa kama vile daftari na vitu vyengine kama hivyo. Kwa hivyo, tatizo hapa Mhe. Spika, tunalijua ni tatizo la ukosefu wa fedha. Sasa pale ambapo tunapata fedha na hapa pana tatizo moja kubwa Mhe. Spika. Tatizo lililopo ni kwamba fedha zinapotiwa katika kifungu cha Mahakama, fedha zile zinatiwa kama ni za Mahakama, lakini tujue tu kwamba tuna Mahakama nyingi Unguja na Pemba.

Sasa fedha hizo hizo ndio uzigawe kwa kama ni stationaries.Kwa hivyo, stationaries kwa Mahakama zote za Unguja na Pemba. Kwa hivyo, zile fedha zinavyotiwa unaweza ukaziona nyingi milioni 20 kwa mfano, lakini ukizigawa milioni 20 kwa madaftari ya Unguja na Pemba, kwa kalamu pengine na kwa vifaa vyengine Unguja na Pemba. Mhe. Spika, hilo ni tatizo kubwa sana.

Kwa hivyo, fedha ambazo tunapata ni kidogo na hazikidhi haja kwa Mahakama zote tulizonazo Unguja na Pemba. Tunajitahidi hivyo hivyo, lakini pale ambapo itafika haja kwamba madaftari hapana, basi tunaomba zile sehemu ambazo zinahusika watuarifu mapema.

Kwa sababu kwa mfano tatizo hili Mhe. Spika, ndio kwanza nalisikia katika Baraza. Sasa pengine wangelituelezea mapema tungeliweza kufanya hatua nyengine ili kupata mafaili haya au vifaa ambavyo vinahusika. Kwa hivyo, mimi nakiri kwamba matatizo haya yapo, lakini hii kama nilivyosema ni changamoto ambayo tumepewa na Kamati hii na tunaahidi kwamba tutaifanyia kazi ipasavyo.

Mhe. Spika, suala la uwezo wa Mahakimu lilizungumzwa sana. Mahakimu kama tunavyojua ni kwamba wana utaratibu wao wa uteuzi. Sasa kama kuna suala ambalo tunalitilia wasiwasi kwa Mahakimu, basi mimi nahisi ni vyema tukakaa pamoja tukalitizama na halafu tukafuata utaratibu ule ule wa uajiri wa Mahakimu katika *Judiciary Service Commission* ili tuweze kuona tutafanya namna gani kuyatatua matatizo haya. Lakini kama nilivyosema suala hili mimi nitalichukua na nitalifanyia kazi ili tuweze kuona namna gani tunaweza tukasaidia katika uwezo huu wa Mahakimu.

Mhe. Spika, ni kweli kuna baadhi ya kesi hukumu ambazo zimetolewa, kwa kweli haziridhishi kabisa. Unapotoa hukumu ya mtoto aliyebakwa ukatoa faini ya shilingi laki nne kwa kweli hilo si jambo la maana hata kidogo. Na sisi Wizarani tulipopata habari hii tuliwasiliana na Afisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali na tukakata rufaa na rufaa hiyo, sina uhakika kama imeshamalizika au bado.

Mhe. Spika, tulikata rufaa na naamini kwamba ikiwa ushahidi upo, basi adhabu hiyo inaweza ikabadilishwa kutokana na utaratibu wetu ambao tulihisi kwamba tuufanye. Kwa hivyo, tunapopata kesi kama hizo haraka tukipata taarifa tunachukua hatua nyengine za kukata rufaa kwa mujibu wa utaratibu wa sheria ambazo zimewekwa.

Suala la dhamana nalo lilizungumzwa. Mhe. Spika, hapa nafikiri lazima Waheshimiwa Wajumbe tuwe wakweli. Dhamana ni haki ya kila mtu na kama mshtakiwa atapelekwa Mahakamani hakupewa dhamana, ni sisi ambao tunajaribu kulalamika. Na tukitoa dhamana, ni sisi ambao tunalalamika. Kwa hivyo, nafikiri tujue tu kwamba dhamana ni haki ya kila mshtakiwa, lakini ina masharti yake, unaweza ukanyimwa dhamana au unaweza ukapewa dhamana.

Na kuna kesi nyengine ambazo kwa mujibu wa sheria, *DPP* atakataa kutoa dhamana. Lakini zile ambazo unaweza ukatoa dhamana kuna utaratibu wake lazima uukamilishe. Sisemi au siondoi lile suala la kusema kwamba pengine rushwa inacheza ili kwa mtu kupewa dhamana, lakini lazima tutizame utaratibu kwamba dhamana ni haki ya kila mtu na hivyo ndivyo Mahakama inavyofanya.

Kama kuna mtu mmoja au wawili ambao wanakwenda kinyume na utaratibu huo inawezekana. Lakini hapa tunaomba yanapotokea mambo kama haya sisi mkitujulisha na mkiwa mpo tayari kutoa ushahidi hapo ndio tunaweza kuchukua hatua. Lakini mbali ya hayo Mhe. Spika, sisi tutayatizama na tutajaribu kukaa na wahusika ili tuweze kulipitia suala hili na kutizama hasa utaratibu mzuri wa kutekeleza majukumu haya.

Kuna suala jengine ambalo lilizungumzwa la Mahakama ya Wawekezaji. Mhe. Spika, suala la Mahakama ya Wawekezaji hili kidogo mimi bado sijaliafiki. Kwa sababu hatuwezi kuanzisha Mahakama za mtu mmoja mmoja au za kikundi itakuwa sivyo. Hapa mimi nitakubaliana na wachangiaji tukisema kwamba suala hili lipewe *priority* katika mfumo ule ambao tunataka kuanzisha kama Mahakama katika kesi za ubakaji. Yaani kuwe na *session cases.* Linakuja suala la wawekezaji anapewa Hakimu anaambiwa ushughulikie kesi hii mpaka imalizike. Lakini kabisa hatuwezi kuanza Mahakama nyengine za wawekezaji, halafu kesho kutwa tukasema

Mahakama nyengine za watu hawa, itakuwa Mahakama zetu tunazigawa kitabaka kitu ambacho si kizuri.

Hili mimi nitalitizama kwa njia hiyo ya kuwa na *session cases*, pale wawekezaji wanapokuwa wana kesi, basi tutizame kwamba tunaweza tukampa Hakimu tukamwambia kwamba suala hili lishughulikie mpaka limalizike kama ambavyo tunataka kuanza kwa kesi za ubakaji.

Mhe. Spika, kesi za ubakaji tuna utaratibu hivi sasa tunauandaa ili ikenda kesi ya ubakaji anakabidhiwa Hakimu hana suala la kusema kesi imeahirishwa mpaka tarehe 30, tarehe ngapi, anaendelea moja kwa moja mpaka kesi ile inamalizika. Kwa hivyo, hapo itachukua muda mfupi na hatua zile kama ni adhabu au kama ni hatua nyengine zitakuwa haraka haraka na watu watajulishwa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba niwahakikishie Wajumbe kwamba suala hili la kuanzisha Mahakama ya Wawekezaji mimi au Wizara yetu tutalitizama kwa misingi hiyo.

Mhe. Spika, kuna suala jengine ambalo limezungumziwa katika *case delay.* Kama nilivyosema kwamba *case delay* hizi tunazijua na tumeunda Kamati za kusaidia mambo kama haya.

Mhe. Spika, kuna suala jengine ambalo lilizungumzwa la *Law Review Commission.* Napenda niseme tu kwamba katika kurekebisha sheria, si Wizara tu peke yake ambayo ina jukumu la kurekebisha sheria. Na sisi tumetoa taarifa kwa kila Wizara kwamba kama wana sheria ambayo wanahisi ni ya zamani na haiwezi kufanya kazi tena katika mazingira haya, basi watuarifu ili tuweze kuishughulikia.

Na huu ndio utaratibu ulivyo. Lakini ofisi yangu ya *Law Review Commission* haiwezi ikajua sheria zote za Mawizara yote ambazo hazifanyi kazi. Ni kila Wizara ambayo inahusika. Kama uko kilimo au uko ufugaji, basi wewe ndio utasema sheria hii ya ufugaji ya mwaka 1917 hivi sasa haikidhi haja tena. Kwa hivyo, wewe ndio unani-*initiate* lile suala la sheria kufanyiwa marekebisho. Tukifanya hivyo, tunaweza tukenda haraka haraka.

Hata hivyo Mhe. Spika, kuna sheria karibu tisa ambazo tumeshazifanyia marekebisho kwa misingi hiyo. Kuna Sheria ya Ushahidi ya mwaka 1917 tumeshaifanyia kazi, Sheria ya Vileo sura ya 163, Sheria ya Rasilimali ya Mifugo, Tume ya Kurekebisha Sheria yenyewe, Sheria ya Usafirishaji Bidhaa, Sheria ya Makampuni na sheria nyengine ambazo zimo katika mkondo huu wa kufanyiwa marekebisho. Sheria ya Mikataba kwa mfano, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sheria ya *Legal Practitioners,* zote hizi tumeshazifanyia marekebisho kwa misingi hiyo.

Kwa hivyo, *Law Review Commission* tunafanya zile sheria pale ambapo tutapata *hint* kwa Wizara inayohusika kwamba sheria hii ni ya zamani na hivi sasa haikidhi haja tena. Na Wizara tunaomba sana watwambie ni sheria zipi ambazo wanahisi zimeshapitwa na wakati ili tuweze kuzitizama na kuzipitia.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limezungumzwa ni suala la Baraza la Katiba na Katiba Mpya. Mhe. Spika, suala hili ni suala la nchi nzima. Bunge la Katiba ambalo litakaa na kujadili Katiba hiyo. Lakini mimi binafsi kama Abubakar, nahisi ni vizuri kwamba tukiwa tunakwenda kule tuwe na kauli moja katika suala zima la utaratibu wa Zanzibar.

Hili tunajua kuna *collective responsibility*. *Collective responsibility* hii inabebwa na Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza. Mimi kama ni Waziri wa Katiba na Sheria nitamshauri kiongozi wangu na maamuzi yatatoka kwa njia hiyo ambayo Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza atatuelekeza. Kwa hivyo, ninachoweza kusema ni kwamba nimelipokea suala hili nitalipeleka kwa kiongozi wetu wa serikali, tena yeye atatoa maelekezo kwa mujibu wa utaratibu huo.

Mhe. Spika, suala jengine lililozungumzwa ni suala la *DPP*. Ni kweli kulikuwa kuna matatizo ya maslahi kutokana na marekebisho yaliyofanywa, lakini matatizo hayo tuliyashughulikia na tukaonana na wahusika na hivi sasa *process* ipo katika harakati za kutizamwa, ni kitu gani ambacho kimekosekana ili waweze kufanya marekebisho yanayostahiki. Kwa hivyo, Mhe. Spika, suala la *DPP* na wafanyakazi wake hatujalisahau tumeona matatizo yaliyopo na bado tunalifanyia kazi na naamini kwamba tunaweza tukapata mwelekeo mzuri.

Mhe. Spika, suala la wakfu nalo lilizungumzwa zaidi ni kuhusu uelimishaji wa shughuli za wakfu. Nina furaha kusema kwamba Kamisheni ya Wakfu imetoa kitabu kuhusu muongozo wa wakfu katika maeneo mbali mbali. Kwa mfano mashamba, nyumba za wakfu na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Ningeliomba Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi wengine wakapitia kitabu hichi cha muongozo ili waweze kujua utaratibu gani ambao tumeuandaa kwa suala zima la nyumba za wakfu na mashamba ya wakfu.

Matatizo tuliyonayo hivi sasa hasa katika mashamba ni kwamba mashamba mengi ya wakfu yamechukuliwa na wananchi, lakini wananchi hao wamekaa siku nyingi miaka na miaka wameshajenga, lakini bado lile ni eneo la wakfu. Kwa hivyo, yule aliyejenga pale bado ana dhima. Utaratibu tumeshafanya wa kuwaita watu kuwaelimisha haya na tunakubaliana namna gani ya kuwaondoshea dhima ile kwa watu wale na vizazi vyao. Na kesi ya Mtoni kwa mfano Pemba, tuna kesi hapa ya Mfenesini ambayo karibu nayo

tutaimaliza na sehemu nyengine kama hizo. Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa Wajumbe waelewe tu kwamba kweli matatizo haya yapo, lakini tunayashughulikia kila yanapotokea.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa ni suala la Bwana Abdulrahman Bakari Rashid. Huyu Bwana Abdulrahman Bakari Rashid ni mwananchi wa Jimbo la Mhe. Salmin Awadh Salmin. Tatizo Mhe. Spika, kwa wananchi wetu ni kwamba ama ni waongo wanaarifu Waheshimiwa visivyo au wanataka kila kitu kifanywe kwa sababu yeye tu kaleta malalamiko yake na hivyo haiwezekani.

Mhe.Spika, huyu Ndugu Abdulrahman Bakari Rashid alikuwa na kesi kuanzia 2004 Mahakamani na tatizo ni kwamba alikuwa anadaiwa, alikopa shilingi milioni moja na laki tano wakati huo na yeye mwenyewe akasema kama sikulipa banda langu la nyumba liuzwe. Sasa bahati nzuri hakushtakiwa kwa wizi wa hadaa, maana yake huyu ni mwizi wa hadaa, lakini hakushtakiwa hivyo au ni mwizi baada ya kuaminiwa, lakini yote hakushtakiwa hivyo.

Huyu aliyekopesha akataka pesa zake tu na akasema kwamba basi hili banda madhali tulikubaliana liuzwe, mimi nina-*apply* Mahakamani liuzwe. Likauzwa banda hilo wakati huo, lakini baada ya kuuzwa, *of course process* zote za Mahakama zikachukuliwa mpaka kuweka *notice* pale. Lakini huyu kila ikiwekwa ipokuwa ikiwekwa *notice* alikuwa haji na haendi Mahakamani, alikuwa hatoi taarifa yoyote na alisema kwamba yupo Dar-es-Salaam. Lakini kwenye nyumba ile watoto wake wapo na watoto wakaulizwa kwa mujibu wa *proceedings* hizi, wakasema kwamba wao waliona na wakamuarifu.

Sasa Mahakama ikaendelea kutoa *expert judgement*. Baada ya kutolewa ndio tena yeye akaja, lakini wakati huo alipokuja ni karibu 2008, akenda Mahakamani akaambiwa akate rufaa hivyo hivyo *out of time*, akakata rufaa ikafika kesi kwa Jaji wa Mahakama Kuu Jaji Mshibe na yeye akaamua kutokumpa haki huyu Abdulrahman Bakari Rashid.

Sasa baada ya hapo akakaa mpaka 2012, miaka minane baadae akaja ofisini kwangu kwa mara ya mwanzo, akanielezea na aliponielezea, hizo mbwembwe alizotia ni za kutisha. Akajifanya yeye ni mtu *official* kabisa, naomba nihifadhi hiyo ofisi ambayo alisema anafanya kazi na alikuwa anasema hana nafasi huko Dar-es-Salaam. Lakini Mahakamani imeshaekwa ile *notice* watoto wake wapo na alipokuja ofisini kwangu akafanya hivyo hivyo kwamba yeye ni mtu mkubwa labda nimuogope.

Mimi nikamsikiliza yote tarehe 19 Novemba, 2012 nikamwandikia barua hii hapa, nikamwandikia barua kubwa kumuelezea. Mwisho nilimuandikia *points* tatu hizi kwamba kesi yake ilianza tarehe 19 Januari, 2004 na kutolewa hukumu tarehe 21 Oktoba, 2005. Baada ya maamuzi hayo akakata rufaa Mahakama kuu na maamuzi hayo ya Jaji Mshibe alisisitiza rufaa yake na yeye akatoa maamuzi, maamuzi hayo hayakumridhi kwa sababu rufaa yake ilikataliwa.

Hapo akenda tena kumuona Jaji Mkuu, akaambiwa basi omba *revision*, hakuomba. Sasa baada ya hapo akakaa mpaka dalali wa serikali alipokwenda kuuza nyumba, ikauzwa nyumba na pesa zile zote zikalipwa huyo aliyekuwa akimdai, na yeye akanyamaza kimya kwa muda wa miaka minane akaja 2012 ofisini kwangu na mimi nikamwambia hii imeshapitwa na wakati. Kwa hivyo, hii kesi haipo tena, ndio barua yangu niliyomuandikia hiyo.

Mwaka 2013 akakaa karibu mwezi wa Julai akaja tena ofisini kwangu kwa kesi hiyo hiyo. Mimi nikamueleza yote, baada ya kumueleza akasema basi naomba angalau zile pesa zangu zilizobakia katika mauzo nipewe mwenyewe. Nikamwambia sasa pesa hizo miaka minane hiyo iliyopita tutazipata vipi? kwa nini hukueleza huko mwanzo. Lakini *still* mimi kibinadamu nikamwambia basi subiri nitafute.

Kumbukumbu Mhe. Spika, za miaka nane Mahakamani unajua ni taabu kuzipata, lakini hata hivyo ili kumsaidia huyu mwananchi tarehe 26 Novemba, 2013, mimi nikaandika barua Mahakamani, hii hapa barua ipo kuomba hizo kumbukumbu za miaka hiyo tuzipate, tutizame iliuzwa kiasi gani hiyo nyumba na pesa gani zilizobakia, kama zimebakia na zilikwenda wapi.

Mahakama nikawapigia simu wakasema Mheshimiwa kumbukumbu hizi ni taabu kuzipata miaka yote hiyo. Lakini wacha tuzitafute, zikatafutwa mpaka tarehe 15 Julai, 2013 nikawaandikia tena kuwakumbusha ili tupate hizo kumbukumbu na tutizame iliuzwa kiasi gani. Bado kumbukumbu hizo zinatafutwa, miaka minane ni mingi na *filing* yetu unaijua.

Huyu alikuja mara tatu ofisini na yote hayo niliyoeleza nikamwambia, mbali ya barua, mbali ya kumbukumbu kwamba zinatafutwa tukizipata tutatizama njia gani ya kumsaidia ingawa *file* limeshafungwa, kesi imeshafungwa.

Sasa mimi ninasikitika sana kwamba yeye kenda kumwambia mwakilishi labda kamwambia kwamba hatushughuliki na nini. Lakini kushughulika yenyewe anajue kwamba hiyo kesi yake hivi sasa imeshafungwa tokea miaka

hiyo, ni miaka minane na *correspondents* zote zipo hizi tulizompa yeye na tulizopeleka Mahakamani.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi ninachopenda kusema ni kwamba bado kibinadamu, bado mimi nitaendelea kutafuta hiyo kujua kiasi gani fedha zake kama zipo zilibakia katika kuuzwa hiyo nyumba na baada ya kulipwa huyo aliyekuwa anamdai, kama zimebakia, basi bado sisi tutazitazama na kama zipo kwa ushahidi ambao tutapata tutampa mwenyewe.

Ni vyema kwa kesi kama hii Mhe. Spika, huyu Abdulrahman Bakari Rashid akastahamili kwa sababu si kitu cha kwenda tu kuchukua katika kumbukumbu hizo, ni lazima zitazamwe na halafu sisi tukishakuzipata ndio tutamjibu ipasavyo. Kwa hivyo, ninachosema ni kwamba Ndugu Abdulrahman Bakari Rashid tulimwambia yote haya na bado hivi sasa tunatafuta hizo kumbukumbu hizo, fedha ni kiasi gani, kama zipo pesa zake mimi ninahakikisha kwamba tutampa na kama hazipo tutamwambia zilitumiwa kwa njia gani na njia gani, au kama hilo banda lililouzwa wakati huo lilikuwa halifiki au linafika.

Na kwa taarifa Mhe. Spika, banda hilo baada ya kufuatilia hivi sasa limeshauzwa mikono kiasi mitatu. Baada huyu aliyeuziwa naye akauza na huyu aliyenunua naye akauza, tena baadae likatengenezwa kuwa nyumba kamili. Sasa yote hayo tumeyafuatilia. Kwa hivyo, ni kesi ambayo kidogo ni *complicated* na hatuwezi tu kwa sababu yeye anataka apewe hizi fedha wakati mimi sizijui ni kiasi gani mpaka nifanye uchunguzi wa kutosha ili niweze kusema kwamba tumpe au tusimpe na kwa utaratibu gani.

Mhe. Spika, kisheria unajua kesi yake imeshamaliza kwa sababu *limitation decree No. 12* inasema kwamba ikifika miaka miwili hujadai basi ndio basi, lakini ni miaka minane na sisi bado tunaendelea kumsaidia. Tutaendelea kumsaidia mpaka hapo tutakapopata ufumbuzi.
Mhe. Spika, baada ya kusema hayo...

UTARATIBU

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, haelezi hasa madai ya yule Ndugu Abdulrahman Bakar Rashid. Anachodai Ndugu Abdulrahman Bakar Rashid ni kwamba nyumba yake imeuzwa shilingi milioni nane, alichokuwa akidaiwa milioni moja na nusu, anachotaka ni pesa zake zilizobakia apewe mwenyewe.

Suala la kusema kumbukumbu za miaka minane katika Mahakama hazionekani, ndio yale tuliyozungumza jana kwamba miaka minane ni

kidogo. Chombo kama Mahakama hakiwezi kusema toka muda huo inatafuta kumbukumbu za madai. Linaloonekana pale kwa Mahakama kwamba zile pesa zake wamezila na wanababaisha.

Kwa hivyo, hoja yangu ni kwamba Mhe. Waziri, bado una muda mpaka kufika mwezi wa kati wa bajeti, itakapofika wakati wa bajeti kama suala hili halitojulikana ninaendelea kukwambia nitatoa kifungu katika mshahara wako ili uone uchungu wa kudhulumiwa. Hiyo ndio taarifa yangu. (*Makofi)*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Maelezo niliyosema ni haya. Mimi nilisema kwamba hii nyumba iliuzwa na tunajaribu kutafuta kiasi gani ambazo pesa zile zimo na zimebakia. Hicho ndicho tutachotafuta.

Kumbukumbu zote hizi ndivyo tunavyofanya. Sasa sifikirii kama sikusema hayo, mimi nilisema kwamba nyumba iliuzwa na kuna fedha zilizozidi na hizi ndio ninazozitafuta mimi, miaka minane toka mwaka 2004, ndio ilipouzwa. Miaka minane hiyo lazima tu-*check* kule.

Mhe. Spika, nikasema bado hili nitaendelea kulitafuta. Sasa maelezo yangu ni hayo. Sina maelezo mengine kwa hivi sasa hapa mpaka hapo nitakapopata taarifa kutoka Mahakamani.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, mimi ninapenda nirejee tena kusema kwamba yale yote ambayo yamezungumzwa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, sisi tutayachukua na tutayafanyia kazi na ninaamini katika kikao kinachokuja *inshaallah* tutaripoti katika misingi ya maelezo ambayo yametolewa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Spika, ninakushukuru.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri, kwa majibu hayo na sasa ni wakati muafaka ingawa tumechelewa kidogo kumkaribisha Mhe. Mwenyekiti wa Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Ussi Jechi Simai (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kutoa ufafanuzi baadhi ya michango ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu. Lakini pia kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya maagizo ambayo yalitolewa na kamati yangu hii kipini cha mwaka jana.

Mhe. Spika, awali ya yote kwa niaba ya Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala, tunapokea pongezi tulizopewa na Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali ambao wametupa, lakini vile vile na sisi tutoe pongezi zetu kwa

Waheshimiwa Wajumbe kwa kuchangia kazi yetu hii, lakini pia kwa Waheshimiwa Mawaziri kwa kazi njema walizozifanya kwa kuyatekeleza maagizo mengi kabisa na kuyaacha machache. Kwa hivyo, tunakupongezeni sana Waziri muliomo katika chini ya Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Spika, katika maagizo yaliyotolewa mwaka jana, nianze na Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa wakati huo, kulikuwa na agizo Nam. 1. Mhe. Spika, agizo hili lilikuwa ni kwamba kamati iliagiza wizara kukutana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa wakati ule ili kuwasaidia JKU katika bonde la Kwapweza kule Pemba waweze kupata maji katika bonde hilo, ili waweze kuendeleza kile kilimo chao cha kumwagilia maji.

Mhe. Spika, utekelezaji wa agizo hili sikubaliani nao kama mimi kama ni mwenyekiti. Utekelezaji wake ni mbovu, yaani hadi hivi sasa mwaka mzima Mhe. Spika, kwamba lile tendo la kukutana tu Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati basi wanakwambia kwamba wizara inaendelea kuzitafuta taasisi nyengine, kukutana tu, basi angalau wangetwambia tulikutana nao. (*Makofi*).

Sijui Mhe. Spika, kuna tatizo gani ama tuseme kwamba labda pengine hawa Mawaziri hawafamiani na wanaogopana, kwa sababu naona hizo wizara hazipo mbali kiasi hicho. Wizara zote zipo Unguja. Kwa hivyo, Mhe. Spika, agizo hili bado ninasisitiza kwamba kuna haja wizara mpya ikutane na Wizara ya Makaazi, Maji na Nishati kwa ajili ya kuona kwamba wanatatua namna gani suala hili la kuwapatia maji wale watu wetu wa JKU katika bonde la Kwapweza ili waweze kutatua matatizo yao ya kilimo.

Mhe. Spika, vile vile, kuna agizo Na. 8 katika wizara hii. Pamoja na majibu yaliyotolewa katika agizo Na. 8, kamati inasisitiza umuhimu wa Idara ya Zimamoto na Uokozi kupatiwa vifaa vya kutosha na vya kisasa pamoja na ofisi katika maeneo ya bandarini pamoja na uwanja wa ndege kutokana na umuhimu wake.

Majibu yaliyotolewa tumeyaona, lakini umuhimu wa sehemu hizi tumekwenda na tumeona hali iliopo pamoja na kusema kwamba wizara imetafuta vifaa, vifaa hivyo havitoshi kutokana na umuhimu wa maeneo hayo Mhe. Spika.

Vile vile, kuna agizo Na. 9 kuhusiana na matengenezo ya jengo la uwanja wa ndege Pemba. Mhe. Spika, katika agizo hili wizara wametwambia wamezungumza na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na wakasema kama

watalijenga lile jengo ili liweze kuwasaidia wale Idara ya Zimamoto na Uokozi katika Kiwanja cha Pemba.

Tunasisitiza kwamba bado wawasiliane na walitatue tatizo hili kutokana na kuona kwamba idara hii imetupwa kiasi fulani na ndio yenye umuhimu mkubwa kabisa katika maeneo ya uwanja wa ndege pamoja na bandarini. Mhe. Spika, tunaomba hili lifuatiliwe na baadae huko mbele tuje tupate majibu wamefikia wapi. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kuna agizo Na. 1 ambalo Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma. Mhe. Spika, kamati yangu haikuridhika na agizo Na. 1 ambalo tumetoa. Ninakumbuka katika kikao cha bajeti kwenye *hansard* ya tarehe 3 Julai, 2013, Mhe. Spika, ninakumbuka siku hiyo wewe ulikuwepo katika kiti chako hicho hicho cha enzi na ulikuwa umekikalia na tukakubaliana katika Baraza hili kwamba wizara hii basi ikae na kamati iwapatia ile *breakdown* ya matumizi ya fedha za mradi wa *e-government*. Tulikubaliana hivyo Mhe. Spika, lakini vile vile serikali inawajibika kwa pamoja kuna *collective responsibility*.

Hapa mradi huu unauhusisha wizara tatu; kuna Wizara ya Fedha, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Wizara ya Utumishi wa Umma. Basi kilio cha Waheshimiwa siku zote wanalalamika juu ya suala hili, basi hata wizara moja isilete zile *breakdown*.

Mhe. Spika, hili siridhiki nalo na kwa niaba ya kamati yangu pamoja na Waheshimiwa Wajumbe, ninasisitiza tena ipo haja ya kuundwa Kamati Teule kuchunguza suala hili, kwani siku zote tumekuwa tukipigwa danadana kwa hili, kwa nini kuna ugumu gani kuleta karatasi yenye maandishi ambayo inayoonesha mtiririko wa fedha, jambo hili liwe gumu. Hapa Mhe. Spika, ninasisitiza tena ipo haja inaonekana kuna kitu kinafichwa hapa, tunataka uwazi tuambiwe. (*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya uzungumzaji wa maagizo hayo takriban manne ambayo kamati yangu haijaridhika nayo, sasa ni vyema tukaingia katika kutoa ufafanuzi baadhi ya michango ya Waheshimiwa Wajumbe wako.

Mhe. Spika, niendelee tena kuwashukuru Wajumbe wengi hasa ambao wamechangia katika ripoti yeti hii ya kamati, lakini pia niendelee kuwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wote watatu kwa ufafanuzi mzuri ambao umenisaidia sana katika kutoa ufafanuzi wangu ambao hautokuwa mkubwa sana kutokana na wao kuyachambua baadhi ya mambo mengi sana ambayo ni muhimu na ndio ambayo yaliyowagusa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu hili. (*Makofi*).

Mhe. Spika, jumla ya Waheshimiwa Wajumbe ambao wamechangia katika ripoti yetu ni Wajumbe 21, 17 walichangia kwa maelezo ya kusema na 4 walichangia kwa maandishi. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba muwatambue Waheshimiwa Wajumbe ambao wamechangia ripoti yetu hii:

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2.Mhe. Hamza Hassan Juma
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
4.Mhe. Suleiman Hemed Khamis
5.Mhe. Wanu Hafidh Ameir
6. Mhe. Salmin Awadhi Salmin
7.Mhe. Asha Bakari Makame
8.Mhe. Mgeni Hassan Juma
9.Mhe. Abdalla Mohamed Ali
10.Mhe. Bikame Yussuf Hamad
11.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
12.Mhe. Mohamed Mbwana
13. Mhe. Mohamed Haji Khalid
14. Mhe. Marina Joel Thomas
15.Mhe. Mahmoud Muhamad Mussa
16.Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum SMZ
17.Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe watatu walichangia kwa maandishi. Nao ni:-
1. Mhe. Panya Ali Abdalla
2.Mhe. Fatma Mbarouk Said
3.Mhe. Kazija Khamis Kona.

Mhe. Spika, baada ya kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe ambao wamechangia na wametusaidia sana na wamewasaidia Waheshimiwa Mawaziri katika kutoa ufafanuzi wa masuala mbali mbali yanayohusu taasisi ambazo wanazisimamiwa wao pamoja na sisi kama Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Spika, katika idara zilizochangiwa kwa kiasi kikubwa sana na kwa hisia kali ambazo Waheshimiwa Wajumbe wamezionesha miongoni mwao ni Idara ya Mahakama na mimi ninaona ni vyema nikaanza hapa. Pamoja na yote kwanza ninapenda nipongeze Idara ya Mahakama kwa kufanya kazi licha ya kwamba kuna changamoto nyingi zinazowakabili wao kwa upande wa serikali, lakini pia zile changamoto ambazo zinakabili wao kama ni watendaji wa Mahakama.

Mhe. Spika, ninaipongeza Idara ya Mahakama kutokana na kwamba tulipotembelea katika baadhi ya Mahakama tumeona kwamba kuna upungufu hivi sasa angalau umepungua zile kesi, ule mrundikano wa kesi umepungua. Kwa hivyo, inaonekana kwamba wanafanya kazi licha ya kwamba kuna changamoto nyingi na matatizo ambayo yanawakabili wao.

Mhe. Spika, vile vile, kwamba matatizo ya vifaa katika Mahakama zetu tumeyaona na Mhe. Waziri, amezungumza, yale tuliyoyazungumza hata karatasi za wito zilikosekana katika baadhi ya Mahakama, haya ni kweli na Mhe. Waziri amekiri. Nimpongeze Mhe. Waziri, kwa kukubaliana na ukweli huu, kwani kamati yetu ilifanya kazi kubwa ya kufanya uchunguzi wa kina, lakini pia ilipata msaada mkubwa kutoka kwa watendaji wa wizara hii ambao walifanikisha kazi hii.

Mhe. Spika, nizungumze suala jengine la rufaa ambayo yamezungumzwa hapa na Mheshimiwa amefafanua, tunajua kwamba rufaa zina taratibu zake. Kamati ilisisitiza jambo la muhimu katika rufaa kwamba ni kufuata taratibu za utoaji, sio rufaa, ni *bail* tunaita ambayo ni dhamana, utoaji wa dhamana hatukuzungumza kwamba hii si haki ya msingi.

Hii ni haki tunaijua ya mtu kupata dhamana, lakini tulichosisitiza sisi ni taratibu za kutoa hiyo dhamana ambapo tumepata maelezo kwa wadau wengi wanasema kwamba dhamana zinatolewa kama kwamba kuna biashara ambayo inafanywa, watu wanatoa dhamana kwa ajili ya kupata kipato.

Mhe. Spika, kwa hivyo, sisi tunaendeleza kusisitiza kwamba Mahakama ni chombo kimoja muhimu sana, wananchi wa Zanzibar wanategemea Mahakama ambalo ndio kimbilio lao la kupata haki zao. Kwa hivyo, tunawasihi watendaji wa Mahakama kwamba waache tabia chafu ambazo zinatia aibu Mahakama zetu. Mahakama ni chombo ambacho kinaheshimika sana na kina uhuru mkubwa sana katika kufanya kazi zake Kikatiba.

Jengine lililozungumzwa hapa masuala ya hukumu ambazo zilizokuwa zikitolewa kinyume na utaratibu, nalo hili tumeliona. Masuala kama haya Mhe. Spika, yanapatisha taabu sana Idara ya Muendesha Mashtaka (*DPP*) kutokana na kwamba wao wanahangaika sana kutafuta kesi, wakipeleka kule, tukizingatia kwamba kesi za jinai ni kesi ambazo zipo dhidi ya serikali, zina *interest* na serikali, lakini kesi hizo zinapotea katika mazingira ambayo hayaeleweki. Kwa hivyo, jambo hili tuache kwa sababu sisi sote tunaitumikia serikali hii na wananchi hawa hawa, tunaitia serikali hasara tunapozipoteza kesi kwa makusudi.

Mhe. Spika, katika eneo hili kuna mambo mengi sana ambayo Waheshimiwa wamechangia, lakini pia Mhe. Waziri, ametoa ufafanuzi. Tuelekee katika eneo jengine kuhusu Tume ya Kurekebisha Sheria. Mhe. Spika, Tume ya Kurekebisha ni taasisi moja muhimu sana tunajua kwamba sheria nyingi zimefanyiwa marekebisho na pia bado zipo nyengine zinahitajiwa kufanyiwa marekebisho hayo.

Tatizo liliopo kule Mhe. Spika, bajeti hii ambayo wanaingiziwa katika Tume ya Kurekebisha Sheria ni bajeti moja ndogo mno haiwezi ikafanya kazi zao ngumu kutokana kwamba katika kurekebisha sheria kuna mchakato mkubwa, kuna wadau, kuna wananchi wa kawaida wanatakiwa wafikwe, lakini vile vile, waweze kutoa maoni yao sio jambo dogo.

Jengine hapa ukosefu wa ofisi ya kudumu, lakini ile waliyonayo waliyokodi nayo pia ina matatizo. Hivi karibuni tumeshuhudia kwamba lile jengo lilidata na wafanyakazi mule wakatolewa katika sehemu nyengine. Kwa hivyo, tunaiomba serikali ishughulikie suala hili wapatiwe jengo jengine angalau lile lililotajwa la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, basi angalau wangelipewa.

Mhe. Spika, katika eneo hili Wajumbe wengi sana wamechangia kama Mhe. Makame Mshimba Mbarouk , Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Wanu Hafidh Ameir ambaye ni mjumbe wa kamati na Waheshimiwa wengine.

Mhe. Spika, vile vile, kuna hii Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ambapo Wajumbe wengi wamechangia kwa hisia kali. Moja ni tatizo la maslahi madogo ambalo Mhe. Waziri, amelizungumza hapa kwamba wamo katika utaratibu wa kuwafanyia maslahi yao kidogo angalau yaongezeke.

Mhe. Spika, ofisi hii inakabiliwa na tatizo la usafiri ambapo waendesha mashtaka wanashindwa kufika kazini kwao kwa wakati, kule ambapo wanakwenda kushughulikia masuala ya kesi. Kwa hivyo, tunaiomba serikali ifanye utaratibu wa kuwapatia angalau ile gari; kigari chao kile kibasi kidogo tulipofika katika kamati wakati ule kilikuwa ni kibovu. Kwa hivyo, tunaiomba wasaidiwe hawa wapate angalau usafiri wa kuweza kuwarahisishia kazi zao.

Jengine Mhe. Spika, kuna tatizo la ofisi katika Mahakama zetu ambapo mawakili hawa wa serikali wanapata shida katika kufanya kazi zao. Tumeshuhudia mahakama ya Mfenesini, kuna siku waendesha mashtaka walikuwa wanamuhoji shahidi katika gari, walishindwa kabisa kupata nafasi ya kuweza kufanya kazi zao, wanafanya kazi katika mazingira magumu na yasiyostahiki kabisa kutokana na hadhi na sifa walizonazo waendesha mashtaka wetu.

Mhe. Spika, tunaomba serikali ifanye jitihada zake zote, hawa ndio watu muhimu ambao wana maslahi makubwa sana serikalini kutokana na kwamba wao ndio washtaki. Kesi za jinai kama tulivyosema ni kesi ambazo zinahusiana na serikali moja kwa moja.

Mhe. Spika, eneo jengine tuangalie katika Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma. Nizungumzie katika Idara ya Nyaraka, ambapo eneo hili limegusa hisia sana za Waheshimiwa Wajumbe, pamoja na Waheshimiwa Mawaziri. Mhe. Haji Omar Kheri jana alikiri kutokea kwa wizi huu, lakini tukiacha wizi tuzungumze mambo mengi tu ambayo changamoto zilizopo katika idara ile.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe waliochangia hapa ni Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Hamza Hassa Juma, Mhe. Wanu Hafidh Ameir na Waheshimiwa wengine wengi walichangia katika maeneo haya. Idara ya Nyaraka kama nilivyozungumza katika hotuba yangu kwamba ni idara moja muhimu sana, ukizingatia kuwa urithi wetu wa kale upo pale, lakini urithi wa kale ndio unaoleta urithi wa leo Mhe. Spika.

Kwa hivyo, tukumbuke kwamba changamoto nyingi zilizopo pale, tumeshuhudia vitu vya taasisi ya serikali. Huu ni ukweli Mhe. Spika, vimefungwa kamba kwa ubovu, sio kwamba visikimbie, ni kwa sababu ya ubovu na mtendaji wa serikali aweze kukaa pale.

Mhe. Spika, hawezi kukaa pale, hii ni aibu kubwa sana. Sisi kama sio kuona kuwa tungefanya vibaya kwa serikali yetu, basi tulikuwa tuko tayari kwenda kununua viti angalau vile vya mbao tukaenda kuwawekea wale wafanyakazi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tunasisitiza kwamba vifaa pale hakuna. Nadhani mimi kwa kiti kile hata sijazaliwa na wala sijafikiriwa kuwepo. Nafikiri vinafanana na hizo kumbukumbu zilizoibiwa kwa huo uzamani wake. Mhe. Spika, hii ni hatari.

Pia kuna tatizo la mazingira mabovu mno Mhe. Spika, ambapo wafanyakazi wale wanafanya kazi, hakuna hata kifaa kimoja cha kuweza kuwasaidia angalau kunusuru afya zao. Wafanyakazi wale wanafanya kazi kama watumwa na utumwa nchi hii umeondoka, wale ni wafanyakazi wa serikali, kwa hivyo wathaminiwe.

Kwa hivyo, tunaiagiza tena wizara inayohusika na tunatilia mkazo, kwamba tutakapofika katika bajeti ijayo tukaona kwamba idara ile bado haijaleta mabadiliko yoyote, Mhe. Spika, hatutoiachia serikali sijui imuwajibishe mtu, hapana, tutaiwajibisha serikali kwa kuzuia moja kwa moja fungu zima la

wizara, halafu serikali itajua wapi ikatafute pesa, au kama itawapa kwa ubabe, kwa nguvu kwa sababu kwa uwezo, basi itawapa, lakini mimi kama Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wangu tumekubaliana na Waheshimiwa Wajumbe nawaombeni, muje muniunge mkono ili tuzuie moja kwa moja bajeti ya wizara hii.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo katika ripoti yangu na katika hotuba yangu nilisisitiza, ni suala la ukaguzi wa nyaraka mara kwa mara. Nilikuta kuna tatizo ambapo nyaraka zile ukaguzi wake naona kama haupo, kwa sababu nyaraka zilizoibiwa mule ni nyingi na kwa muda. Kama kungekuwa kuna ukaguzi unafanywa basi watu wangebaini na wangeweza kuepukana zaidi na tatizo lile, lakini inaonekana kuwa lile gofu limetupwa pale.

Kwa hivyo, hakuna mtu ambaye anaweza kuuliza masuala ya zile nyaraka yanakwenda vipi. Mhe. Spika, mimi niseme tu kwamba nyaraka zile ni zetu sisi Wazanzibari na tunazitaka na zina umuhimu mkubwa sana kwetu sisi.

Jengine Mhe. Spika, nizungumzie kuhusu suala la wizi wa nyaraka katika eneo hili. Mhe. Spika, nasema tena kwamba kamati yangu inasikitishwa pamoja na Waheshimiwa Wajumbe ambao wamechangia kwa hisia kali, inaonekana kwamba wanasikitishwa sana na wizi wa nyaraka uliotokea pale. Sitaki kupingana na kaka yangu Mhe. Haji Omar Kheri kwamba *CCTV camera* sio chanzo cha wizi, lakini zingetusaidia sana katika kupunguza hilo tatizo la wizi.

Mhe. Spika, mimi nasisitiza tena kwamba ipo haja ya kupelekwa kwa haraka *CCTV camera*, nyaraka nyengine bado zipo. Mwenyezi Mungu akitujaalia Mhe. Spika, akikubali kuundwa kwa kamati teule na atakubali kutokana na maombi ya Wajumbe wengi, basi tutakwenda kuona zile nyaraka ambazo zimepotea au zimeibiwa kwa makusudi. Mimi nasema zimeibiwa kwa makusudi. Mhe. Spika, *CCTV camera* ingesaidia sana, bado tunaendelea kutoa agizo hili kama kamati, *CCTV camera* itafutwe na zibandikwe pale ili zipunguze matatizo ya baadae.

Mhe. Spika, mimi nakubaliana na Waheshimiwa wengi waliochangia akiwemo Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Ismaili Jussa Ladhu, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Salmin Awadh Salmin na Waheshimiwa wengine wengi ambao walichangia katika eneo hili la kuundwa kwa kamati teule.

Mhe. Waziri alipokuwa akijibu hapa baadhi ya hoja zile alipokuwa akitoa ufafanuzi, alizungumza sana kwa kusema kwamba ziko taasisi nyengine za serikali ambazo zinafuatilia masuala haya, sisi hatukatai. Lakini Mhe. Spika,

tunataka tutumie kifungu cha 117 cha kanuni zetu, kwamba na sisi tuna mamlaka au uwezo wa kuweza kuunda kamati teule kwa ajili ya uchunguzi. Serikali kwa upande wao watachunguza na wao, lakini sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao ndio tunawabeba wananchi, mimi nahisi tuna wajibu wa kwenda kuangalia katika eneo hili. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nakuomba ukubaliane na wazo letu la kuundwa kwa kamati teule, ili tuisaidie kazi serikali Mhe. Spika.

Mhe. Spika, vile vile kuna masuala mengine katika Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma, kuhusu suala la uongezaji wa mishahara. Suala hili limelalamikiwa sana na Waheshimiwa Wajumbe, kwa kweli mpaka hivi sasa pamoja na serikali kuweka utaratibu, inaonekana bado halijakamilika. Kwa hivyo, tunaiomba serikali izitengeneze hizi taratibu, hasa ikizingatia mishahara isiyofanana kabisa kwa baadhi ya watumishi wa umma, katika ripoti yangu nilizungumza sana na nikaelezea suala la wanasheria wetu wa serikali. Kwa mfano Idara ya Mashtaka, Idara ya *DPP*, yaani tumezungumzia mahakama, tumezungumzia hii Tume ya Kurekebisha sheria kuna tofauti kubwa Mhe. Spika, tukiangalia kazi zao zinafanana. Kwa hivyo, suala hili nalo bado serikali ina wajibu wa kulishughulikia, ili kuondosha matatizo ya watendaji kuhamiahamia na kuhamahama katika maeneo mengine ya taasisi za serikali.

Mhe. Spika, nikija katika maeneo mengine, niangalie katika Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, nitaanza na Idara ya Zimamoto ambayo nimezungumza kule katika maagizo.

Mhe. Spika, Idara ya Zimamoto ina matatizo makubwa sana, hasa ya vifaa na idara hii ndio muhimu sana katika masuala ya uokozi na uzimaji moto. Tunasisitiza tena kuwa wapatiwe vifaa, pamoja na mambo mengine yanayowahusu wao.

Kwa ujumla Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala, nizipongeze idara zote za SMZ kwa kufanikisha vyema Sherehe za Mapinduzi, lakini vile vile kwa kufanya kazi nzuri ya ulinzi na usalama katika nchi yetu.

Mhe. Spika, Idara ya KMKM wao hasa tuwapongeze kwa ujenzi wa hospitali nzuri ambayo tulikwenda na tukaiona, lakini pia imejengwa kwa fedha kidogo sana, tukilinganisha na majengo mengine ya serikali. Kwa hivyo, tunawapongeza kwanza kwa utumiaji mzuri wa fedha katika eneo hili, nasema katika eneo hili la ujenzi wa hospitali hii, hapa ni muhimu sana.

Mhe. Spika, tunaiomba serikali kwamba hapa pana matatizo mengi ya vifaa. Hospitali hii Mhe. Spika, ni muhimu sana kutokana na kwamba ina sehemu za *VIP*, Waheshimiwa wakipata matatizo wanaweza kwenda pale. Lakini kwa sasa hawawezi kupelekwa pale, watapelekwa Hospitali ya Mnazi Mmoja kutokana na hospitali ile vifaa hakuna. Kwa hivyo, tumeiomba serikali iwaingizie fedha ili wapate baadhi ya vifaa pamoja na majiko, madawa na mtambo wa *ICU*.

Mhe. Spika, kuhusu Chuo cha Mafunzo ambacho kinakabiliwa na matatizo mengi. Suala hili lilizungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi, siwezi kuwataja wote, lakini wamechangia wengi. Changamoto kubwa iliopo ni mrundikano wa mahabusu ambapo wanapata bajeti ndogo sana. Mahabusu Mhe. Spika, hawana siku ambayo wanaaga wanafika kule. Nchi yetu kama tunavyoona mara yanatokea machafuko hapa, kwa hivyo askari wanawakamata watu wanawapeleka kule.

Kwa hivyo, kuna haja kubwa ya kuongezwa bajeti hasa ya chakula kwa wale wanafunzi pamoja na mahabusu. Vile vile Mhe. Spika, tunaiomba wizara ama serikali kuwaongezea eneo lile la jirani pale Chuo cha Mafunzo, ili waweze kuendeleza miradi yao ya ujenzi wa maduka.

Mhe. Spika, Kikosi cha Valantia kina matatizo ya mabweni ya kulala maaskari pamoja na matatizo mengine, tunaomba serikali waangalie. Ukisoma ripoti yetu pamoja na ile hotuba kuna mambo mengi ambayo yamezungumzwa.

Mhe. Spika, tunawapongeza JKU na wao kwa kujenga skuli yao pale, ambayo itasaidia sana katika masuala ya kuwaondoshea matatizo vijana wetu, hasa ya kupata taaluma ya ufundi ambapo serikali yetu inahimiza sana wananchi kuweza kujiajiri wenyewe.

Mhe. Spika, tulitembelea baadhi ya halmashauri na nyengine tulipata taarifa zao tukiwa katika kupokea taarifa ya utekelezaji ya Mhe. Waziri.

Halmashauri ya Magharibi inakabiliwa na matatizo kama vile ya gari, hawana gari na pia kuna tatizo la Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini A, ambapo utekelezaji wa bajeti haujaturidhisha sisi kama Kamati. Halmashauri ambayo ina maeneo mengi ya kuweza kukusanya mapato, lakini la kusikitisha hadi hivi sasa mpaka tunatoka kwenye kamati ni asilimia 25 tu ambayo ni utekelezaji wa bajeti yake. Mhe. Spika, tunaiomba serikali na wizara kufuatilia suala hili ili kuona ni matatizo yepi yanayoikabili halmashauri yetu hii.

Mhe. Spika, vile vile Baraza la Manispaa limezungumzwa na baadhi ya wachangiaji. Kwanza kwa niaba ya kamati nichukue fursa hii kuipongeza manispaa kwa kufanya usafi, hasa tulipokuwa tunaelekea katika sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi, walizidi kujitahidi. Kwa hivyo, kamati yangu inaendelea kusisitiza kwamba waendelee na utamaduni huo wa kufanya usafi kila pembe ya maeneo ya mji wetu, ili kuweza kuleta ile haiba ya mji wetu.

Jengine Mhe. Spika, Mhe. Waziri jana alipokuwa akitoa ufafanuzi alisema kwamba Wazanzibari sasa hivi tumekuwa na tabia mbaya ambayo sijui tumerithi wapi ya uchafu! Kwa hivyo, wananchi tuwe tunatunza mazingira yetu, lakini pia tuwe tunafanya kazi za usafi katika maeneo ambayo yanatuzunguka ili tuwapunguzie kazi hawa watu wetu wa manispaa.

Mhe. Spika, mwisho kabisa napenda niwashukuru tena Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia ripoti yangu, Waheshimiwa Wajumbe wa kamati, Waheshimiwa Mawaziri, makatibu kamati wangu, pamoja na makatibu wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC), katibu wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano makubwa ambayo wamenipa nilipokuwa nikifanya muhtasari wa hotuba yangu pamoja na kamati.

Pongezi za mwisho zikuendee wewe Mhe. Spika, kwa kuniruhusu, lakini pia kwa kuliongoza vyema Baraza letu hili. Mhe. Spika, baada ya hayo machache naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa majumuisho hayo machache, lakini yamechukua muda mrefu kidogo, na nia na madhumuni ilikuwa ni kujaribu kujibu zile hoja mbali mbali ambazo Waheshimiwa Wajumbe wamezitoa.

Waheshimiwa Wajumbe katika ripoti hii ya kamati pamoja na ripoti za utekelezaji, kuna mambo mawili makubwa ambayo Waheshimiwa Wajumbe wanaonekana, pamoja na Mhe. Mwenyekiti hawakuridhika.

Jambo la kwanza ni lile la Mhe. Salmin Awadh Salmin ambalo kuna mwananchi wake. Suala hili naelekeza kwamba tumpe Waziri kwa sababu hili liko kwenye mtiririko wa utawala wa mahakama na kimsingi mtiririko huo ulimalizika. Kwa bahati nzuri sitaki nikatae kwamba huyo ndugu amehangaika sana, hata kwangu amefika na nikamwelekeza kwamba hili ni jambo la mahakamani kwa hivyo rudi mahakamani, kama shughuli zote zimemalizika basi muone Mhe. Jaji Mkuu yeye ndio kiongozi wa pale, atakupa maelekezo ya nini cha kufanya. Nafikiri ndio hiyo *revision* aliyotakiwa aifanye.

Waheshimiwa Wajumbe suala hili kuna maneno mengi kwa kweli, maana kimtiririko wa kimahakama inaeleweka tumo wanasheria humu na hasa kesi ikiwa ni ya madai, kama upande mmoja haukufika basi kesi isikilizwe kwa upande mmoja uliopo, na huyo alikiri kwamba kweli alikuwa Dar es Salaam alipokuja kwangu. Sitaki nitumie maneno yangu ili yawe ndio maamuzi ya chombo hiki, lakini kimsingi Waheshimiwa Wajumbe, mahakama imefuata mtiririko wake mpaka mwisho.

Mhe. Waziri hapa amechukua juhudi ya kwenda kufukua kumbukumbu, kwa kuwaomba mahakama wazitafute kwa madhumuni ya kumsaidia jambo la muda mrefu. Nadhani tuendelee na huu utaratibu, wazitafute hizo kumbukumbu ili yaonekane mauzaji hasa yalikuwa ni ya kiasi gani, kwa sababu kuna taarifa nyingi juu ya jambo hili. Kwa hivyo, suala hili mimi nadhani tuliache, kama Mhe. Mjumbe aliyetoa hoja hii alivyosema basi tuone katika hicho kipindi kilichopo nini kinafanyika.

Hoja nyengine ni kuhusu huu mradi wa *E-Government.* Maelezo yaliyotolewa na Kaimu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma, ni kwamba mradi huu usimamizi wake uko kwa Mhe. Waziri wa Fedha. Hoja hii imekuja chini ya Wizara ya Kazi na Utumishi wa Umma. Suala linalohusu Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inategemewa wakati wowote baada ya kumaliza shughuli ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kumaliza shughuli yake, nitegemee kwamba jambo hilo lipate maelezo kwenye hiyo kamati inayohusika.

Waheshimiwa Wajumbe, hapa siamui kwamba hoja iwepo ile ya kutengeneza kamati teule au laa, lakini acha tuje tupate maelezo kamili ya Waziri anayehusika na mradi huu wakati kamati yake na ripoti yake itakapotakiwa itolewe kwenye kipindi hicho, baada ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kumalizika. Vyenginevyo akiyatoa sasa hivi itakuwa tunafanya *duplication* ya kazi, kwa sababu na wakati wa wizara yake itabidi atoe taarifa hiyo vile vile.

Kwa hivyo, suala hili mimi nasema tuliakhirishe mpaka kwenye shughuli yake yeye, Waheshimiwa Wajumbe mkija kuona maelezo hayakuwaridhisha, hiyo hoja tutaamua kutengeneza hiyo kamati teule au vyenginevyo, lakini katika kipindi cha wizara ya fedha itakapokuja kutoa ripoti yake kwenye shughuli za Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Basi baada ya maelekezo hayo sasa Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubaliana na ripoti ya utekelezaji...

Mhe. Ussi Jecha Simai: (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Katika maelezo yangu pamoja na ile hotuba niliyokuwa naisoma, lakini ripoti yangu ya kamati, Mheshimiwa kutokana na wizi uliotokea pale Idara ya Nyaraka, tuliomba kwamba iundwe kamati teule juu ya suala hili. Kutokana na umuhimu wa nyaraka zile Mhe. Spika, lakini naona hapa tunataka kuendelea katika maeneo mengine sijui vipi hili, tunaomba muongozo wako Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Ni kweli kabisa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora nilimzuia asiondoke, kwa bahati mbaya sana na inasikitisha kidogo, mambo mawili yamegongana, shughuli ya hapa na shughuli ambayo ametumwa na serikali anaelekea Dar es Salaam hivi sasa. Suala hilo ilikuwa jana atoe maelezo, lakini taarifa ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu alipokuwa anachangia, kwa kweli inaonekana kuna mambo *very sensitive*. Kuna ile tunaita Mamlaka ya Rushwa inafanya kazi juu ya jambo hili, kitu ambacho nilimuomba Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora asiondoke ili atoe taarifa kwa ufupi bila ya kuingia ndani, kwa sababu ukiingia ndani, aah! Wanasheria mpo hapa, tena Mhe. Waziri ulijibu jana. Kuna hatari ya kuharibu baadhi ya mambo ambayo yamebaki yakiendelea kushughulikiwa na hii Mamlaka ya Rushwa.

Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri alinileta taarifa hapa juu ya mambo ambayo alitaka nimpe ushauri kama ayaseme au asiyaseme. Namshukuru Mhe. Ismail Jussa jana aliposema kwamba kuna mengine hata hayasemeki, alinionesha kwenye maandishi hayo ambayo yalikuwa yana ugumu wa kuyazungumza. Mimi nilimshauri kwamba *position* ya hili kulisema kwenye *public* namna hii, basi tunaweza tukaingilia ule uchunguzi unaofanywa na hii Mamlaka ya Rushwa, na kile ambacho kinahitajika baadae ichukuliwe hatua ya kisheria, kuna hatari ya kuharibika.

Sasa mimi nilimtaka huyu aje atoe maelezo juu ya hatua au kiwango gani cha mamlaka hiyo imefikia katika kulichunguza hili jambo. Lakini ni kweli kabisa kuna mambo mazito yaliopo pale, ambapo mimi nilikuwa nawasihi sana Waheshimiwa Wajumbe kwamba Mamlaka hii ya Rushwa imalize kazi yake kwanza, ili tupate ripoti rasmi baadae na juu ya hatua za kisheria ambazo zitakuwa zimechukuliwa baada ya uchunguzi wake.

Waheshimiwa Wajumbe, kuna mambo *sensitive* kamati yenyewe bila shaka wameona huko na Mhe. Ismail Jussa Ladhu alidiriki kusema kwamba kuna masuala mazito, na huo uzito aliokuwa ameusema lakini hakuueleza wazi. Mhe. Waziri mimi alinileta, lakini nikaona hapana, kwa upeo wangu isingekuwa vyema kuutoa kwa sasa.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe, nia yetu sisi ni moja ya kuona mambo yanakwenda vyema, shughuli za serikali zinatekelezwa vizuri kwa kiwango kikubwa cha ufanisi. Lakini mambo yanayohusu matatizo ya kiuhalifu, kwa kweli hatimaye inabidi tuwe na hadhari sana, kuyaacha *public* wakati hasa uchunguzi wenyewe bado unaendelea.

Suala hili mimi nadhani Mamlaka inayohusika tuipe muda ifanye kazi yake, tukiwa na imani kwamba ikifikia pahala watachukua hatua zinazofaa, bila shaka kwa mashirikiano makubwa na serikali na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Waheshimiwa Wajumbe, nawaomba sana maana Dk. Mwinyihaji alikuwa yuko tayari sana kutoa hiyo taarifa, nikaona hapana kwa kweli ni nzito. Mwenyekiti nadhani maelezo kuhusu hoja hiyo umeyasikia.

Mhe. Ussi Jecha Simai: (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, maelezo nimeyafahamu sana, lakini mimi nasema bado kwamba Taasisi ya Kuzuia Rushwa ilipowekwa katika kuchunguza masuala haya, haikunyima uhuru Baraza la Wawakilishi kufanya kazi zake za Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa ile kanuni ambayo inatuongoza Mhe. Spika, ya kifungu cha 117 kinaonesha dhahiri.

Kwa hivyo, mimi bado nasisitiza kwamba iko haja Baraza lako tukufu kuunda kamati kwa ajili ya uchunguzi na Mamlaka ya Rushwa kwa upande wake watafanya kazi zao wala hatuwaingilii, na sisi tutafanya kazi zetu. Tutatunza siri, kwa sababu tunachofahamu sisi ni kwamba kazi za kamati za Baraza ni siri, na sisi Waheshimiwa tunafahamu hilo, tutatunza siri hizo mpaka wakati huo utakapofika, sisi kwa upande wetu tutafanya kazi hiyo Mhe. Spika, na wao watafanya kazi zao wala hatutoingiliana. Mhe. Spika, naomba tufanye hivyo.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria hebu toa maoni yako juu ya hilo, maana ni vizuri tukaamua mambo tukiwa na uhakika ili tusiharibu upande mwengine, ni muhimu sana.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwanza nafikiri ni kifungu cha 120 ndio Kamati Teule. Sasa kamati teule inaweza kuundwa wakati wowote ule, mradi kamati ile inafanya shughuli zake tofauti na shughuli nyengine, ile Mamlaka ya Kuzuia Rushwa ni chombo cha serikali kinafanya shughuli zake kiserikali, lakini huku Baraza la Wawakilishi ni mkono mwengine. *(Makofi).*

Kwa hivyo, mimi Mhe. Spika, sioni kwamba zinagongana hizi shughuli, kwa sababu huku ni mkono mmoja na kule ni mkono mwengine kila mtu anafanya kazi kwa wakati wake. Sasa inategemea wewe mwenyewe matakwa yako, lakini inawezekana. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mimi kimsingi baada ya kuona taarifa aliyokuwa ananipa Dk. Mwinyihaji, kwa kweli nilikuwa nina hofu, na hatutakiwi tutoe maamuzi kwa hofu, lakini nilikuwa nina hofu na nikafikiri kwamba labda muda tungetoa kwa Tume ya Rushwa. Sina tatizo katika kutengeneza Kamati Teule kabisa. Narudia kwamba sina tatizo katika kutengeneza kamati teule na inavyoonekana Waheshimiwa Wajumbe mnataka iwe hivyo. *(Makofi).*

Waheshimiwa Wajumbe, lakini shida yangu Waheshimiwa Wajumbe ni ile *sensitivity* aliyoonesha Dr. Mwinyi juu ya jambo hili. Baada ya kuieleza hivyo Waheshimiwa Wajumbe hili ni letu sote, nia na madhumuni haya yote yatengenee, yaende vizuri, ndio nia kubwa. Hata hiyo Kamati Teule nia yake ni kuleta taarifa ili hatimae tufanye maamuzi ambayo yatasaidia kulitengeneza hili ndio nia. Mamlaka ya Rushwa uchunguzi wake nia yake wahalifu wakipatikana wachukuliwe hatua za kisheria kama inavyoonekana inafaa. Kwa hivyo *converging point* ni moja kulitengeneza, njia kuna hizi mbili kuiachia Mamlaka moja ikafanya kazi au shughuli zote zikaenda sambamba kwa pamoja. Bado Waheshimiwa serikali ninaiachia itoe maoni yake ili tuone tunakwenda wapi tufanye maamuzi.

Waheshimiwa mimi niwe *referee* hapa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Na mimi vile vile sitaki nieleweke kwamba nina tatizo la kuundwa Kamati Teule. Hata nilipotoa maelezo yangu jana nilisema hivyo, lakini tuangalie kama maelekezo yako ambayo umeendelea kutupa Mhe. Spika, kwamba hivi sasa kuna vyombo vinashughulikia jambo hili, na kikawaida taarifa ya rushwa inapobainika kwa mujibu wa ile sheria ya Mamlaka ya Rushwa, inatakiwa iletwe kwenye chombo hiki, wakishamaliza shughuli zao na kubaini ile taarifa kwa ujumla ya mambo ya rushwa yalivyojitokeza inatakiwa iletwe kwenye chombo hiki. Kwanza hilo moja lakini Kamati inaweza ikaenda ikafanya kazi hiyo na Mamlaka ya Rushwa ikaenda ikafanya kazi hiyo mimi naiangalia kwa upande mwengine wa shilingi ambao sitaki kuusema hapa. Kwa upande mwengine wa shilingi kwamba hivi vyombo vyote hivi vitakuwa vinafanya kazi hii hii moja, kwa nini tusiwape wale Mamlaka wakamaliza kazi yao halafu baadae kama hatukuridhika na zile *findings* zilizokuwa zimetolewa halafu sisi tukaunda Kamati Teule.

Mimi ushauri wangu ulikuwa ni huo, lakini sina tatizo hata kidogo kwa sababu tukio kweli limetokea na lazima tulishughulikie. Na kama nilivyosema mwanzo serikali msimamo wake hizo nyaraka ziliko tukishapata uhakika zitatumika njia za kusema kwamba tuletewe nyaraka zetu. Lakini katika tuhuma na kuchunguza mimi kama nilivyosema jana Taasisi za Serikali tayari limeanza kulifanyia kazi hili jambo, na kama alivyosema Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Utawala Bora, kwamba kuna mambo mengine kama atayasema waziwazi hapa yanaweza yakatuharibia ule uchunguzi ambao unafanywa, lakini sina tatizo na Baraza hili likiona kwamba liunde Kamati Teule liunde, lakini ushauri wangu nilikuwa naona kama inawezekana tungesubiri hizi mamlaka ambazo zinafanya kazi zikafanya kazi. Na kwa sababu zinawajibika kuleta taarifa kwetu, tukasubiri wakati huo kama kuna haja sasa ya kuunda Kamati Teule tukafanya hivi.

Mhe. Spika, nilikuwa na hayo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, na nataka nithibitishe kwamba jicho lako halina kificho limeniona hasa, kwa sababu nilinyanyuka kwanza kabla ya Mhe. Hamza, kwa hivyo ninafikiri atanistahamilia kaka yangu.

Mhe. Spika, nilikuwa nataka kuzungumzia kuhusu utaratibu si kwa kutumia kanuni kwa kutumia Katiba. Katiba yetu ya Zanzibar ibara 43(5) inasomeka na naomba ninukuu Mhe. Spika:-

> "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Mamlaka ya Rais ndio itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera za serikali kwa ujumla, na mawaziri chini ya uongozi wa Makamu wa Pili wa Rais watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar".

Sasa Mhe. Spika, nimeona nikinukuu kifungu hiki kwa sababu tunazungumzia suala muhimu sana hapa. Jana tumezungumzia tulipokuwa tukijadili kwamba tunazungumzia urithi wa kitaifa. Mhe. Spika, na nadhani tangu jana ukifuatilia mjadala wa Wajumbe na hata huu unaoendelea hivi sasa kuna masuala mawili. Kuna suala la uchunguzi wa kijinai ambao Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi tumeipa uwezo huo chini ya sheria ambayo tumepitisha hapa, lakini vile vile na vyombo vyengine kwa mfano Polisi havizuii vile vile kufanya uchunguzi wake kwa mujibu wa sheria za nchi.

Kuna mambo mengine yanayohusu utawala na uwajibikaji ambayo hayo mamlaka ya kuisimamia serikali yako kwenye chombo hiki. Katika michango

yetu Mhe. Spika, kulitokeza mambo ambayo yalikuwa yanaashiria udhaifu wa utawala na uwajibikaji pale katika chombo kile. Lakini vile vile tulitaka pafanyike kazi au tulitoa rai kwamba ifanyike kazi ya kupitia faharisi (*index)* na nyaraka mbali mbali zilioko pale ili kujiridhisha. Si suala hili tu ambalo tunazungumzwa sasa lakini kwa ujumla wake usalama wa nyaraka zetu ulivyo pale. Lakini na vile vile hifadhi ya mambo mbali mbali, na tukadirie alivyosema Mhe. Spika, humu ndani kwamba kwa sababu tunatambua suala lenyewe ni la fani maalumu linahitaji utaalamu basi hata tukiunda Kamati Teule kuna taratibu zinazoturuhusu kutumia wataalamu tutake waongezwe wataalamu ili ifanyike kazi hiyo. Kwa sababu baadae ni muhimu sana Mhe. Spika, kuwa wananchi kupitia chombo hiki kujua hali halisi ya hifadhi yao ya urithi wa kitaifa ilivyo katika jumba la nyaraka.

Kwa hivyo mimi nilikuwa nasema kwamba katika hili, kwa sababu serikali imeshatwambia tangu jana Waziri mwenye dhamana ya sekta kaimu wake hivi sasa kwamba haina pingamizi na suala hili la kuundwa kwa Kamati Teule, basi mimi nilikuwa naomba Mhe. Spika, hasa kwa sababu imeonekana Wajumbe walio wengi Barazani wameunga mkono suala hili, tena *across the benches,* basi nilikuwa naomba sana Mhe. Spika, kwamba turidhike kwamba na utapoandika tu labda hizi hadidu rejea tukikubaliana hapa kwamba zisiingilie uchunguzi wa kijinai ambao huo unafanywa na Mamlaka husika lakini Kamati ya Baraza la Wawakilishi ikafanye kazi yake kwa ujumla wake ili tujue mbivu na mbichi inayoendelea Kilimani katika jumba la Nyaraka.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nadhani nikiongeza zaidi aliyoyazungumza Mhe. Jussa nitakuwa ninatoa ile ladha yenyewe, nilikuwa mimi kitu ambacho nilichotaka kukisema ndio kile, kwamba serikali ile Tume ya Rushwa tumeiunda kwa mujibu wa sheria. Na sisi hata kama hatujaunda Kamati Teule wale wataendelea kufanya kazi mbali mbali, lakini na vile vile na jambo lolote ambalo na sisi tutahisi iko haja kwenda kulifanyia uchunguzi, kwa hivyo vile vile na sisi tutakuwa hatuingilii kazi zao. Kwa hivyo ina maana ile Tume itaendelea kufanya shughuli waendelee na sisi Waheshimiwa kwa mujibu wa taratibu zetu na Kanuni zetu turuhusu tuifanye hiyo kazi. Nashukuru sana.

Mhe. Spika: Serikali kuna maneno yoyote nataka tufanye maamuzi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Kwanza ninakushukuru kwa kunipa nafasi na pia niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe kwa namna walivyo makini kuhakikisha mambo ya nchi yanakwenda vizuri. Kwa msingi huu wamekuwa wakichukua kila hatua ili kusawazisha pale ambapo panajitokeza kasoro, lakini Mhe. Spika, ningependa niunge sana maneno yako uliyoyaeleza hapa kwa kuweka tahadhari na

maamuzi ambayo tutakayoyafanya. Na mimi nilikuwa navutika sana kabisa na ushauri wako kwamba, kwa kuwa kuna chombo hiki cha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa kitafanya kazi, na baada ya kukamilisha kazi hiyo tutaileta hapa mbele ya Baraza lako Tukufu kwa njia moja au nyengine chombo hiki kingetusaidia sana kufanya maamuzi vizuri zaidi baada ya kufanya kazi hiyo.

Kwa hivyo mimi nilikuwa naliomba tu Baraza lako Tukufu Mheshimiwa likafikiria zaidi kuhusu kutoa nafasi zaidi kabla ya kuundwa Kamati Teule ili hiyo kazi ifanyike na kwa njia moja au nyengine kutokana na ile hadhari ambayo Waziri mwenye dhamana ya sekta alikuwa ameiona, ni vizuri sana Mhe. Spika, Baraza lako likavuta subra likangojea maelezo zaidi kutoka chombo hiki cha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na vyombo vyengine vitakavyofanya uchunguzi wa jambo hili, ili tukifanya maamuzi tufanye maamuzi kwa kina, pengine wakati huo Baraza lako litakuwa limeridhika na hatua iliyofikiwa na kusiwe na haja tena ya kuunda Kamati Teule na matokeo yake yakawa kuchukua hatua ya yale yaliyotendeka.

Ikiwa Baraza halikuridhika na yale ambayo vyombo vyetu vitayafanya, basi pale ingekuwa ni muafaka na ni busara kuunda Kamati Teule. Mimi nilikuwa ninaliomba tu Baraza lako liendelee kuvuta subra uione kazi itakayofanyika na baadae itoe maamuzi. Ninaamini yapo mambo mengi lakini kama ni hivyo bora hayo mambo yaagizwe serikali izidi kuiambia mamlaka hii ya Rushwa iende ikayafanyie uchunguzi zaidi. Kwa sababu kwa vyovyote vile itakavyokuwa, Kamati yetu hii itabidi kutumia baadhi ya wataalamu hao hao ambao watakuwa na kazi hiyo wanayoifanya. Kwa hivyo mimi nilikuwa naomba tu Baraza livute subra, lingojee kazi hiyo na pale ambapo halikuridhika litaunda Kamati Teule.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwamba unatumia busara na hekima kubwa ili kuhakikisha kwamba tunafanya maamuzi yenye maslahi na wananchi wa Zanzibar. Mhe. sitaki kuingia katika akili za watu wengine kujaribu kufikiria nini kinachohofiwa hicho ambacho umesema hata wewe Mhe. Spika, umekiona. Lakini katika mchango wangu nilitaja kitu na naendelea kutaja hivyo na nakuhakikishia kwamba sitafanya jambo ambalo litatuingiza katika matatizo, nilisema kwamba sihofii kusababisha mgogoro wa kidiplomasia ndio maneno niliyoyatumia, basi ningetaja suala fulani.

Sasa Mhe. Spika, kwa vyovyote itakavyokuwa nchi yetu inatangulia kwanza kuliko nchi nyengine yoyote, kuliko jambo jengine lolote. Sisi tumeletwa na

wananchi wa Zanzibar kusimamia maslahi yao, lakini nije katika nukta yangu kutokana na maneno ambayo kayazungumza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, mimi binafsi sitaki kuwasemea wenzangu ningeliweza kuridhika na maelezo hayo lakini Baraza hili Mhe. Spika, lina *record* moja upande wa serikali hasa, kwamba mara nyengine linatuahidi mambo halafu tunashuhudia kwamba utekelezaji wake tunapigwa dana dana, kazungumza punde Mhe. Hamza, mfano hai ni suala la *E-Government* lakini hilo mbali Mhe. Spika, kwa hili mimi ninachokihofia kitu kimoja tu kwamba tunasema tuiachie Mamlaka hii ya kuzuia rushwa na uhujumu uchumi. Halafu ikiwa hatukuridhika tunaweza kuunda Kamati Teule.

Mhe. Spika, limeshawahi kutokezea jambo si moja wala si mawili hapa na mimi mwenyewe nilikuwa ninahusika nimelizungumza hapa tukazuiwa tukaambiwa liko mahkamani. Na tukatoa hoja kwamba kilichopo mahkamani ni nchi nyengine ya suala lile ambacho hakihusiani na kinachozungumzwa lakini ikatumika vizuri kwamba suala hili liko mahkamani tuliache. Sasa na hili Mhe. Spika, inawezekana kabisa baada ya hatua ya mamlaka kukamilisha kazi yake likapelekwa mahkamani na pengine likagusa ncha moja tu kati ya yale mengi ambayo tumeyazungumza, likishakuwepo kule ikawa baada ya hapo sasa Baraza hili haliwezi kuingilia tena kwa sababu kanuni ya 59(4) inatukataza kujadili suala ambalo liko mahkamani.

Kwa hivyo ndio maana mimi nilikuwa nasema Mhe. Spika, kwamba ni vizuri mamlaka ikaendelea na uchunguzi wake wa kijinai na Baraza likapewa haki yake iliyopewa na Katiba ya Zanzibar likafanya uchunguzi wa yale mambo mengine ambayo ni nje ya jinai, kwa sababu Baraza hili hata likiandika ripoti Mhe. Spika, tunajua sote kwa mujibu wa sheria ya Kinga, Haki na Fursa ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ripoti ya Kamati Teule haiwezi kutumika kama ni ushahidi mahkamani tunajua hilo.

Kwa hivyo uchunguzi wa hapa hautokuwa wa kijinai, lakini utatupa nafasi sisi Wawakilishi wa wananchi kwanza kujua nini kilichopo pale, kuna mapungufu zaidi juu ya yale ambayo tunayoyazungumzia hapa na baadae kuielekeza serikali katika taratibu za kiutawala na za kiuwajibikaji ili kupata ufanisi zaidi. Naomba sana Mhe. Spika, tuache Mamlaka ifanye shughuli za jinai na Baraza lipewe haki yake ya kikatiba. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ninafikiri sasa inatosha tuamue kwa kuzingatia maelezo yaliyotoka humu ndani, tuamue na hoja aliitoa hasa Mwenyekiti pale kwamba kuhusiana na suala la matatizo ya nyaraka pale hili lingeundiwa Kamati Teule.

Basi Waheshimiwa Wajumbe baada ya maelezo ya pande zote mbili na mashauriano ya kina tuliyopeana hapa niwahoji sasa.

Wale wanaopendelea kuunda Kamati Teule bila ya kusubiri kwanza Mamlaka ya Rushwa kufanya shughuli yake na ikamaliza kwamba Kamati Teule iundwe sasa na ifanye shughuli zake sambamba na Mamlaka ya Rushwa kufanya shughuli zake wanyanyue mikono. Wanaokataa,

Kwa hivyo wanaopendelea kwamba Kamati Teule iundwe sasa wameshinda.

Mwachie Spika sasa aje atangaze hiyo Kamati Teule na lini kuanza kazi yake hiyo tutaitangaza baadae.

Basi Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo. Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na ripoti ya utekelezaji kwa Wizara mbali mbali pamoja na ripoti ya Kamati iliyowasilishwa wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Kamati Teule itaundwa, Spika atatangaza baadae Kamati Teule hiyo na lini ianze kazi na kwa muda gani.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

TAARIFA ZA SERIKALI

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya mwaka 2012/2013

Mhe. Spika: Nikuombeni Waheshimiwa Wajumbe tutumie muda mfupi kwa sababu shughuli zetu kidogo zimebanwa na kuna jambo kubwa sana linalohusu masuala ya kazi kubwa na wajibu wetu mkubwa wa mambo yanayohusu kujitayarisha na Bunge Maalum la Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe awali ya yote napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia uzima wa afya na kutuwezesha kukutana hapa leo hii kujadili utekelezaji wa maagizo tuliyopewa na Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, kabla ya kutoa ufanunuzi wa utekelezaji wa maagizo hayo naomba nitoe kwa muhtasari maelezo ya muundo na majukumu ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, wizara imeanzishwa kwa lengo la kuinua na kuimarisha hali na ustawi wa wanawake, vijana, watoto na watu waliokuwa katika makundi maalumu, ikiwa ni pamoja na wazee wasiojiweza, mayatima na watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi.

Aidha, wizara ina jukumu la kusimamia, kuongeza na kutanua programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi. Wizara inatekeleza malengo yake hayo kupitia Idara zake nane na Ofisi Kuu Pemba. Idara hizo ni Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Uendeshaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Idara ya Ushirika, Idara ya Mikopo, Idara ya Ustawi wa Jamii, Idara ya Maendeleo ya Vijana, Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto na Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, katika kipindi cha utekelezaji wa mipango iliyojipangia kwa mwaka 2012/2013 Wizara ilipewa maagizo 12 ya kuyafanyia kazi na kamati ya maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ili kuimarisha ufanisi na ufikiwaji wa malengo na majukumu iliyopewa.

Sasa naomba niwasilishe taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kama hivi ifuatavyo:

Agizo namba 1. Kamati iliitaka Wizara ihakikishe kuwa inakipatia kituo cha kulelea watoto Mazizini jenereta. Mhe. Spika, katika kulitekeleza agizo hili wizara ilipanga kununua jenereta kubwa ili kuondoa tatizo la umeme katika nyumba ya kulelea watoto huko Mazizini kutokana na kuzimwa kwa umeme mara kwa mara. Hata hivyo kutokana na ufinyu wa fedha jenereta hilo halikuweza kununuliwa. Aidha kwa hivi sasa tatizo la kuzimwa umeme mara kwa mara limepungua. Wizara ina mpango wa kununua genereta dogo ili litumike wakati wa dharura katika bajeti ijayo.

Agizo namba 2. Kamati iliitaka Wizara kuandaa taarifa maalumu za *Data Base* za maendeleo ya kila mtoto anaelelewa katika kituo cha Mazizini ili kuelewa kumbukumbu zake kwa ajili ya maendeleo yake ya baadae. Mhe. Spika, ili kulitekeleza agizo hili Wizara kwa kutumia wataalamu wake wa ndani imetengeneza mfumo rahisi kwa kukusanyia taarifa yaani *data base*, ili kuhifadhia kumbukumbu za watoto wanaolelewa katika kituo cha Mazizini kwa wakati huu kazi ya kuingiza takwimu za watoto katika mfumo huu inafanyika vizuri.

Agizo namba 3. Kamati iliagiza Wizara kwamba malipo ya fidia za wafanyakazi yarejee Hazina na kwamba Wizara ya Fedha ilipe deni hilo. Wizara ya Uwezeshaji Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto imekuwa na deni kubwa la muda mrefu la zaidi ya shilingi milioni 92,844,586 kwa ajili ya fidia ya wafanyakazi waliopata ajali kazini ambapo inashindwa kulilipa. Mhe. Spika, wizara inaendelea na juhudi za kulitatua tatizo la deni kubwa la fidia kwa wafanyakazi waliopata ajali kazini.

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Vijana Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi iliandaa kikao maalumu kulitafutia ufumbuzi tatizo hilo. Kikao hicho kilifanyika tarehe 29/11/2013 katika Ofisi ya Baraza la Wawakilishi Chukwani, na kilijumuisha Makatibu Wakuu kutoka Wizara ya Uwezeshaji na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Fedha. Katika kikao hicho ilikubalika kwamba Makatibu Wakuu hao wachukue hatua ya kulitatua tatizo hili ambapo mambo yafuatayo yamefanyika.

Wizara ya Uwezeshaji, Vijana, Wanawake na Watoto imeandaa orodha ya wafanyakazi wote wanaodai fidia, pamoja na kiwango cha fidia wanachodai na kuiwasilisha kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha kwa hatua zaidi. Wizara ya Fedha imetoa ahadi ya kulilipa deni lote la fidia shilingi milioni 92,844586 kabla ya kufikia mwishoni mwa mwezi wa Machi 2014 baada ya kukamilisha baadhi ya taratibu ikiwemo uhakiki wa madeni hayo. Wizara imekubaliana na Wizara ya Fedha kuwa wakati huu utumike utaratibu wa kuweka fedha maalumu kwa ajili ya malipo ya fidia ili kuondoa tatizo liliopo. Fedha hizo zitatumika kwa matumizi hayo tu. Pamoja na hayo Wizara inaona kuna haja kwa Wizara husika yaani Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma kujadili kuhusu utaratibu mzuri zaidi wa kushughulikia suala la fidia kwa kuzingatia sheria iliyopo yaani sheria ya fidia ya mwaka 2005.

Mhe. Spika, wizara inaendelea kufanya mawasiliano ya kuratibu na Wizara ya Fedha ili kuhakikisha kuwa deni liliopo sasa linalipwa kama ilivyoahidiwa. Aidha Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha itasimamia utekelezaji wa maamuzi mengine yaliyofikiwa ili kuwa na utaratibu ulio bora zaidi wa kusimamia malipo ya fidia kwa wafanyakazi wanaoumia au kupata madhara wakiwa kazini.

Agizo namba 4. Kamati imeagiza wizara kuchukua hatua za dharura za kuiezeka jengo la Idara ya Maendeleo ya Ushirika ili kuwapatia watendaji wake mazingira bora ya Afya na Usalama kazini.

Mhe. Spika, Wizara imechukua hatua na kufanikiwa kuipatia Idara ya Ushirika jengo jengine lenye mazingira bora zaidi ya kufanyia kazi. Jengo hilo lipo eneo la Migombani karibu na Mnara wa Mbao. Hata hivyo kwa kuwa jengo hilo halijatumika kwa muda mrefu linahitaji matengenezo makubwa yanayohitaji fedha nyingi ili iweze kutumika. Wizara tayari imeandaa taratibu za kufanikisha matengenezo hayo.

Agizo namba 5. Iko haja ya Wizara kuendelea kuelimisha jamii juu ya dhana nzima ya ushirika, kwani hadi sasa ni asilimia ndogo tu ya wanajamii wanayoifahamu kufanya hivyo kutawasaidia wale wenye nia ya kujikomboa kutokana na janga la umaskini uliokithiri na ambao hawazijui fursa za kiuchumi zilizopo kwenye mazingira yao na jinsi ya kuzitumia kwa manufaa, kuibua miradi mbali mbali itakayowainua kimaisha.

Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika kwamba jamii iliyo kubwa bado haijaelewa dhana nzima ya ushirika ikiwemo misingi, kanuni pamoja na falsafa ya vyama vya ushirika. Wizara inaendelea kuchukua juhudi mbali mbali za kuelimisha jamii kuhusu masuala ya ushirika. Juhudi hizo ni pamoja na utoaji wa mafunzo kwa njia za semina, mikutano na programu za *radio* na televisheni. Wizara pia inaendelea kuwaelimisha wananchi kupitia vipeperushi vilivyoandaliwa maalumu ambavyo vinaelezea haki na wajibu wa wanachama. Namna ya kutambua fursa za kiuchumi zilizopo kwenye maeneo yao na jinsi ya kuzitumia ipasavyo katika kuinua miradi mbali mbali kupitia vyama vyao vya ushirika.

Agizo namba 6. Wizara imetakiwa kuweka mpango endelevu wa kuwapatia elimu watendaji wa Idara ya Ushirika inayohitajika kwani Kamati imegundua kuwa hali ya ukaguzi duni inachangiwa kwa kiasi kikubwa na upungufu wa wakaguzi waliobobea kwenye fani hiyo.

Mhe. Spika, Wizara inapenda kukiri kwamba ni kweli kuwa hali ya ukaguzi duni inachangiwa kwa kiasi kikubwa na upungufu wa wakaguzi uliobobea kwenye fani hiyo. Katika kulifanyia kazi tatizo hili. Wizara tayari imeandaa mpango wa kuongeza idadi ya wakaguzi wenye sifa ili kuimarisha utoaji wa huduma za ukaguzi kwenye vyama vya ushirika. Mpango huo ni pamoja na kuwatumia vijana waliosoma taaluma ya uhasibu walioko kwenye sekta bianfasi, ili watumike kutoa huduma ya ukaguzi kwenye vyama vya ushirika.

Aidha, wizara imeandaa mpango wa kuwaandaa vijana hao ili waweze kutoa huduma hiyo kitaalamu na kwa ufanisi. Pamoja na juhudi hizo, wizara pia imeandaa mpango wa mafunzo kwa maofisa ushirika. Kupitia mpango huo, maofisa wanapatiwa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, ili waweze kutekeleza kazi zao kwa ufanisi.

Agizo nambari 7. Wizara imetakiwa kusimamia utengenezaji wa mkataba utakaotumika wakati wana ushirika wanapohitaji kuagiza vifaranga, ili kupunguza udanganyifu unaofanywa na wasambazaji wa vifaranga kwa wanavikundi kwa kuwapatia vifaranga vyenye maradhi.

Mhe. Spika, kuhusiana na hoja ya udanganyifu unaofanywa na wasambazaji vifaranga kwa wanavikundi ambapo huwapatia vifaranga vyenye maradhi, wizara inalifanyia kazi suala hili kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Zanzibar (KUZA) iliyoko Kisiwandui. Hii ni pamoja na kuviimarisha vyama vikuu vya ushirika, ili hapo mbele viweze kusimamia masuala haya pamoja na masuala ya masoko.

Pia wizara itaendelea kushirikiana na wizara inayohusika na masuala ya mifugo ili kuhakikisha kuwa udanganyifu unaofanywa na wasambazaji vifaranga kwa wanaushirika unadhibitiwa kisawa sawa.

Agizo nambari 8. Wizara iendelee kutoa elimu kwa jamii juu ya dhana ya uwezeshaji na jinsi gani wananchi wanavyowezeshwa, kwa njia mbali mbali kwa kutumia vyombo vya habari vya taifa na redio jamii zilizopo nchini.

Mhe. Spika, katika kulitekeleza agizo hili, wizara imekuwa ikitumia taaluma juu ya masuala ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kupitia programu za TV na redio zinazoandaliwa na Kitengo cha Habari na Mawasiliano cha wizara yenyewe. Elimu pia inatolewa kupitia makala zinazoandaliwa na kutolewa kupitia kwenye magazeti hususan Gazeti la Zanzibar Leo. Aidha, elimu imekuwa ikitolewa kila pale ambapo wizara imekuwa ikikutana na wananchi wenyewe kwa masuala mbali mbali. Pamoja na hayo, wizara imekuwa na tabia ya kualika vyombo vya habari vya *ZBC* Redio wakati wa shughuli zao za mafunzo na utoaji mikopo, ili ziweze kuwatangazia wananchi na kuelewa shughuli zinazofanywa na wizara katika utekelezaji wa shughuli za kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Agizo nambari 9. Wizara ifuatilie usajili wa vikundi vya wanaushirika. Vikundi vingi Pemba bado havina muamko na havielewi taratibu za usajili. Mhe. Spika, wizara inaendelea na kazi ya kuvihamasisha na kuvishajihisha vikundi kupitia maofisa wake wa wanawake na watoto wa wilaya na mkoa. Maofisa vijana wa mikoa na maofisa ushirika ili waweze kujisajili na waweze kutumia fursa zilizopo.

Pia wizara imeendelea kusajili vikundi vya ushirika Unguja na Pemba ambapo mwaka 2012/2013 jumla ya vikundi 136 vimesajiliwa. Aidha, katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2013 jumla ya vikundi 178 vimesajiliwa. Vile

vile wizara inaendelea na uhamasishaji ili kuhakikisha vikundi vyote vya uzalishaji mali Pemba vinasajiliwa kama vyama vya ushirika.

Agizo nambari 10. Kamati iliagiza kufanywa tathmini juu ya faida ipatikanayo kutokana na mradi wa mboga mboga na mauwa ya Rosela unaoendeshwa na kikundi cha vijana cha *ZASOSE* Tunguu.

Mhe. Spika, mradi wa shamba la mauwa na mboga mboga la Tunguu lilifanyiwa tathmini na wataalamu wa kilimo kutoka Wizara ya Kilimo na Maliasili, ambapo walitoa ushauri mbali mbali kwa kuendeleza shamba hilo, ili kuhakikisha kuwa linaleta tija ya haraka kwa vijana wanaolifanyia kazi.

Wizara imesaidia uanzishaji wa kilimo cha *green house* kupitia *green house* ambazo zimeanzishwa na tayari mavuno yameanza kupatikana. Mazao yanayozalishwa katika shamba hilo ni pamoja na mboga mboga, tungule, pilipili boga, vitunguu maji, mabilingani na hasa mauwa ya Rosela, kwani shamba lenyewe hasa linajuilikana kama shamba la Rosela.

Mhe. Spika, kufuatia ushauri uliotolewa na wataalamu, imependekezwa kufanya mashamba ya vijana ya Tunguu Unguja na Mbuzini Pemba kuwa ni mashamba darasa ili vijana waliopo waweze kutoa mafunzo kwa vijana wenzao, ili nao waweze kujiajiri kupitia shughuli za kilimo.
Mhe. Spika, mbele yako nataka niseme kwa kweli vijana wa Rosela Tunguu wanafanya kazi nzuri sana, na ni wa kupewa hongera kubwa kwa kazi nzuri.

Agizo nambari 11. Kamati imeagiza wizara kuwa na wakili maalum Pemba atakayesimamia kesi za ubakaji. Mhe. Spika, katika kutekeleza agizo hili, wizara tayari imeshaajiri ofisa wa sheria na ameshaanza kazi huko Pemba. Pamoja na kazi nyengine ofisa huyo anashughulikia kesi za ubakaji.

Agizo nambari 12. Kamati imeitaka wizara kuhakikisha kuwa imeweka usafiri wa uhakika katika kituo cha mkono kwa mkono ili kusaidia kituo hicho kuhudumia kesi za udhalilishaji. Mhe. Spika, wizara imelipokea agizo hili. Hata hivyo, naomba ieleweke kuwa kituo cha mkono kwa mkono kipo chini ya Wizara ya Afya ambayo ndio yenye wajibu wa kuhakikisha upatikanaji wa mahitaji maalum kwa uendeshaji wa kituo hicho.

Hivyo, Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto itashirikiana vizuri na Wizara ya Afya katika kusaidia upatikanaji wa usafiri kwa kituo cha mkono kwa mkono.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri tunakushukuru kwa uwasilishaji wa taarifa hiyo ya utekelezaji wa maagizo mbali mbali.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa idhini na kwa ruhusa yako na mimi naomba kuwasilisha taarifa fupi ya Wizara ya Afya juu ya maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, naomba nifanye sahihisho tu katika masuala ya ku-*print*. Ukurasa wa pili wa ripoti ile utakuta kuna namba hizo zinazoonesha mahesabu yaliyojumlisha mpaka shilingi bilioni nne. Taarifa hiyo ilikuwa ije mwakani kwa ajili ya kujibu masuala ya mwakani tuliyoulizwa mwaka huu, lakini katika kuandika ikaingia. Sasa hiyo sehemu ya pili ukurasa wa pili hapo juu, naomba iwe haionekani kama ni sehemu ya taarifa.

Mhe. Spika, baada ya sahihisho hilo dogo nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa tukiwa na afya njema. Mheshimiwa naomba pia kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na kwa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mashirikiano yao ya dhati kwa Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, kwa muda wote wa kamati, tulipata mashirikiano makubwa kutoka kwa mwenyekiti na wajumbe wa kamati iliyopita, ambayo hivi sasa imefanyiwa marekebisho na kupata mwenyekiti mpya Mhe. Mgeni Hassan Juma. Nampongeza kwa kuja kushirikiana nasi Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya sasa imeendelea kufanya kazi na wizara yetu kwa maelewano na mashirikiano ya hali ya juu sana. Pia imeweza kutushauri vizuri na kutusaidia sana katika kukabili matatizo yetu. Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo, naomba sasa kwa ufupi nitoe maelezo ya maagizo tuliyopewa ya mwaka 2012/2013 na kamati hii.

Agizo nambari moja. Kamati iliagiza wizara kuhakikisha kuwa inajenga hoja ya msingi kwa serikali kuu ili kuwepo na uhakika wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa. Kamati imebaini kuwa hakuna uhakika wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa. Badala yake serikali hukaa muda mrefu na hutoa fedha chache zisizokidhi haja na kuwategemea wahisani (*DANIDA*), ambao pia wamekuwa na masharti yasio na mwelekeo mzuri wa ufanisi, kwa upatikanaji wa dawa muhimu kwa afya ya jamii.

Ufafanuzi. Wizara katika kuhakikisha upatikanaji wa dawa imetengeneza mfumo mpya wa ununuzi wa dawa ambapo dawa zitakuwa zinanunuliwa kwa

kupitia mfumo wa *frame work contract* badala ya kutegemea *MSD* pekee, yaani lile Shirika la *DANIDA* lilioko Dar es Salaam.

Aidha, katika kuhakikisha suala hilo linapatiwa ufumbuzi wizara imefungua *account* ya dawa ambapo fedha kutoka serikalini na fedha za *DANIDA* zinaingizwa katika *account* hiyo. Katika kulihakikisha hilo upande wa fedha wa wafadhili ambao ni *DANIDA*, wamesisitiza kuwa hawataingiza fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa hizo mpaka wahakikishe kuwa serikali inachangia fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa hizo, ili kuthibitisha kwamba kuna hoja ya msingi kufika serikalini sasa.

Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ofisi ya Mfamasia Mkuu imepokea jumla ya shilingi 584,943,500 kutoka Mfuko wa Serikali, kati ya shilingi 1,547,000,000 tulizotengewa katika bajeti ya mwaka ule, ambayo ni sawasawa na asilimia 37.81.

Sambamba na hali hii, wizara pia imepata fursa kutoka kwa washirika wengine wa maendeleo ambao wako pamoja na serikali kutatua tatizo la upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Ufafanuzi wa fedha hizo kutoka kwa wafadhili hao ni kama ifuatavyo:-

- *Project Hope* imetoa shilingi 1,674,280,032
- Shirika linaloitwa **Prepha** limetoa shilingi 793,925,988
- DANIDA imeingiza shilingi 256,977,500

Jumla misaada tuliyopata kwa mwaka ule kutoka kwa wahisani ni shilingi 2,725,883,520.

Mhe. Spika, agizo nambari mbili. Kamati iliiagiza wizara ihakikishe inavipatia ofisi vitengo vya Afya Mazingira, kitengo cha UKIMWI, Ofisi ya Afya Elimu, Elimu na Kitengo cha Ufuatiliaji wa Magonjwa. Kamati hairidhiki na hali mbaya ya jengo la chanjo la Machomane ambalo liko Pemba, ambalo linatumika kwa ajili ya ofisi hizo. Jengo linavuja na kuwa na idadi kubwa ya wafanyakazi.

Ufafanuzi Mhe. Spika. Katika kulitafutia ufumbuzi tatizo hilo Wizara ya Afya imehakikisha jengo linajengwa. Hivyo basi, tangu miezi sita iliyopita tayari jengo hili la chanjo Machomane limeshakamilika na linaendelea kutumika. Aidha, kiasi cha fedha shilingi 11 milioni zimetumika katika ujenzi huo hadi kukamilika.

Agizo nambari tatu. Kamati imeagiza Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kulifuatilia suala la wizi wa magrili ya madirisha na milango

katika majengo yanayofanyiwa matengenezo kwa ajili ya Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali huko Maruhubi, ili hatimaye kuwabaini wale wanaohusika na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Ufafanuzi. Mhe. Spika, baada ya Mkemia Mkuu wa Serikali kulifuatilia kwa kina suala hili na kulithibitisha kuwa kweli huu wizi umefanyika, Wizara ya Afya ikishirikiana na Wizara ya Fedha imepeleka kesi hii polisi na kwa sasa wizara inasubiri taarifa ya upelelezi wa wizi huo.

Mhe. Spika, ni vizuri hapa niseme, Waziri wa Katiba na Sheria na Wajumbe walikuwa wamejadili hali ya mwenendo wa kesi za aina hii zinavyokwenda. Kwa hivyo, sisi baada ya kuikabidhi kesi hiyo tunabaki kungojea Mahakama inasema nini.

Agizo nambari nne Mhe. Spika. Kamati imeagiza wizara kuhakikisha kuwa inapata mashine ya kuchomea taka katika Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja. Kamati imebaini kutokuwepo kifaa hiki hospitali na kupelekea taka zote kuchomwa katika eneo la ufukwe wa bahari. Hali hii inapelekea uchafuzi wa mazingira na kuhatarisha afya za jamii.

Ufafanuzi Mhe. Spika. Katika kulitekeleza suala hili wizara tayari imeshafanya mchakato wa ununuzi wa mashine ya kuchomea taka na tayari ununuzi umeshafanyika. Kinachosubiriwa ni kikao cha mazungumzo ya makubaliano baina ya wizara na msambazaji ili kuleta mashine hiyo.

Agizo nambari tano. Kamati imeiagiza wizara kuhakikisha nyumba zote zilizopangwa kuvunjwa kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali mpya ya Abdalla Mzee huko Pemba zinavunjwa na wahusika kulipwa fidia kwa mujibu wa maelekezo ya tathmini ya Idara ya Mazingira. Maamuzi hayo yatasaidia katika mpango wa muda mrefu kwa matumizi ya eneo la ardhi la hospitali hiyo. Pamoja na kuepuka athari za kiafya na mazingira zinazoweza kutokea kwa jamii kutokana na shughuli za hospitali.

Ufafanuzi. Wizara imetenga jumla ya shilingi 900,000,000 tayari zimeshatolewa kutoka serikalini kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wale wote ambao wamevunjiwa nyumba zao. Jumla ya wananchi 15 pamoja na msikiti, kanisa na maskani ya CCM ni walengwa wa malipo hayo. Tayari fidia kwa ajili ya msikiti, maskani ya CCM pamoja na wananchi 13 wameshalipwa fidia hiyo na wananchi wawili bado hawajachukua fedha zao.

Agizo nambari sita. Kamati imeitaka wizara kuhakikisha kuwa sehemu ya *DNA machine* iliyopatikana inahifadhiwa vizuri pamoja na sehemu ya vifaa

vilivyobaki vinakamilishwa katika bajeti ya mwaka 2013/2014, ili iweze kutumika.

Ufafanuzi Mhe. Spika. Kama tulivyoeleza katika ripoti za awali kuwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014, sehemu iliyobakia ya vifaa vya *DNA* havitonunuliwa kutokana na uhaba wa fedha za ruzuku kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali. Bado vifaa hivi gharama zake ni kubwa, suala ambalo linaleta kikwazo kwa wizara. Katika kulipatia ufumbuzi tatizo hili, wizara kwa sasa imo katika matayarisho ya kuingiza bajeti ya ununuzi wa vifaa hivyo kwa mwaka wa fedha ujao, kwa kununua vifaa ili kuhakikisha azma hiyo.

Mhe. Spika, naomba kuongeza. Hata hivyo, tatizo la suala hili ni kubwa kuliko linavyoonekana. Kuna hoja tatu au nne; eneo la kuliweka linalotakiwa ni kubwa, fedha za kununulia ni nyingi na wataalamu itabidi wafundishwe na wasomeshwe kabla mashine hazijafungwa. Bahati nzuri Shirika la *COSTECH* la Utafiti la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumekutana nalo na limetukubalia kwamba tupeleke maandiko ili waone watatusaidia vipi. Lakini hata hivyo, eneo la pale Maruhubi inabidi tujenge nyumba ya juu, kwa sababu kieneo kilichopo cha Mfamasia Mkuu hivi sasa kwa kutia mashine hiyo hakitotosha.

Mhe. Spika, agizo la saba. Kamati imeagiza wizara kuhakikisha kuwa Hospitali ya Wete na Mkoani wanapatiwa gari la uhakika la kubebea wagonjwa. Kamati imebaini kuwa gari zinazoendelea kutumika hivi sasa ni chakavu na hazifai, ambazo zimetolewa tangu miaka ya 1990.

Ufafanuzi. Kama tulivyoeleza katika ripoti iliyopita kuwa Hospitali ya Wete tayari imeshapatiwa gari jipya na linaendelea vizuri na kazi zake za kawaida. Na kwa Hospitali ya Mkoani gari lililokuwepo limefanyiwa matengenezo makubwa na linaendelea kufanya kazi. Gari nyengine nne tunazitarajia kuwasili hivi karibuni kwa ufadhili wa Shirika la Watu Duniani (*UNFPA*). Gari hizo ni kwa ajili ya Hospitali ya Kivunge, Mwembeladu, Micheweni na Mkoani.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto (Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwanza naomba kukushukuru wewe kwa kunipa ruhusa na heshima ya kuwasilisha ripoti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuhusu utekelezaji wa maagizo mbali

mbali yaliyotolewa na Kamati ya kudumu ya Baraza lako tukufu, katika mwaka wa fedha 2013/2014.

Pili napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza lako tukufu na wajumbe wote wa kamati hiyo, kwa ushirikiano, michango na maoni mbali mbali wanayotoa kwa wizara.

Tatu, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa ushauri na maagizo mbali mbali wanayoyatoa kwa wizara. Michango ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu imesaidia sana katika kufanikisha kazi za wizara.

Mhe. Spika, maagizo ya Kamati ya kudumu. Katika mwaka 2012/2013 wizara imepokea maagizo tisa kutoka katika Kamati za Kudumu za Baraza. Wizara inatoa shukurani za dhati kwa kamati hizi kwa maagizo iliyoyatoa. Maagizo hayo ni muhimu na utatuzi wake utasaidia sana katika kupeleka mbele maendeleo ya sekta ya elimu. Wizara imeyafuatilia maagizo hayo na nina furaha leo hii kutoa taarifa ya utekelezaji wake kama hivi ifuatavyo:-

Agizo nambari moja. Kamati inasisitiza wizara kufuatilia malipo ya walimu wa *TAP* kwa namna yoyote ili, ili walimu hao wapate nyongeza zao.

Mhe. Spika, wizara imewasilisha Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma mapendekezo ya nyongeza kwa walimu hao wa mafunzo ya *TAP*. Wizara inaendelea kufuatilia juu ya suala hili.

Agizo nambari mbili. Kamati inaamini kuwa, eneo la Skuli ya Mpendae lina mgogoro na wananchi. Hivyo wizara kufuatilia suala hili kufahamu ukweli wake na kupatikana kwa ufumbuzi wa tatizo husika.

Mhe. Spika, wizara imefuatilia suala la mgogoro na wananchi, lakini haikubaini kuwepo kwa mgogoro. Eneo lililojengwa skuli ni la wizara ambalo lilitolewa na wizara inayohusika na masuala ya ardhi na hatimiliki ya eneo ipo.

Agizo nambari tatu. Wizara ichukue hatua ya makusudi ili kufuatilia ujenzi wa holi na nyumba za kudumu za Askari Polisi katika eneo la Skuli ya Shamiani, Madungu kwa suluhisho la kudumu.

Mhe. Spika, wizara imelifuatilia suala hili Idara ya Ardhi na kubaini kuwa waliojenga nyumba ya kudumu wamepewa eneo hilo na wana hatimiliki

zilizotolewa na Idara ya Ardhi. Nyumba mbili ni za taasisi za serikali na moja tu ni ya mtu binafsi.

Maelezo zaidi. Wizara inaangalia uwezekano wa kutaka kuinunua nyumba ya mtu binafsi pindipo mmiliki wake atakubali kuiuza kwa bei muwafaka.

Agizo nambari nne. Wizara ihakikishe kuwapatia walimu wa sayansi Skuli ya Kiwani, Mauwani na kusaidia kuondokana na tatizo la maji. Mhe. Spika, skuli imepatiwa walimu watatu wa masomo ya sayansi. Pia skuli inapata maji isipokuwa maji yanapatikana kwa mgao, kama zilivyo sehemu nyengine za Kiwani.

Agizo nambari tano. Skuli ya Kitogani ifanyiwe matengenezo. Hali ya skuli hiyo hairidhishi. Kamati haikuridhika na uchakavu wa majengo ya skuli hiyo katika ziara yake na ililazimika kuyafunga madarasa manne.

Mhe. Spika, jengo moja lenye madarasa sita tayari limefanyiwa matengenezo makubwa. Wizara itaendelea kufanyia matengenezo majengo mengine kadiri ya hali ya fedha itakavyoruhusu.

Agizo nambari sita. Kamati imeiagiza wizara kusimamia suala la ajira kwa wahitimu wa Kituo cha Ualimu wa Maandalizi Saateni, ili nao waweze kupata ajira katika skuli za serikali na hata binafsi.

Mhe. Spika, wizara imeyapokea maagizo hayo. Hata hivyo, kutokana na wingi wa walimu waliohitimu ngazi mbali mbali za elimu, serikali imetoa kipaumbele kwa ajira ya walimu waliohitimu stashahada na shahada za sayansi ambapo mahitaji ni makubwa sana. Pia mafunzo waliyopata wahitimu wa kituo hicho ni ya awali tu, na walikusudiwa zaidi kusaidia ufundishaji katika skuli za maandalizi za jamii. Baadhi ya wahitimu hawa wamejiajiri wenyewe kwa kufungua vituo vyao na baadhi wameajiriwa katika skuli za maandalizi za binafsi na za jamii.

Agizo nambari saba. Wizara ihakikishe inasimamia majengo yaliyochakaa katika Skuli ya Haile-Selassie. Aidha, kwa kushirikiana na walimu husika wa skuli, wizara isimamie kufikiria kuanzisha miundombinu itakayosaidia kutumika vizuri eneo lililo wazi. Badala ya kutumika kwa jaa la taka na gereji lililo ndani ya eneo la skuli.

Mhe. Spika, wizara inakusudia kuyafanyia matengenezo majengo ya Skuli ya Sekondari ya Haile-Selassie pamoja na miundombinu yake hali ya fedha itakaporuhusu.

Agizo nambari nane. Kamati imeiagiza wizara kuhakikisha kwamba Skuli ya Sekondari ya Haile-Selassie inafanya uchaguzi ndani ya kipindi cha mwezi mmoja ili kuwa na kamati mpya ya maendeleo ya skuli. Kamati imebaini kuwepo kwa kamati ya maendeleo ya skuli kwa zaidi ya miaka 20 bila ya kufanyika kwa uchaguzi.

Mhe. Spika, skuli imefanya uchaguzi na kamati mpya ya skuli imepatikana yenye wajumbe 24.

Agizo nambari tisa. Kamati imeiagiza wizara kuhakikisha kwamba, Manispaa inavunja maeneo ya kudumu ya kutupia taka katika Skuli ya Sekondari ya Jang'ombe ili kuokoa athari za kiafya. Kamati imebaini kuwepo kwa matumizi mabaya ya eneo la skuli ikiwemo maegesho ya gari. Kuwa na mpango endelevu wa kufanya mapitio ya sera ya elimu iliyopo kwa lengo la kuoanisha ufanisi wa sera hiyo na viwango vya ufahamu wa vijana.

Mhe. Spika, wizara imelitembelea jaa la taka liliopo Skuli ya Jang'ombe na imeitaka Manispaa kuliondoa jaa hilo. Pia watu wanaoegesha magari yao eneo hilo, wametakiwa wayaondoe. Maelezo. Baraza limeahidi kukusanya taka kila siku. Pia wizara itashirikiana na Kamati ya Skuli kujenga ukuta wa kuzuia uvamizi wa eneo hilo na kuzuia watu kutupa taka.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwanza naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae amenipa nguvu ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili ya kuwasilisha Muhtasari wa Hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa Fedha 2013/2014, kama Kanuni ya 108(14) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2012 inavyoelekeza.

Mhe. Spika, kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii katika kazi zake iliweza kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara zilizo chini ya Kamati hii. Kwa kufuatilia utekelezaji wa malengo ya Bajeti za Wizara, utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na ile ya wananchi. Utekelezaji wa ahadi zilizotolewa wakati wa kupitishwa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 na utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyoagizwa kupitia Ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa mwaka uliotangulia.

Mhe. Spika, pia kamati ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali kwa lengo la kuona hali halisi ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa, katika maeneo hayo na kujiridhisha na utekelezaji na hatimae kushauri ipasavyo.

Mhe. Spika, Kamati yetu ina jukumu la kufuatilia Wizara ya Afya, Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.
Katika mwaka wa Fedha wa 2013/2014 Kamati ilifanya kazi kwa muda wa wiki sita. Unguja kwa vipindi vitatu tofauti, ambapo katika mzunguko wake wa mwanzo ilianza kazi kuanzia tarehe 09/09/2013 hadi tarehe 20/09/2013. Mzunguko wa pili kuanzia tarehe 18/11/2013 - 29/11/2013 na hatimae kumalizia mzunguko wa tatu kwa upande wa Unguja, mnamo tarehe 30/12/2013 - 10/01/2014.

Mhe. Spika, aidha Kamati ilifanya kazi kwa muda wa wiki mbili Pemba. Kuanzia tarehe 13/05/2013 hadi tarehe 24/05/2013 kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa Bajeti katika Idara na Taasisi za Serikali, katika kipindi cha Aprili - Juni 2012/2013.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, napenda kuchukua fursa hii kuwataja wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, ambao kwa namna moja au nyengine tulishirikiana kwa pamoja katika kufanya majukumu yetu. Wajumbe wenyewe ni:-

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma — Mwenyekiti
2. Mhe. Hassan Hamad Omar — Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Farida Amour Mohamed — Mjumbe
4. Mhe. Mwanaid Kassim Mussa — Mjumbe
5. Mhe. Abdi Mosi Kombo — Mjumbe
6. Mhe. Ali Salum Haji — Mjumbe
7. Mhe. Mohamed Mbwana Hamad — Mjumbe

Mhe. Spika, pia napenda kuwataja makatibu wetu wa Kamati ambao huwa tunaambatana nao katika kazi zetu za Kamati, na wamekuwa wakitusaidia kwa karibu katika kufanikisha kazi zetu nao ni:-

1. Ndg. Maryam Rashid Ali
2. Ndg. Asha Said Mohamed

Mhe. Spika, kamati yetu inaipongeza wizara kwa kuweza kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa vipindi tofauti katika mwaka wa Fedha 2013/2014, licha ya kuwa Wizara imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya muda mrefu ya ufinyu wa Bajeti na Uingizwaji mbaya wa fedha.

Mhe. Spika, wizara imekuwa ikitegemea zaidi fedha za wafadhili katika utekelezaji wa shughuli zake za Vitengo, Idara na Taasisi, huku uingizwaji wa fedha za Serikali ukiwa ni wa kusuasua na ambao kiukweli unazorotesha utekelezaji wa shughuli za Wizara.

Mhe. Spika, uchache wa fedha katika Wizara ya Afya umechangia uwepo wa changamoto nyingi ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi kwa haraka. Kwa vile Wizara hii ina umuhimu mkubwa wa kuhakikisha kuwa wananchi wanapatiwa huduma zilizo bora za afya, kwa lengo la kustawisha siha zao.

Mhe. Spika, fedha ni rasilimali na nyenzo muhimu katika utendaji wa shughuli za Wizara, lakini Kamati yetu ina masikitiko makubwa juu ya uingizwaji mbaya wa fedha kwa Wizara. Hasa katika Idara ya Kinga na Elimu ya Afya, kupitia Kitengo cha kupambana na Maradhi yasiyopewa kipaumbele, Kitengo cha Lishe, Kitengo cha Huduma za Matibabu ya Macho ambapo fedha za utekelezaji wa shughuli zao inategemea zaidi wafadhili.

Mhe. Spika, aidha, Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo inajumuisha Hospitali ya Mnazi Mmoja, Hospitali ya Wagonjwa wa Akili na Hospitali ya Mwembeladu, nayo inakabiliwa na changamoto nyingi kutokana na uhaba wa Fedha.

Mhe. Spika, kamati inasikitishwa sana na hali ya Hospitali Kuu ya Mnazi mmoja ambayo ina uhaba wa vifaa, na hata kukosekana kwa vifaa muhimu kama vile *DNA*, na *PCR* ambacho kifaa hicho hutumika kwa kupimia damu za watoto ambao wamezaliwa na mama walioambukizwa Virusi vya Ukimwi.

Mhe. Spika**,** kutokana na kukosekana kwa kifaa hicho katika hospitali ya Mnazi Mmoja, inapelekea damu za watoto waliozaliwa na mama walioambukizwa Virusi vya Ukimwi, kusafirishwa kwenda Hospitali ya Muhimbili kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi, ambapo pia kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa wa majibu.

Mhe. Spika**,** aidha, Kamati yetu haifurahishwi hata kidogo kwa kukosekana kwa tanuri la kuchomea taka katika hospitali. Hali inayopelekea taka kuchomwa pembezoni mwa ufukwe wa bahari na kupelekea athari kwa viumbe waliopo nchi kavu na baharini.

Mhe. Spika, Kutokana na ufinyu wa Bajeti, Hospitali ya Wagonjwa wa Akili kwa upande wa fedha za chakula, fedha zinazopatikana kwa mwezi ni shilingi milioni mbili tu au chini ya hapo, wakati mahitaji halisi ni shilingi milioni sita na kupelekea wagonjwa kupatiwa mlo mmoja tu kwa siku, ambao huwa si mlo kamili kwa mahitaji ya wagonjwa hao. Vile vile Hospitali ya Mwembeladu nayo inakabiliwa na tatizo hilo hilo la chakula kwa wagonjwa, kwa zaidi ya miezi nane sasa.

Mhe. Spika, kamati imebaini kuwa changamoto nyingi ambazo wanakabiliana nazo wizara, zinatokana na ufinyu wa bajeti na Uingizwaji Mbaya wa Fedha kwa Wizara hii. Hivyo Kamati inaitaka Serikali kuipatia Wizara Fedha ambazo zinapitishwa na Baraza la Wawakilishi wakati wa vikao vya Bajeti na pia Kamati inasisitiza fedha hizo ziingizwe kwa kipindi kilichopangwa na kwa ajili ya matumizi yaliyokusudiwa. Kufanya hivyo kutaiwezesha Wizara kufanya majukumu yake kwa ufanisi na kufanikiwa kuondoa kasoro mbali mbali zilizopo.

Mhe. Spika, kamati inaona umuhimu wa kuwepo kwa Baraza la Wauguzi na Baraza la Tiba Asilia na Tiba Mbadala. Mabaraza ambayo yote kwa pamoja yanatekeleza kazi ambazo ni muhimu kwa jamii.

Mhe. Spika, Baraza la Wauguzi miongoni mwa majukumu yake ni kusimamia na kuhakikisha kuwa utoaji wa huduma za uuguzi na ukunga zinakuwa katika kiwango kilichowekwa. Kwa kufuata miongozo ya taaluma za Wauguzi. Aidha, Baraza linasimamia haki za wauguzi na haki za jamii katika kupata huduma bora.

Mhe. Spika, Malengo ya Baraza la Wauguzi ni mazuri na ya msingi, lakini Kamati imebaini kuwa malengo ya Baraza yanashindwa kutekelezwa kutokana na kukosa fedha. Baraza limekuwa linashindwa hata kufanya vikao vya kawaida kwa zaidi ya miaka kumi sasa, hali inayopelekea kukosa maamuzi ya pamoja baina ya wajumbe wa Baraza na kushindwa kutoa miongozo ya maadili kwa wauguzi.

Mhe. Spika, mbali na kukosa kutekeleza majukumu yake ya kawaida, Baraza pia linakosa fursa ya kushiriki katika Mikutano ya kitaifa na Kimataifa kama vile *International Council of Nurses,* kutokana na kuwa Tanzania Bara inawawakilisha Baraza la Wauguzi la Zanzibar Kimataifa.

Mhe. Spika, kutokana na matatizo yaliyopo na yanayoendelea kujitokeza katika Baraza la Wauguzi, Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha kuwa Wizara inafuatilia upatikanaji wa fedha kwa Baraza ili liweze kutekeleza majukumu yake. Vile vile, Kamati inaitaka Wizara kutafuta mbinu ambayo itawezesha

Baraza la Wauguzi Zanzibar kuweza kushiriki mikutano ya kitaifa na kimataifa, ili kuenda sambamba na mabadiliko ya ukuaji wa taaluma ya uuguzi kwa kubadilishana uzoefu na watu wengine.

Mhe. Spika, kwa upande wa Baraza la Tiba asilia na Tiba Mbadala, nalo linakabiliwa na changamoto ya fedha na kupelekea kushindwa kufanya majukumu yake.

Mhe. Spika, kamati inaitaka Wizara kuwa karibu na Baraza la Tiba Asilia na Tiba Mbadala. Pia kulisimamia kwa kulipatia fedha za bajeti ili litekeleze majukumu yake.

Mhe. Spika, wizara ikilisimamia Baraza ipasavyo, itaweza kulisaidia Baraza lenyewe katika kufanikisha majukumu yake na kuisaidia jamii ya kizanzibari juu ya kupata uelewa wa namna bora ya kutumia dawa za asili, ambazo Baraza wanazisimamia na kwa vile kumekuwa na ongezeko kubwa la dawa hizo ndani ya nchi yetu.

Kamati inaishauri Wizara kufanya upanuzi na ukarabati wa majengo ya Wizara ambayo yamekuwa ni machakavu na hayatoshelezi. Kamati imebaini kuwa Wizara ina uchakavu mkubwa wa majengo yake kama vile vituo vya afya na nyumba za madaktari. Sambamba na hilo Wizara ina ufinyu wa majengo, ambapo miongoni mwa majengo hayo ni Kitengo cha Huduma za Matibabu ya Macho na Kitengo cha Afya ya Wafanyakazi.

Mhe. Spika, kamati imegundua kuwa usafiri ni changamoto nyengine ambayo inaikabili Wizara katika kutekeleza majukumu yake. Kamati ilipofanya kazi katika maeneo tofauti ya Wizara ilibaini kuwa kukosekana kwa usafiri wa uhakika katika Hospitali ya Mwembeladu, Bodi ya Ushauri wa Hospitali binafsi na kwa baadhi ya Ofisi za Timu za Afya za Wilaya kunawakosesha wafanyakazi kutekeleza kazi za ufuatiliaji, ambazo zina umuhimu katika kufanikisha malengo ya Wizara.

Mhe. Spika, aidha Kamati iligundua kuwa Hospitali ya Wagonjwa wa Akili nayo ina tatizo la gari kukosa mafuta, na kupelekea gari hiyo kushindwa kutumika.

Mhe. Spika, kamati inaitaka Wizara kulitafutia ufumbuzi tatizo la Usafiri kwa Hospitali ya Mwembeladu, Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi na Ofisi za Timu za Afya za Wilaya na pia Kuitaka Wizara kuhakikisha kuwa gari la Hospitali ya Wagonjwa wa Akili linapatiwa mafuta ya kutosha ili litumike kwa shughuli za hospitalini hapo.

Kitengo kina jukumu la kuweka taarifa za wagonjwa ambao wanafika Hospitalini kwa ajili ya kupata huduma za kimatibabu. Kiukweli, taarifa zinazoekwa na Kitengo hicho ni muhimu sana kwani zinasaidia katika kumpatia mgonjwa matibabu.

Mhe. Spika, kamati imesikitishwa sana na ufinyu wa nafasi katika Kitengo pamoja na miundombinu ya umeme kutokukidhi haja. Ufinyu wa nafasi umepelekea mafaili ya wagonjwa kutowekwa katika mpangilio mzuri. Pia kutokana na miundombinu ya umeme kutokukidhi haja, usiku unapoingia inakuwa ni vigumu na usumbufu mkubwa katika kupata taarifa za wagonjwa.
Mhe. Spika, kamati yetu inaitaka Wizara kukiboresha Kitengo cha Takwimu za Hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na kufanya utaratibu wa kupata eneo jengine la kutunza kumbukumbu za wagonjwa vizuri. Kwani kiukweli eneo linalotumika sasa ni finyu na mafaili ya wagonjwa, yanashindwa kupangwa katika utaratibu mzuri.

Mhe. Spika**,** mbali na changamoto ambazo Wizara inakabiliana nazo, Kamati inapenda kutoa pongezi zake za dhati kwa Wizara hii kwa kuweza kuendelea kufanya kazi zake katika mazingira magumu na kuweza kufanikisha Ujenzi wa kituo cha afya Mwera. Pamoja na Nyumba ya wafanyakazi, ambapo ujenzi huo upo katika hatua ya mwisho ya kumalizika ikiwemo utiaji rangi, pamoja na ujenzi wa uzio kwa upande wa Unguja. Aidha, kwa upande wa Pemba, Kamati inaipongeza Wizara kwa kukamilisha ujenzi wa wodi ya wazazi na watoto katika Hospitali ya Wete na Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Mzambarauni, pamoja na nyumba ya wafanyakazi kufikia katika hatua ya mwisho**.**

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza wizara kwa utekelezaji wa majukumu yake na pia kwa kutoa mashirikiano katika kipindi chote ambacho Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ilipokuwa inafanya kazi zake.

Mhe. Spika, wizara hii pia inakabiliwa na changamoto ya fedha kama nilivyoweza kueleza mwanzo changamoto hii katika Wizara ya Afya.

Kamati imekuwa inalisimamia deni la fidia la wafanyakazi walioumia kazini kwa kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikifanya kazi zake. Kamati inasimamia deni hilo kwa karibu, kwasababu fidia ni haki ya kisheria kwa kila mfanyakazi kulipwa, pindi anapopatwa na ajali akiwa katika mazingira ya kazi.

Mhe. Spika, kamati imeelezwa kuwa Wizara imekuwa ikitenga bajeti yake ya fedha kwa ajili ya kulipa deni angalau kwa robo tatu au kwa nusu ya deni

liliopo kwa mwaka. Lakini Wizara hushindwa kufanya malipo hayo kutokana na kutoingiziwa fedha za kutosha.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2012/2013 kwa upande wa Unguja, deni lilikuwa ni shilingi milioni arubaini na tano (45,000,000) na matarajio yalikuwa ni kupata kiasi cha shilingi milioni ishirini (20,000,000), ili kupunguza deni . Lakini fedha zilizopatikana zilikuwa milioni kumi na moja (11,000,000) na kuweza kupunguza deni kwa kiasi kidogo.

Mhe. Spika, aidha katika Bajeti ya mwaka wa Fedha 2013/2014 Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto imetenga Jumla ya shilingi milioni hamsini (50,000,000) kwa ajili ya malipo ya fidia, Unguja na Pemba. Katika kipindi cha robo ya mwanzo ya Bajeti ya mwaka wa Fedha 2013/2014 (Julai/Septemba),Wizara kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii imeweza kulipa shilingi milioni mbili (2,000,000) kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Pemba, hakuna fedha yoyote iliyopatikana kwa ajili ya malipo ya fidia.

Mhe. Spika, mbali ya deni hilo pia kuna wafanyakazi wengine ambao bado wamo katika uhakiki. Kwa uapade wa Pemba ni wafanyakazi 23 wanaodai shilingi milioni ishirini na sita, laki tano na thalathini na tano elfu, mia moja na sabini na saba na nukta tano nane (26,535,177.58). Kwa upande wa Unguja ni watu kumi ambao wanadai shilingi milioni moja laki mbili,thalathini na sita elfu mia saba na mbili (1,236,702).

Mhe. Spika, kutokana na Ukubwa wa deni ni dhahiri kuwa Wizara inashindwa kulilipa deni hilo kwa wakati. Kwa hivyo, Kamati iliona haja ya kufanya mazungumzo baina ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto na Wizara ya Fedha. Baada ya mazungumzo hayo Wizara ya Fedha iliahidi kulipa deni lote liliopo sasa la fidia la shilingi milioni tisini na mbili, laki nane arubaini na nne elfu mia tano na thamanini na sita (92,844,586) kabla ya kufika mwishoni mwa mwezi wa Machi 2014, baada ya kukamilisha taratibu ikiwemo uhakiki wa madeni hayo.

Mhe. Spika, kwa dhati kabisa Kamati inaipongeza Wizara ya Fedha kwa uamuzi wa kutoa ahadi ya kulilipa deni la fidia kwa wafanyakazi walioumia kazini. Aidha, Kamati inasisitiza kubuniwa utaratibu wa kuweka fedha maalum kwa ajili ya malipo ya fidia, ili isije ikatokea tena mrundikano wa madeni ya fidia.

Kamati inaunga mkono jitihada za Wizara za kuanzisha Kamati za Shehia zinazoshughulikia maswali ya kuzuia na kupinga vitendo vya udhalilishaji, katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu. Miongoni mwa maeneo

yaliyoanzishwa Kamati hizo ni Shehia ya Matetema na Shehia ya Mahonda. Kiukweli Kamati hizo ni muhimu sana, kwani kumekuwa na ongezeko kubwa la vitendo vya udhalilishaji katika jamii.

Mhe. Spika, kamati hizo huwa zinafanya kazi kubwa katika jamii, lakini zimekuwa na masikitiko juu ya kesi zinazokosa ushahidi kwa vile zinarudisha nyuma jitihada zao. Hivyo, Kamati yetu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inaitaka Wizara kuendelea kuishajihisha jamii kushikiri kikamilifu katika kutoa ushahidi wa kesi za udhalilishaji, ili zipatiwe ufumbuzi na pia Wizara kuendelea kuzisimamia kamati hizo, ili ziweze kupata maeneo rasmi ya kutekeleza shughuli zao.

Kamati ilifanya ziara katika nyumba ya kulelea watoto Mazizini na kuona hali za watoto ambao wanaendelea kupata huduma katika nyumba hiyo. Kiujumla wapo katika hali nzuri, lakini Kamati imebaini kuwa walezi wanaowahudumia watoto hao hawana ujuzi wa kutosha wa kuwahudumia watoto, ambao watakuwa na mahitaji maalum pindi inapotokezea kuletwa katika nyumba hiyo.

Mhe. Spika, Kamati inaitaka wizara kuwapa mafunzo wafanyakazi wanaolea watoto katika nyumba hiyo. Mafunzo ambayo yatawasaida katika kumudu kulea watoto wa aina tofauti wakiwemo watoto wenye mahitaji maalum.

Kamati imeridhishwa sana na jitihada za wizara za kuzifanyia matengenezo nyumba za wazee Sebleni na inaitaka Wizara kuzipatia nyumba hizo wahudumu wa kutosha, ili ziweze kutunzwa vizuri. Aidha, Kamati inaishauri wizara kuwapatia wazee usafiri wao wa uhakika, ambao utatumika katika kufanikisha shughuli mbali mbali katika nyumba hiyo, ikiwemo kuwapeleka wazee hao hospitali pindi wanaposumbuliwa na maradhi.

Kamati imesikitishwa na hali ya Ofisi ya Idara kwani ni chakavu na haitoshelezi kwa mahitaji yao. Kamati iliarifiwa kuwa Idara imepatiwa jengo jengine eneo la Migombani kwa ajili ya Ofisi yao, lakini Kamati ilipolitembelea ilibaini kuwa jengo linahitaji matengenezo makubwa kabla ya kuhamiwa. Hivyo, Kamati inaitaka Wizara kuipatia Idara hii fedha kwa ajili ya kulifanyia matengenezo jengo la Migombani ili liweze kuhamiwa na wafanyakazi wafanye kazi zao kwa ufanisi.

Mhe. Spika, Idara ya Mikopo ina jukumu la kuwapatia mitaji wananchi kupitia mikopo nafuu na huduma za ushauri ili wananchi watumie mikopo hiyo kwa ajili ya shughuli za uzalishaji na kunyanyua hali zao za maisha na kiuchumi.

Mhe. Spika, Idara inaendelea kutoa mikopo kwa wananchi, lakini tatizo lilopo katika jamii ni mtazamo hasi juu ya Mifuko inayosimamiwa na Asasi za Serikali. Hivyo Kamati inaishauri wizara kuendelea kutoa elimu katika jamii ili mikopo inayotolewa waitumie ipasavyo na kuondokana na dhana mbaya juu ya mikopo hiyo.

Mhe. Spika**,** Wizara ya elimu na Mafunzo ya Amali ni miongoni mwa Wizara tatu ambazo Kamati yetu inazisimamia ambapo majukumu makubwa ya Wizara hii ni kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora nchini kuanzia maandalizi, msingi, sekondari hadi vyuo vikuu. Aidha, Wizara inaratibu na kufanikisha upatikanaji wa elimu ya ufundi stadi kupitia vyuo na vituo vya mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika**,** kama tunavyofahamu kwamba katika miaka ya hivi karibuni, elimu yetu imekuwa ikishuka kutokana na ufaulu mdogo wa wanafunzi wetu katika mitihani ya Taifa hasa ya kidato cha nne. Hali inayosababishwa na matokeo mabaya kwa watahiniwa hao, na kupelekea kushuka kwa kiwango cha wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu mbali mbali kutokana na kutokuwa na sifa zinazotakiwa. Hali hii pamoja na mambo mengine, inasababishwa na matatizo mbali mbali yanayoikabili sekta ya Elimu na Wizara kwa ujumla wake.

Mhe. Spika**,** Kamati imebaini kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekuwa ikishindwa kukamilisha na kufanikisha malengo wanayojipangia katika kuimarisha Sekta ya Elimu nchini, kutokana na bajeti finyu wanayopangiwa. Lakini pia ufinyu wa uingizwaji wa bajeti yenyewe.

Hali hii husababisha kuzorotesha Elimu visiwani mwetu kwani hupelekea uchakavu wa miundombinu ya skuli kama vile madarasa, uchache wa walimu, ukosefu wa madawati na mambo mengi ambayo Wizara inashindwa kuyatekeleza kutokana na kutokuwa na fedha za kutosha.

Mhe. Spika**,** Kamati imesikitishwa sana na taarifa ya uingizwaji wa fedha za bajeti. Hali ambayo ni ya kusikitisha na kukatisha tamaa katika kufikia malengo ya kuboresha Elimu visiwani mwetu. Kamati katika suala hili la uingizwaji wa fedha usioridhisha, Kamati inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuipa kipaumbele sekta ya elimu katika kuhakikisha kuwa; kwanza inaipangia bajeti ya kutosha kwa lengo la kufanikisha malengo ya Wizara hii muhimu. Na pia kuhakikisha bajeti hiyo itakayoidhinishwa kuwa inaingizwa kwa wakati na kwa mujibu wa mahitaji yaliyopo. Ili kuweza kufikia malengo ya kukuza maendeleo ya elimu nchini, kwani ni dhahiri kuwa Taifa lolote lenye vijana walioelimika hupiga hatua kubwa ya maendeleo.

Mhe. Spika, kamati inaipongeza Wizara kwa kukamilisha ujenzi wa skuli zake za Sekondari za ghorofa zilizopo Kiembesamaki, Mpendae na Faraja iliyopo Kwamtipura. Ni dhahiri kuwa wanafunzi wetu watapata fursa ya kuendelea na elimu ya sekondari katika skuli za kisasa kabisa. Mbali na pongezi hizo, hali ya miundombinu ya skuli za Unguja na Pemba si ya kuridhisha kwani baadhi ya Skuli ni chakavu na mbovu sana kiasi ya kuwa ni hatari kwa wanafunzi wetu kuendelea kusoma katika skuli hizo.Madarasa yanavuja, hayana sakafu ya kuridhisha na pia wanafunzi hulazimika kukaa chini kutokana na ukosefu wa madawati.

Mhe. Spika, Kamati imesikitishwa sana na hali hii kutokana na kwamba imepata wasi wasi mkubwa kuwa endapo wanafunzi walioandikishwa mwaka huu kujiunga na darasa la kwanza, wote wameweza kupata nafasi kutokana na baadhi ya miundombinu ya skuli zetu kuwa mibaya sana.

Mhe. Spika, hivyo kutokana na hali hii Kamati inaitaka serikali kulichukulia jambo hili kuwa ni la muhimu na la dharura kwa kuhakikisha kuwa inaipatia Wizara fedha kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo skuli mbali mbali ili kunusuru maisha ya wanafunzi na kuboresha elimu nchini.

Kuhusu Suala la Uhaba wa Walimu

Mhe. Spika, uhaba wa walimu katika Skuli za Msingi na Sekondari, bado ni changamoto kubwa inayoikabili Sekta ya Elimu nchini. Kwa upande wa skuli za msingi kuna msongamano wa wanafunzi, lakini walimu ni wachache na hawatoshelezi kumudu kusomesha kwa umakini wanafunzi hao.

Mhe. Spika, skuli za sekondari nazo zinakabiliwa na upungufu wa walimu hususan walimu wa sayansi, hali ambayo hupelekea wanafunzi kupata matokeo mabaya hasa kwa masomo ya sayansi na hatimae kushusha kiwango cha elimu nchini. Hivyo, Kamati inaishauri serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuongeza nafasi za ajira kwa walimu ukizingatia kwamba kuna wahitimu wengi wa kada mbali mbali za ualimu ambao bado wanasubiri kuajiriwa.

Kuhusu Suala la Ukosefu wa Hatimiliki za Maeneo ya Skuli

Uvamizi wa maeneo bado ni changamoto inayozikabili maeneo mengi ya skuli na kupelekea migogoro baina ya jamii na Wizara ambayo ndio wamiliki wa skuli zetu. Chanzo cha tatizo hili ni kukosekana kwa hatimiliki ya maeneo ya skuli, Hivyo, hupelekea kutokea kwa baadhi ya wajanja miongoni mwa jamii na kudai kuwa maeneo hayo ni ya kwao. Mfano wa hayo ni skuli ya Fuoni Kitongani, Chuo cha Kiislamu Micheweni, Skuli ya Ufundi Kengeja na

kadhalika. Hivyo, Kamati inaitaka Wizara kutafuta namna ya kulishughulikia suala hili na kuhakikisha kuwa wanakuwa na hatimiliki kwa skuli zote ambazo zinamilikiwa na Wizara.

Kuhusu Suala la Utoro wa Wanafunzi

Mhe. Spika, Kamati imesikitishwa na taarifa ya kuwepo kwa utoro wa wanafunzi maskulini, taarifa hizo ni kupitia Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu anbapo miongoni mwa majukumu ya msingi ya ofisi hii ni kukagua skuli mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kuwa skuli zote kuanzia maandalizi hadi sekondari zinatoa elimu iliyo bora.

Mhe. Spika, katika kufanikisha majukumu yao hayo wamegundua kuwa kuna tatizo la utoro katika skuli mbali mbali hasa katika skuli zilizopo katika maeneo ya ukanda wa utalii. Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu katika kutekeleza wajibu wao wamewashauri walimu wakuu njia mbali mbali katika kukomesha hali hii kwani huchangia kushuka kwa maendeleo ya elimu nchini.

Mhe. Spika, Kamati inaishauri Wizara ya Elimu kupitia Ofisi yake ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu kuwashajihisha wanafunzi kupenda kuhudhuria skuli na vile vile kushirikiana na Kamati za Skuli, walimu na wazee wa wanafunzi ili kupunguza utoro maskulini.

Kuhusu Suala la Uhaba na Ufinyu wa Nafasi (Ofisi)

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inakabiliwa na ufinyu wa nafasi kwa ajili ya ofisi zao. Kimsingi Wizara ina Idara na Vitengo vingi ambavyo vyote hulazimika kujibana katika jengo la Makao Makuu ya Wizara kutokana na kuwa hawana sehemu nyengine ya kufanyia kazi. Jengo la Wizara bado halitoshelezi kutokana na wingi wa vitengo na wafanyakazi wake. Hivyo, Kamati inaishauri serikali katika mpango wake wa ujenzi wa ofisi za Mawizara ya Serikali kuiangalia tena Wizara ya Elimu ili waweze kupata ofisi zaidi kwa baadhi ya Idara na Taasisi za Wizara hiyo.

Mhe. Spika, kiujumla huo ndio muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Maendelo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mujibu wa matakwa ya kanuni ya 108 (14) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2012. Ripoti ambayo kwa uthabiti wake imetoa ushauri na maagizo mbali mbali kwa Wizara na Taasisi ambazo Kamati inazisimamia kwa lengo lile lile la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo na katika kuliletea Taifa tija na maendeleo yaliyokusudiwa.

Mhe. Spika, kwa kumalizia napenda kuchukua nafasi kuwashukuru Mawaziri na Manaibu Waziri wa Wizara hizi, pamoja na watendaji wao wakiwemo Makatibu Wakuu na Manaibu Katibu Wakuu kwa mashirikiano yao wakati wote wa kazi za Kamati. Bila ya mashirikano yao tusingeweza kufanikisha kazi hizi kwa manufaa ya watu wetu.

Aidha, shukrani za pekee nazielekeza kwako Mhe. Spika, kwa ushauri na miongozo mbali mbali ambayo huwa unatupatia mara kwa mara katika kutekeleza kazi zetu za Kamati. Hakika miongozo yako daima hutuelekeza na hutupa mafanikio katika kazi zetu.

Mhe. Spika, baada ya kuyasema hayo, nasema ahsanteni kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha**.** Ahsante.

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti, tunakushukuru kuwasilisha ripoti hiyo. Mjadala uanze. Namkaribisha Mhe. Jaku Hashim Ayoub na baadae Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Lakini Waheshimiwa Wajumbe niwaombe muda wetu kidogo uko finyu. Kwa hiyo, tujaribu kujipanga vizuri ili tuweze kumaliza shughuli hii leo wakati wa jioni, ili kesho Mungu akipenda tuendelee na shughuli nyengine. Naomba sana kwamba tujibane kidogo ikibidi tuongeze muda jioni ili kazi hii imalizike leo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuwa mchangiaji wa mwanzo kama Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein katika uteuzi wake alipotua katika ofisi yake Wizara ya Afya aliiteua mwanzo kuliko Wizara zake zote. Na kafanya hivi nafikiri kwa makusudi kuona umuhimu wa afya na wananchi wake.

Vile vile, nimshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwa jitihada anazochukua kwa wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba. Ikiwemo lile alililoliondosha la huduma za wazazi, suala ambalo lilikuwa ni zito kwa wananchi wa visiwa hivi vya Unguja na Pemba.

Vile vile, niendelee tena kutoa mkono wangu wa pole Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema Dkt. Malik Abdalla Juma kutokana na hali yake. Kwa hiyo, namuombea dua Mwenyezi Mungu amjaalie hali yake izidi kuimarika siku hadi siku. Na hichi ndio kioo cha Wizara ya Afya.

Baada ya hapo Mhe. Spika, nianze katika Wizara ya Afya kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Agizo namba moja. Kamati imeagiza Wizara kuhakikisha kuwa inajenga hoja za msingi kwa Serikali Kuu ikiwa kuwepo uhakika wa upatikanaji wa fedha kwa ununuzi wa dawa. Kamati imebaini kuwa hakuna uhakika wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa na badala yake serikali hukaa muda mrefu na kutoa fedha chache zisizokidhi haja kuwategemea wahisani *DANIDA.*

Mhe. Spika, mtegemea cha ndugu hufa maskini. Mimi kabla hujanihamisha katika Kamati hii hapa nilionekana mchungu na baadhi ya Wajumbe wenzangu. Kilitokea kipindupindu miaka mitatu ya nyuma kama tunakumbuka, nakumbuka mimi wakati huo sijawa Mwakilishi. Wafadhili walikuwa ni watu wawili Marehemu Said Battash wa Mkunazini na wa pili mfanyabiashara maarufu Ndugu Said Salim Bakhressa, ndio walichangia madawa. Mwenyezi Mungu awajaalie na aliyekwenda mbele ya haki Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi. *Amin*.

Niliwaambia mimi Wizara ya Afya katika Kamati kwamba lazima watenge shilingi milioni mia tatu, hamjui saa ngapi maradhi haya ya kipindupindu yatakuja, wala dakika gani. Ikawa pana ubishi hapa, nikawaambia mimi nipo tayari kwa lolote kwa suala hili. Akataka kushtakiwa mwandishi mmoja kwa suala la gazeti la Nipashe wakawa wakali hawa. Wakenda tukakutana wakarudi mwisho wakakubali kuona. Huwezi kumtegemea mtu mpaka akuletee pesa huku wananchi wazidi kuumia, si utaratibu mzuri. Baadae nawashukuru sana wenzangu Wizara ya Afya wakalisikia na wakaliona umuhimu wake.

Mhe. Spika, nije katika ufafanuzi kifungu cha pili, asilimia 37.81 Wizara ya Fedha imekuwa ikiwapa tabu sana Wizara ya Afya. Na mimi itafika siku nitawaomba Wajumbe humu tugome, nitathubutu kufanya hivyo kama yalivyotokea Uganda. Hawa tulikuwa tunawalaumu siku zote watendaji wa Wizara ya Afya, Waziri wa Fedha hawawezeshi Wizara ambayo ni muhimu hakuna kinachoendelea. Hii bajeti yao haifiki asilimia 60, hii Wizara nzito. Juzi nilimpigia simu Waziri wa Fedha huyu nikamwambia bwana nipo hospitali kuna mgonjwa wangu hapa inatakiwa *x-ray* Mnazi Mmoja hamna.

Nikapiga bahati nzuri Mhe. Waziri wa Fedha akapokea simu hiyo. Akanambia nini tatizo kwani Jaku? Hapa kuna tatizo Mhe. Waziri. Katika marudisho yao za *first track* zikaja kule zinakawia kutolewa. Akanambia hicho kitu mbona si kweli. Ananambia kama inawezekana kufika tarehe 3 hebu angalia. Sasa sijui tukamate wapi ambapo ni haki yao ikafika pale zitoke kwa wakati zile pesa. Wananchi wanazidi kuumia, hali zao ni nzito. Ningemuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha, hili akaliangalia lisije likafika

kama Wabunge wa Uganda walivyofanya wakagomea bajeti ya Wizara ya Afya.

Nije katika agizo namba nne. Katika kutekeleza suala hili Wizara tayari imefanya mchakato wa ununuzi wa mashine ya kuchomea taka. Mhe. Spika, huu ni wimbo wa taifa. Mhe. Spika, hapo nyuma nililipigia kelele suala hili katika Kamati mpaka masuala yakafika Barazani, hii sijui itafika lini.

Baada ya hapo Mhe. Spika, nije katika Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar katika Kitengo cha Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hospitali ya Mnazi Mmoja inakabiliwa na changamoto za uhaba wa vitendea kazi na vifaa vikiwemo vitanda vya kubebea wagonjwa na viti hali ambayo hupelekea usumbufu kwa wagonjwa na wafanyakazi. Mhe. Spika, hii hali inasikitisha sana, inatia huruma sana, mimi nimeshalipigia kelele sana katika wakati huo nilipokuwa kwenye Kamati hii. Sasa itakuwa haya haya tunarudia yale kwa yale utekelezaji haupo. Maisha ya wananchi wetu tunazidi kuyaweka katika hali ya kitendawili. Hivi sasa ukenda hospitali utakaribia kulia kutokana na hali ilivyo.

Mhe. Spika, nije katika Kitengo cha Wagonjwa wa Akili. Mhe. Spika, mpaka *hansard* ninazo. Katika wakati wa bajeti mlisema shilingi milioni mbili kwa Hospitali ya Wagonjwa wa Akili wagonjwa mia kwa siku ni shilingi 700/=, wataishi kweli wale. Atakula nini mgonjwa yule ukizingatia dawa anazotumia pale ni za nguvu. Tuache usafi mle ndani tuangalie ile hali ya yule mgonjwa, kula ndio uhai wa mtu. Mfanyabiashara mmoja ndio kaja akasaidia pale kutoa mikate asubuhi.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, mimi nilimbana hapa akaniahidi na kutokana na muda akanambia angalau milioni sita. Nikamwambia lini? Akanambia niangalie katika mwezi Januari ndio zitapatikana milioni sita hizo. *Hansard* zipo na ninazo Mhe. Spika, sio za kubahatisha. Na katika kuweka ushahidi sawa bora ninukuu Mhe. Spika, maana yake isije ikawa nazungumza kitu ambacho sina uhakika nacho.

Unajua mambo ni mengi yaliyokuwepo hapa Wizara ya Afya. Mhe. Spika, nilipokuwa nachangia nilikaribia kulia Kitengo cha Kidongochekundu *Mental* kutokana na milioni mbili kwa mwezi wanazopewa hazikidhi hata pesa za sabuni. Wakati mwengine hizo fedha kwa kusikitisha hazipatikani kwa wakati. Naomba kumnukuu Waziri wa Afya: "Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwamba suala hili nimelielewa na tumelizingatia katika bajeti ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Maana hizo milioni mbili tulizokuwa tukijikongoja katika hali hiyo tuliyokuwa nayo

katika mwaka uliopita, lakini tutahakikisha kuwa hicho kinapatikana kama inavyohitajika".

Mhe. Spika, bado kitendawili kipo hichi. Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri, anambie tu kutoka milioni mbili ataongeza milioni ngapi? Tukenda mimi na wewe nafikiri utakaribia kulia magodoro hakuna, sabuni za kuogea hakuna. Mhe. Waziri anasema "Mhe. Mwenyekiti, hapa mwisho sikumsikia vizuri". Nikarudia tena hoja hiyo. Bado Mhe. Waziri, mimi nikuombe tena kule hali tete, hali hairidhishi, mimi nipo katika hilo, tuache mahali pa kulala na sabuni. Uliahidi katika Baraza lako hili hili kwamba ifikapo Januari.

Mhe. Spika, kikao hichi hichi nilihoji mimi kuhusu *CT scan* nikaambiwa katika Baraza lililopita kwamba inafanya kazi Mnazi Mmoja. *CT scan* bwana haifanyi kazi mpaka muda huu, sasa kama kuanzia juzi sijui. *X-ray* nimempeleka mgonjwa pale, lakini yaliyonikuta nayajua mimi na Mwenyezi Mungu. Ni kitu cha kusikitisha Mhe. Spika, kitanda kimoja kulaza wagonjwa wawili au watatu ni hatari, haielekei na vitanda vyenyewe wakati mwengine vimetandikwa maboksi yale matupu masponji havina. Si kitu cha kubahatisha Mhe. Spika, toka juzi nakwenda hospitali na Waziri tunakutana mimi hii hali naiona.

Kamati iliyopita iliyomaliza muda wake iliiomba Wizara iangalie kuhusu usafiri madaktari wetu wanapata shida kutoka hospitali ya Mnazi Mmoja kwenda kituo cha daladala pale kilipohamishwa sasa hivi Darajani, wanaogopa maisha yao yapo hatarini. Hakuna utekelezaji wowote mpaka muda huu.

Jengine la kusikitisha Mhe. Spika, mimi juzi hapa nimemuaga Mhe. Ismail Jussa Ladhu, bwana nimepigiwa simu jimboni kwangu Katibu na Mwenyekiti wa Tawi la Kitogani kagongwa na gari ya JKU. Gari ambayo ilikuwa ikitembea njiani ikatoka mpira mmoja ikenda ikamgonga kiuno. Kufika hospitali sikupata huduma daktari hayupo. Mchana huo, sikwambii usiku Mhe. Spika, ikabidi atafutwe daktari aje. Maneno haya Mhe. Spika, nayasema ndani ya moyo wangu, mchana daktari anatafutwa sikwambii usiku. Ikachukua muda kutokana na uzoefu wangu ikabidi kuja daktari, *x-ray* hamna. Ikapigwa moja mawingu matupu haikukidhi akarudishwa mgonjwa akapigwa tena. Dawa hakuna za kumtibu mgonjwa huyo ilibidi kuhangaika sisi wenyewe.

Sasa ikafika usiku mgonjwa kapata ajali, daktari atapatikana wapi si atakufa. Hospitali ya Rufaa inayotegemewa kuitwa hiyo, itafika lini kuitwa jina la Hospitali ya Rufaa. Hatuwezi kwenda kwa mwendo huu. Cha kusikitisha zaidi kuna Kitengo cha Macho kimehamishwa katika hospitali ile,

kimepelekwa Hospitali ya Rufaa, leo mtu anafika pale aende zake Kibweni. Kwa gharama gani ya kwenda kule? Kweli tunakwenda mbele, tunarudi nyuma? Haya ndio malengo tunayoyatafuta?

Mimi ningeomba sana wakatafuta kitengo mle mle ndani katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ikabaki kama Mapinduzi Mpya au wapi. Haiwezekani mgonjwa ameshafika pale akaambiwa nenda katika Hospitali ya Kibweni na ile tunategemea Hospitali ya Rufaa, matibabu yote yanapatikana pale.

Mhe. Spika, jengine la kusikitisha, mimi niwaombe sana wenzangu Wizara ya Afya wawe *serious* katika kuwahudumia wananchi, kuna mengine hayataki bajeti. Hebu tuziangalie *stand* za Mnazi Mmoja zimejaa mabuibui na nyengine kuoza. Hebu tuambizane lile linataka bajeti kweli? Tukubaliane Mhe. Spika, uchafu Hospitali ya Mnazi Mmoja umekithiri sikwambii nje.

Mhe. Spika, toka juzi nakwenda hospitali nikarudi mfululizo. Mimi niwaomba watendaji tuwe makini. Mhe. Spika, wali unaweza ukabadilisha mapishi, wali huo huo unaweza ukaubadilisha ukawa pilau, wali ule ukapika biriani, wali ule ukachanganya na chooko ukapata mseto. Cha kusikitisha wakati mwengine unakwenda hospitali vyumba vya daktari vipo viwili pale, ukafika taa haiwaki.

Mhe. Spika, bila ya kupoteza muda, juzi nilipata mtihani kwa bahati mbaya asubuhi sikuwahi kufika hapa katika Baraza lako. Kwa vile suala lile lililozungumzwa lilinihusu mimi Mjumbe wako alilitolea ufafanuzi Mhe. Waziri wa Afya na vile vile na mimi inabidi nigeuze shilingi upande wa pili ili wananchi na Wajumbe wa Baraza hili wapate kujua ukweli ulivyo. Nadhani ningekuwepo mimi Mhe. Waziri, asingezungumza maana yake nisingekubali ningetumia kanuni.

Kwanza Mhe. Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na marekebisho yake ya mwaka 1980, njia za kuingia ndani humu zipo tatu. Kuna Viti Maalum, uteuzi wa Mhe. Rais na kuchaguliwa na wananchi. Uchaguzi wa wananchi ndio wenye nguvu, wananchi hawachagui saa, muda, wala wakati, wala mvua, wala jua wanapotaka msaada, tofauti na wenzetu uteuzi wa Rais au Viti Maalum wakati wowote anaweza kuja, majukumu yetu yamezidi.

Waziri mimi kuniita msanii, hakunitendea haki, mimi si msanii, wala sikutafuta sifa. Kwani ningetafuta sifa, mimi nimeshamfanyia mangapi Mhe. Waziri wa Afya, mangapi ameshaniomba msaada, hana haja ya kutaja mkono wa kulia usije ukapata habari. Ningechukua waandishi wa habari nikawapeleka mbali ya kufanya mimi mwenyewe kwa nafsi yangu.

Nimeshafanya mangapi Wizara ya Afya au mpaka nitangaze. Ningetaka sifa waandishi ningewaalika.

Leo kwenda kunisambaratisha kama vile inabidi waandishi wa habari wamepanga, nani atakubali. Yeye atakubali kuchukua waandishi wa habari kama vile alivyonisambaratisha halafu wanitoe kwenye mitandao. Mhe. Waziri, kuchukua waandishi wa habari kuwaweka pale nimefanya kosa. Kuwaita waandishi wa habari wakuchukue katika mitandao si kitu cha haki. Mhe. Waziri, mimi nikuombe radhi sana haya ni mambo ya kupita, tusihitilafiane kwa mambo madogo tunakotoka mimi na wewe. Kuna hadithi inayosema *"La tahasadu wala tabaghahu wa kuwnu ibada llahi ikhwan"*. Msioneane choyo wala msidhuriane, ndio maana ya hadithi hii.

Mhe. Juma Duni Haji, nikuombe sana haya yaliyopita yameshapita ndivyo alivyoandika Mwenyezi Mungu, wewe mwenyewe shahidi. Ulinipa simu nizungumze na mfanyakazi ambaye ni wa kile kitengo na ukastaajabu alivyojibu. Unasema askari nikawatukane, mimi miaka mingapi nimeshaingia ndani nimewatukana. Hii mitihani ameshaleta Mwenyezi Mungu, tusije tukahitilafiana. Baada ya kuniomba radhi wewe, mimi nitakuomba radhi wewe kwa kuwa ni mkubwa wangu.

Haya ni mambo ya kupita tu, siasa kesho haipo, tutakutana mitaani kama kawaida. Ule utu wetu na ubinadamu wetu mimi nafikiri uzidi kuendelea, vile vile, ni kitu cha mtihani. Wewe mwenyewe ulinambia mpe askari simu ulisikia matusi aliyojibu yale, akatwambia hapa Mhe. Juma Duni Haji, haingii, wewe huingii pamoja na uwakilishi wako. Mimi nakushukuru sana kuacha usingizi wako kuja kunitafutia njia ya kuingia mle.

Mhe. Juma Duni Haji, mimi nitazidi kukuheshimu na nitaendelea kukuheshimu. Ili kuweka mambo sawa mimi ni mlezi, nina watoto si kitu kizuri Mhe. Waziri. Sikuja kutafuta umaarufu mimi, umaarufu ningetafuta sehemu yoyote ningemualika Mhe. Rais katika vyombo vya habari nikafanya jambo lolote sio mle ndani. Mle nilikwenda kwa shida sikwenda kwa raha, tunakwenda kwa dhiki. Yaani nikaache kazi zangu kweli nikashinde hospitali mimi, nina mangapi ya kufanya Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Haya nafikiri muda umemalizika, ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, mimi niende moja kwa moja kwenye Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Mhe. Spika, hupenda sana kutoa wazo ambalo lenye kheri na lenye baraka na ambalo baadae linakuwa hatma katika mambo ya kuweka kumbukumbu.

Mhe. Spika, mwaka jana katika bajeti nilisema kuwepo na benki ya kinamama ambayo ni maalum katika kuwaondolea umaskini. Lakini nimshukuru sana Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, ameipokea yeye na kule ameshaanza kitu ambacho mimi kimenichanganya sana. Kumbe maneno yangu hata nje yanakubalika seuze ndani hapa. Mhe. Spika, naomba tena namwambia Waziri wangu suala hili alitilie maanani kinamama na wao wanataka kujikwamua umaskini kwa kupitia benki zao.

Mhe. Spika, hili suala nimeshasema sana kwa uchungu. Tatizo liko wapi Mheshimiwa? Mhe. Waziri aende aka-*organize* katika mabenki. Mhe. Spika, Mhe. Haroun Ali Suleiman, Mwenyezi Mungu amjaalie apone aje kesho. Alisema kuwa tayari kuna bilioni, fedha fulani ameshakuwa nazo, lakini ilikatazwa baina ya bilioni fulani ili kukamilisha na *BOT* wamruhusu kuweza kufungua hiyo benki. Sasa tangu siku hiyo si angesema matajiri wapo hawa. Mhe. Spika, naomba sana hili suala linatia uchungu bwana, tuwape haki zao kinamama za kimsingi. Nakushukuru sana Mheshimiwa mwanamama wewe peke yako katika ukumbi huu umepiga makofi kwa kuona uchungu huo, wengine waache walale na sadaka hii isiwafike na wao.

Mhe. Spika, ukurasa huu wa pili, naomba sana umeme wa Zanzibar bado haujatosheleza, wanunuliwe majenereta hawa, kauli hii mimi sijakubaliana nayo. Umeme wa Zanzibar unajua upo hafifu. Nakuomba sana Mheshimiwa wanunulie jenereta la *standby*, lazima liwepo. Pale watoto wale wadogo, pana umeme na watu wanaingiliwa ndani kwenda kuibiwa. Nakuomba sana Mheshimiwa, jitahidi kwa uwezo wako na Mungu akusaidie lazima jenereta lipelekwe. Hii lugha mimi bado sijakubaliana nayo.

Mhe. Spika, suala la fidia kama ni kweli Waziri wa Fedha nimshukuru sana kukubali kulipa fidia wafanyakazi hawa. Lakini ni lini? Naomba Mhe. Waziri wa Fedha, njoo unipe jibu zuri nifurahike nalo ili tuweze kuwapa motisha hawa wafanyakazi wetu wafanye kazi vizuri sana.

Mhe. Spika, nimshukuru tena Mhe. Waziri, alivyoona hali halisi ya skauti katika Sherehe za Kutimiza miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar na ameahidi kuwatekelezea wale watoto kiasi cha kupata angalau wakanunua zile nguo. Kwa sababu mtu anakuja shati la bluu, suruali nyeusi. Kwa kweli Mhe. Waziri, nakuomba sana suala la hawa skauti jamani tuwape na wao nafasi yao tuwasaidie, lakini serikali imewaacha. Naomba sana Mhe. Waziri, pigana nao na mimi nitakusaidia kwa hali na mali ili vijana wetu waje juu.

Mhe. Spika, natoa ushauri wangu Mawaziri watatu lazima mkae pamoja. Na hili hata kwa Mwenyezi Mungu tutaulizwa haya mambo, msifanye masihara. Utaulizwa wewe ulipokuwa kiongozi ulitoa ushauri gani. Tusisahau jamani ile

sura yenyewe nimeisahau kidogo kwa kuwa kile kitabu sijakichukua, lakini mpaka aya ningeitoa. Naomba Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Waziri wa Kazi na Utumishi wa Umma na huyo mama mkae muweke jopo lenu, siku moja muwatafutie jinsi gani ya kuwafanyia vijana wetu pamoja na kinamama kupata ajira.

Mhe. Spika, mimi naomba hilo suala mukikaa pamoja suluhu itapatikana, lakini kila mtu akipita njia yake hakuna suluhu. Naomba sana Mhe. Waziri, kwa makusudi wakati wa bajeti sitoliacha. Mimi siku zote huwa ninasema sitomsifu mtu wakati ana baya, hii wazi wala sifichi.

Mhe. Spika, nikiingia katika suala la afya. *Wallahi* mimi nilikuwa mpingamizi sana wa Wizara ya Afya Mhe. Spika, lakini *Wallahi* ninashukuru *alhamdulillah* nenda mapongezi sasa hivi, ile sehemu iliyokuwa ikifungwa vidonda huwezi kuamini wamepaboresha pale Mhe. Spika, sijui pale itakuwa ndio *ICU* ndogo au kitu gani watakuja kunieleza wenyewe wahusika.

Wametengeneza pahali uzuri sana Mhe. Spika, kumbe tembea uone sio ukae nje tu. Lakini la pili Mhe. Spika, kuna jengo sasa hivi linatengenezwa na ndugu zetu wa Spain. Jitihada hizi za Wizara ya Afya, hii nayo ninawapongeza sana, lakini Mhe. Spika, nilisema sana mimi suala la mashine ya kuangalia kensa. Lakini leo *alhamdulillah* sitolisema tena Mhe. Spika, tayari vifaa vimeshatimilia, nimshukuru sana Katibu kwa uwezo wake na jitihada zake za hapa na pale, mtoto wa mjini huyo, amefikisha pahala sasa hivi ni pazuri, hatwendi tena Dar-es-Salaam, anayekwenda Dar-es-Salaam hiyari yake mwenyewe.

Hivi ndivyo tunavyotaka Mhe. Spika, musituone wabaya Mawaziri. Ninamshukuru sana Mhe. Waziri, hakuniona mbaya, aliona hili suala ninamsaidia kwa sababu juzi tulipitisha sheria ya ugunduzi. Kuna mambo nimeshagundua humu humu, sijapewa *certificate*, lakini naomba nipewe *certificate*. Mhe. Spika, tumegundua mengi humu tumeeleza na leo yanafanyiwa kazi na serikali. Hili lazima nishukuru sana Mhe. Waziri wa Afya, pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu, hili tuseme ukweli, panapo ubaya mimi nitasema wala sitoficha.

Sasa jengine Mhe. Spika, mwenzangu kazungumzia *CT Scan* hapa. Sijui ikoje hapa tunamwambia fedha hawajapewa. Mhe. Waziri wa Fedha, inasikitisha leo kusikia Wizara ya Afya unakatwa umeme. Juzi tu wamekatiwa umeme hapo, kauli kubwa imetoka wapi, sijui, lakini Mwenyezi Mungu kaleta rehma zake umeme umerejeshwa. Hivi kweli Wizara ya Afya ukazimwe umeme, kuna mambo mengine hizi wizara nyengine ni muhimu sana. Tuliwatukana

wee! mimi sasa hivi siwatukani tena kwa sababu nilichogundua kuwa fedha wanazoingiziwa hazistahiki, wataweza?

Hilo kweli tuseme jamani, sasa tuondoe kuwashutumu ninasema, fedha wanazoingiziwa ni kidogo na kama ni kidogo au kweli waziri wake yupo yule pale atatueleza vizuri hali halisi ilivyo. Lakini fedha ambazo zile ambazo wanazokusanya wenyewe, hebu wapewe wenyewe warudishiwe, zile fedha wanazokusanya mule ndani wapewe wenyewe.

Jengine Mhe. Spika, mpaka lini watarandaranda hawa watu wa macho. Hichi Kitengo cha Macho kila siku wanaranda huku na huku, kuna mashine nyengine ukizitembeza zinaharibika na sijui kama hazijaharibika. Hebu naomba sana Mhe. Waziri, unisaidie lini hawa wataondokana na hii hama hapa mpaka leo wameshaingia kwa Mhe. Hamza Hassan Juma, wanatoa neema huko. *Alhamdulillah* kafurahi sana Mhe. Hamza Hassan Juma, hataki waondoke tena, lakini itakuwa sivyo, operesheni itashindikana vyumba kidogo kule, lakini hata mimi ningeng'ang'ania wasingeondoka. Mhe. Spika, ningeomba sana hilo tuwasaidie sana kutokana na hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, nikiingia katika suala moja la uwezeshaji huo kupitia akinamama niseme kuwa kuna watu wametapeliwa, hawa Mheshimiwa, wamejitahidi sana, naomba Mhe. Waziri, akinamama hawa wajasiriamali wapo. Kuna watu wamekwenda na ujanja kuwatapeli hawa watu na fedha zao wametoa na risiti hizi hapa mpaka leo hakuna kitu. Na suala hili analijua Afisa Tawala wa Mkoa wa Kusini. Naomba Mheshimiwa nenda, hawa watu ni maskini wa Mungu. Watu wamekuja wamejitia kutoka kituo cha mafunzo cha ujasiriamali cha Tanzania, siku hizi watu wana *technique* nyingi za ujanja.

Mheshimiwa nenda usiache kabisa suala hili kawaokoe hawa wajasiria mali, tena wamepitia katika mkono wa serikali. Ni jambo la kusikitisha sana. Afisi ya Mkoa ndio iliyompokea mtu kama huyu, halafu leo wanasema hawamjui kendea wapi, inasikitisha Mhe. Spika. Naomba sana hili suala lifuatilie haraka haraka sana, njoo, *documents* zao hizi hapa nitakupa.

Niende katika Wizara ya Elimu. Wizara ya Elimu Mhe. Spika, ninashukuru sana na nataka niulize suala dogo tu. Hapa sina mambo mengi, kuwa bado utaratibu ule upo wa kuwa tujikusanye wenyewe wananchi kwenye maeneo yetu tuendeleze, halafu juu watamaliza. Bado utaratibu upo na kama upo bado ninashukuru sana, tuendelee, zipo skuli tunajenga kule kwenye majengo yetu. Naomba hilo watuendelezee na kutusaidia.

Jengine niseme hivi karibuni Mhe. Rais, kila siku anapiga kelele, michezo na hasa riadha. Naomba sana Mhe. Spika, hili suala la riadha hivi sasa kama

alivyosema mwenyewe Mhe. Rais analipigia kelele sana lirudishwe kwenye maskuli. Ninaomba sana suala la riadha lirejeshwe kwenye maskuli ili tutafute vipaji, tutafute viwango.

Mhe. Spika, vipaji tunavyo, viwango tunavyo ni wengi tu hawa wanariadha wa zamani wa Zanzibar waliopata sifa wanatokana na maskuli. Naomba sana Mhe. Spika, hilo ajitahidi sana kuweza kutusaidia na nini. Lakini kuna mama mmoja analia haki yake katika eneo la skuli. Eneo hilo ni la Skuli ya Regezamwendo hapo. Eneo hili liliingia katika eka yao. Yeye anachoomba kitu kimoja tu.

Kwa kuwa serikali imeleta neema pale ya kufanya skul, hana tatizo nalo, wala hana ugomvi nao. Lakini anachoomba kuna bakaa iliyobakia, liko sehemu kubwa na kama si hivyo atafutiwe eka nyengine au sehemu nyengine. Hapo siku zote ndio panapokuwa na matatizo. Mtu yule anakuwa serikali ikishachukua haipati sehemu nyengine ya kuweza kumlipa ili aweze kujiendesha katika maisha yake.

Mimi naomba sana Mhe. Spika, hili suala la Wizara ya Elimu wamtafute huyu mtu ambaye mwenye eka hii anaitwa Bwana Ramadhan Masiku. Naomba sana atafutwe huyo, serikali iwe na nia nzuri tu. Ninaipenda sana serikali yetu kwa kuwa nia nzuri kwa kuweza kusaidia suala hilo. Naomba sana hili suala atafutwe huyu hawa warithi wake ili waweze kusaidiwa pa kupewa pengine, tusiwaache hawa watu wanarandaranda, kwa sababu mtu anakuwa anapiga kelele anasema au apewe fidia, kama umepewa fidia au hujapewa fidia, basi tunaomba watafutiwe kijieneo, kwa sababu kuna makaburi yao katika hicho kisehemu kilichobakia, basi hichi kijisehemu waende wakalee makaburi yao ili waweze kukaa pale kuwarehemu wazee wao, sioni mzigo. Lakini tatizo ni utekelezaji, tunakuwa *very slow* sana katika utekelezaji na siku zote ndio tunapopiga kelele ili utekelezaji wetu unakuwa hafifu sana.

Mhe. Spika, kwa kutaka kujali wakati wako kwa kuwa kama ulivyosema Waheshimiwa tuna dakika chache ulizotupa, mimi niseme kuwa niende katika mwenyekiti wa Kamati hii, halafu nimalizie kusema kuna moja nisije kulisahau, jamani hawa Wajumbe wetu wa kamati wa wilaya ya afya, bado nitaendelea kulisema linasikitisha.

Mhe. Spika, ninamalizia kidogo usiwashe taa, ninamaliza kidogo tu kwa uchungu niseme...

Mhe. Spika: Eeh! ninakwambia kwamba una dakika 5 kumalizia**.**

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Haya hazifiki. Sasa Mhe. Spika, wakiwa na kamati kama hii, sio kama wakifika pale watapata *privilege* ya kuwa Waziri wa Afya, akisikia mtu kasema vizuri atampandisha cheo, wasituvuruge sisi Waheshimiwa Wawakilishi kwa kutaka kujipendekeza kwa watu wengine. Mhe. Spika, hili haliwezekani, mimi ninapinga.

Mimi ninataka nikwambie Wilaya yangu ya Kaskazini B, labda awe afisa mpya na kataka kujipendekeza tu. Lakini maafisa waliokuwepo Mhe. Spika, wakinipigia simu tu, mimi mbio nimekwenda. Iweje leo watwambie Wawakilishi hatuwendi tena, kaniita lini mimi. Mimi sikubaliani na kauli yake, asijipendekeze kutaka kuona aonekane mzuri, hakusaidii kitu. Usitumalize sisi wakati wewe una yako. Maana yake mtu anataka kujipendekeza pale kusema mimi fulani nikimwita tu anakuja mbio, Wawakilishi hawatuiti, katuita.

Katika mtu mmoja *active* ni mimi. Sijisifu Mhe. Spika, lakini gusa simu, saa ishirini na nne ipo *open*, niite usiku wa manena mimi ninatoka. Wewe afisa hapo tu unakwenda kutubomoa hivi hivi kwenye kamati, ionekane wewe kama ni mtendaji na sisi wengine si watendaji.

Ninaomba sana huyu afisa alipofika asifanye tena kitendo kama hicho kwa sababu mimi sitomuonea aibu kabisa, mimi sera kawaida yangu au sera yangu mtu simuoni aibu, ninamwambia ukweli akinuna sawa, akifurahi sawa nipo na wewe, lakini asitubomowe wakati hatuna sifa ya kubomolewa.

Ahsante sana ninashukuru sana. Ninaiunga mkono hotuba ya kamati. (*Makofi*).

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subuhana Wataalla* kwa kutujalia uhai na uzima na kuendelea na shughuli zetu hapa Barazani.

Pili, nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi fursa hii ya kuchangia machache katika ripoti hizi za utekelezaji za wizara tatu. Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu ya Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika, niwapongeze wote ambao wamewasilisha ripoti zao hapa. Jana Mhe. Spika, nilisema neno na ninaomba nirejee leo, kwamba haipendezi katika chombo kikubwa kama hichi serikali inapoleta taarifa zake ikawa tuna kaimu, kaimu, kaimu.(*Makofi*).

Mhe. Spika, neno la Kiingereza linalotumika kumuelezea kaimu ni *acting minister*. Lakini *acting* pia kwa lugha ya kigeni ya Kiingereza ina maana ya kuigiza. Na ndio maana wale waigizaji wanaitwa *actors*. Sasa naogopa sana kuja kufikisha pahala Serikali hii ya Awamu ya Saba nikaja nikaita ni *Acting Government*, ninaogopa sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

Na kipimo cha utendaji wa kiserikali Mhe. Spika, kitapimwa kwa hilo na muda haupo mbali sana. Sasa naogopa sana wananchi wasije wakafanya maamuzi kuitafuta *The Real Government* badala ya kuchoshwa na *Acting Government* Mhe. Spika.

Mhe.Spika, ninalisema hilo kwa sababu jana nilitoa mfano wa Mhe. Haji Omar Kheir kwamba anakaimu wizara tatu na yake ya nne. Lakini leo tunajadili wizara moja nzito sana hapa, Wizara ya Elimu. Waziri hayupo, yupo Kaimu Waziri. Sasa Waziri hayupo, hata Naibu Waziri wa Elimu pia hayupo. (*Makofi*).

Mhe. Spika, ninajiuliza hivi serikali hii kweli ipo makini. *Is this government serious.* Jana Mhe. Spika, ilikuja picha si nzuri hata kidogo na hata leo asubuhi si muda mrefu, kwamba *front beach* linakuwa tupu, sasa hivi kidogo angalau afadhali lakini muda mrefu Mhe. Spika, unakuta nafasi za Mawaziri mbele zipo tupu. (*Makofi*)

Mimi katika Mawaziri ambao ninataka niwapongeze sana na leo ninampa haki yake ni Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Abubakar Khamis Bakary. Katika Waziri ambaye muda mrefu sana tunamkuta yupo Barazani mara zote Mhe. Abubakar Khamis Bakary, itokezee dharura ya kweli kweli na ndio inavyotakiwa iwe Mhe. Spika. Kwa sababu asilimia 95 pengine kama si zaidi ya hoja tunazozijadili hapa ni hoja za serikali, wenye hoja hizi ni serikali. (*Makofi*).

Hapa yanaweza kuchomoza mambo ambayo pengine haihusu wizara ile, Waziri akajiona wizara haipo, asipate hapa. Lakini serikali inawajibika kwa pamoja hapa Mhe. Spika, na ndio msingi wa kifungu cha 45 (3) cha Katiba. Kwa hivyo, panaweza kutokea hoja tukataka maelezo ikawa muhusika mwengine ikawa hatumpati Mhe. Spika. Si utaratibu mzuri na ndio maana jana pia nikazungumza kwamba inashangaza, haidhuru leo kidogo kuna mabadiliko juu kwamba tuna wizara tatu tunaripoti za utekelezaji hapa, lakini safu ya watendaji hatuioni. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nimetumia dakika zangu kadhaa kulieleza hili suala, ninasema hili ndio msingi wa wote Mhe. Spika.

Ninaiomba serikali sana katika hili ijirekebishe Mhe. Spika. Kwa sababu kama nilivyosema wananchi wanayaona mambo, wanaweza kufika pahala

wakasema wamechoshwa na *Acting Government* wakatafuta *The Real Government.*

Mhe. Spika, sasa niende katika ripoti. Mhe. Spika, kamati hii inawezekana Wajumbe wengine tukadhani kwamba kwa sababu inaitwa Kamati ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Wanawake, tukawa hatuioni uzito wake. Lakini katika wizara kubwa ambazo zimo katika serikali hii, basi zipo katika kamati hii na mbili kubwa zinasimamia, moja katika huduma nzito katika nchi yoyote sio Zanzibar tu, sekta ya afya na sekta ya elimu.

Mhe. Spika, nimesikiliza kwa makini ripoti za Mawaziri na ripoti hii ya Kamati. Na mimi ninajiuliza Mhe. Spika, hivi kipaumbele cha serikali hii ya Awamu ya Saba ni nini? Kwa sababu Mhe. Spika, msingi wa pato la serikali ni kodi za wananchi na msingi wa mwananchi kulipa kodi katika nchi ni kupata huduma, *tax means services* Mhe. Spika.

Sasa mwananchi anapolipa kodi, lakini yale ya msingi ikawa hayapati, tunajiuliza Mhe. Spika, kutakuwa kweli kuna uhalali wa mtu huyo kulipa kodi. Mhe. Spika, miaka ya nyuma Uingereza wanaolipa kodi waligoma kulipa kodi, wakasema *no taxation without representation.* Hakuna kulipa kodi kama hakuna kuwakilishwa.

Kwa Zanzibar wanaolipa kodi ndio maana wametuchagua sisi Wawakilishi wao kuja kusimamia maslahi yao hapa ya kodi zao. Sasa Mhe. Spika, ninasema hili kwa sababu gani. Tunazozana ikifika wakati wa bajeti itakuja kuwa na mbinde nyengine hapa. Lakini ukitazama sehemu kubwa Mhe. Spika, ni kwamba Wizara hizi mbili haziingiziwi bajeti za kutosheleza.

Sasa mimi nikajiuliza kipaumbele cha serikali hii ni nini, ikiwa hakipo katika elimu na afya. Maana yake kama mwananchi analipa kodi, huduma ya kwanza atakayoitegemea ni elimu na afya. Mhe. Spika, hatuna takwimu tutazingoja katika bajeti, lakini nimepitia hapa haraka haraka. Katika Wizara ya Afya suala la bajeti ya dawa ni wafadhili, suala la kitengo cha lishe wafadhili, suala la kitengo cha macho ni wafadhili, kitengo cha maradhi yasiyopewa kipaumbele ni wafadhili na kamati inaturipotia kwamba zimeshindwa kufanya kazi zake kwa sababu wafadhili wamekuwa hawaingizi fedha za kutosha.

Kwa hivyo, kama hakuna mfadhili maana yake tumelala. Lakini Mhe.Spika, si hayo tu tunakwenda kuchambua utendaji, utendaji utapatikana wapi ikiwa bajeti haziingizwi. Mhe. Spika, ukenda katika Wizara ya Elimu, kamati imebaini na imetwambia katika ripoti katika ofisi zisizopungua tano hizi,

wanalalamika kamati walipokwenda kufanya ukaguzi kwamba bajeti inaingizwa si ya kukidhi haja hata kidogo.

Wametaja humu katika Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu kwenye Wizara ya Elimu, Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi, Taasisi ya Elimu Zanzibar ambayo ndio inayoandaa mitaala, Bodi ya Huduma za Maktaba, Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA*). Moja ninaikumbusha kamati kabisa ni Idara ya Elimu ya Sekondari, bahati mbaya katika ukurasa wa 84 wa ripoti yao hakukuwa na maelezo. Mimi nina wasi wasi labda katika makosa ya uchapaji yameruka kwa sababu pamechanganywa elimu ya sekondari pana *paragraph* moja, halafu kimeingia Chuo cha Ufundi Kengeja.

Nina hakika nako ningepata maelezo Mhe. Spika, pengine hadithi ingekuwa ndio ile ile kwamba bajeti haitoshelezi. Sasa ninajiuliza Mhe.Spika, wakati haya yanatokea huku tunasikia takwimu kila siku tunasifiwa kwamba mapato ya serikali yanaongezeka.

Karibuni nilisoma ripoti moja wakati wa sherehe za Mapinduzi kwamba mapato ya ndani ya yametoka kutoka bilioni kumi na tatu hadi yamefikia bilioni ishirini na tisa kwa mwezi. Sasa nikasema mambo mazuri kwa sababu hizi ni zaidi ya mara ya mbili zilizokuwa zikikusanywa mwaka 2010 Mhe. Spika. Sasa tulitegemea ongezeko hili la kodi limaanishwe ubora wa huduma wanazopewa wananchi wa Zanzibar, wanyonge maskini wanaodhalilika.

Mhe. Spika, kuna hatari ya kufika pahala ya wananchi wetu wakasema kwamba hatushughuliki kuingiza bajeti katika huduma hizi muhimu kwa sababu sisi labda kwa mishahara tunayolipana minono tunapeleka watoto wetu na sisi wenyewe tukiumwa tunakwenda kutibiwa katika hospitali za nje, tunapeka watoto wetu katika skuli za binafsi au vyuo vikuu vya nje, ndio maana wao tunawadharau. Kwa hivyo, wanaweza wakafika hapo wananchi wa Zanzibar wakasema hivyo Mhe. Spika, na hii si nzuri hata kidogo.

Mhe. Spika, pamezungumzwa Hospitali ya Mnazi Mmoja, kimbilio la wananchi wote. Leo tunasema kwamba katika vipa umbele tulivyoambiwa kuifanya hospitali hii kuwa ya rufaa. Lakini bajeti ndio hii. Sasa kunafanyika nini. Matokeo yake Mhe.Spika, ndio maana sichangii kitu kimoja kiliomo ndani, mambo ni yale yale ukisoma ripoti ya utekelezaji wa Wizara ya Afya, mambo ambayo yamelalamikiwa mwaka jana ambayo Waziri leo anajibu kuhusu utekelezaji wake na mengi yamekwama kwa sababu ya bajeti.

Moja wapo nitoe tu Mhe. Spika, ni suala la bajeti ya madawa. Linaonekana hapa ukurasa wa mwanzo, serikali imeingiza asilimia 37 kwenye madawa. Yale yale Mhe. Spika, yanajirejea katika ya mwaka huu. Nilisema jana na

ninaendelea kusema kila mwaka ripoti za kamati zikirudi zinarejesha yale yale. Halafu huku tunaambiwa serikali inafanya kazi, kama serikali inafanya kazi kusawazisha haya, kwa nini yajirejee kila mwaka yale yale katika ripoti za kamati.

Mhe. Spika, niliwahi kusema hapa mwaka jana wakati nikichangia bajeti ya Wizara ya Afya kwamba kwa hali ya afya ilivyo inawezekana kabisa tumeamua kukata bajeti kununua meli, kwa sababu palikuja maafa ambayo yalipoteza roho za watu wasiopungua elfu mbili. Nikasema kwamba pengine haya ni maafa tumeweza kuwakisia hesabu ya watu elfu mbili, wangapi wanakufa katika hospitali zetu kwa kukosa hudumu muhimu na pengine tungefanya hesabu tungeona kuna haja zaidi ya kujikata bajeti zetu tukaimarisha kwanza hospitali zetu ikawa wananchi wanapata uhai wao, mtu anakufa kwa ahadi yake kweli, lakini Mwenyezi Mungu pia kaweka njia ya binadamu kujinusuru.

Yasini usome Mhe. Spika, lakini na mbio uwe nazo. Sasa sisi tumekuwa Mwenyezi Mungu ndio jaa letu, kila jambo tunasema ahadi imeshafika, lakini tumechukua juhudi gani kurekebisha masuala haya.

Mhe.Spika, vifaa vya *DNA*, vifaa *incenerator*, *X-ray*, mambo yamekuwa yanazungumzwa kila mwaka na pengine tulivyosema kwamba hata usafi hauhitaji bajeti, lakini pengine unapoingiziwa asilimia ishirini na nne, tano kwa mwaka. Ukipata wewe unayesimamia utajiuliza ukafanye nini. Pengine ndio hayo mengine yanaharibika mpaka ya usafi. Lakini ninajiuliza huku tunaambiwa mapato yameongezeka, hii pesa kama imeongezeka inakwenda wapi kama haiendi katika hivi vipaumbele.

Mhe. Spika, tusije tukaambiwa kwamba vinakwenda katika miundombinu, maaana mimi ni mjumbe wa Kamati wa Mawasiliano na Ujenzi na huko asilimia ishirini na tano. Vile vile, bajeti ya maendeleo hakuna kitu. Sasa pesa yote inakwenda wapi kama haihudumii wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, pamezungumzwa suala la bajeti. Pamezungumzwa Hospitali ya Wagonjwa Wakili ambapo pamezungumzwa kwamba bajeti ilikuwa milioni sita na milioni mbili. Hii ninakumbuka mimi si kwa Hospitali ya Wagonjwa wa Akili tu. Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais alipotembelea Wizara ya Afya kwa ujumla wake alipata *shock* alipofika akaambiwa kwamba chakula kimesitishwa kutolewa kwa sababu bajeti haitiwi vizuri.

Katika majumuisho ninakumbuka nilisikia katika vyombo vya habari mimi, akaagiza litafutiwe ufumbuzi. Mpaka leo linaendelea vile vile. Sasa ikiwa viongozi wa kitaifa wanatoa maagizo na bado hayatekelezwi. Jana tuliambiwa

na Mhe. Rais hapa kuhusiana *CCTV Camera* katika nyumba ya nyaraka, leo linakuja la chakula.

Sasa hata hawa viongozi wa kitaifa hatuheshimu maelezo yao, yatakuja kuheshimiwa ya Mhe. Jussa au Mhe. Mtando ndani ya Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, niseme katika bajeti ya mwaka juzi sio mwaka jana, mwaka juzi hili halimo katika ripoti ya kamati wala halimo humu, lakini jana Mhe. Salmin Awadh Salmin alitoa indhari na mimi ninatoa indhari kwa Mhe.Juma Duni Haji.

Mwaka juzi nilimwambia atazame sana suala la upelekaji wa wagonjwa wanaopelekwa nje matibabu nchini India katika hospitali ya Miot. Na tulifika pahali tukakubaliana hapa kwamba kuna serikali Wizara ya Afya kutizama upya kwamba hii Miot inaonekana inafanya kibiashara zaidi, lakini wagonjwa wanaopelekwa kutoka Zanzibari hawapewi kipaumbele kiasi hicho, tukasema itafutwe hospitali nyengine.

Mwaka mzima umekwenda na huu tunakata nusu mwaka. Lakini karibuni nimepewa kadhia moja Mhe. Spika, na ninaomba Mhe. Waziri, aitizame tena. Kuna wagonjwa wanaopelekwa na serikali na mgonjwa alipelekwa kutibiwa binafsi, gharama zikafanyiwa uchunguzi na yule kwa sababu yule aliyekwenda kupeleka mgonjwa si mtu aliyekuwa hajui mambo, alifuatilia pale, gharama za zinazopelekwa na wagonjwa wa serikali kwa matibabu yale ni mara tatu ya zile ambazo yeye kalipa yule mgonjwa aliyepelekwa na binafsi na familia yake. Nilimwambia Waziri wa Afya mwaka juzi na ninaendelea kumwambia ajitayarishe kwa bajeti inayokuja hapa, suala hili mimi ninataka maelezo.

Wana *interest* gani wakubwa wa Wizara ya Afya hata kuing'ang'ania Hospitali ya Miot. Mhe. Spika, jengine ninazungumza Wizara ya Afya kwa sababu ndio kwenye uhai wa wananchi. Ili madaktari na wauguzi waweze kuwatibu wengine wao wenyewe wanataka wajihakikishie usalama wa afya zao.

Leo tunaripotiwa humu katika ukurasa wa 64 na 65 ya ripoti ya kamati kwamba Kitengo cha Afya ya Wafanyakazi kuna vyumba vinne kuhudumia Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa ukubwa wake, kuna chumba kimoja. Lakini wafanyakazi wa kuweza kuwahudumia wafanyakazi wenziwao wanatakiwa kumi na tano wapo wanane. Sasa hawa ni jukumu lao kutunza na kusimamia usalama hao wafanyakazi wa Wizara ya Afya ili na wao waweze kutuhudumia vyema sisi wananchi. Hali ndio hii Mhe. Spika.

Mhe. Spika, lakini hali ilivyokuwa mbaya sijui kwa sababu bajeti, kwenye ukurasa wa 66 leo tunaambiwa gari ya Kitengo cha Macho haina dereva, daktari wa macho ndio dereva mwenyewe, yamo humu katika ukurasa wa 66. Someni katika ukurasa wa 66 wa ripoti hii, daktari wa macho mwenyewe ndio dereva wa gari wa kupeleka wagonjwa kuliko waliko kupeleka Mnazi Mmoja. Nimemnukuu sana Waziri Rashid Seif alipokuwa *backbench are we serious*? Akipenda sana kuliuliza swali hili na mimi leo ninaliuliza. Sijui mwenzangu kwa sababu leo yupo mbele kama kishalisahau hili.

Mhe. Spika, leo tunaambiwa humu, nimalizie tunaambiwa Mhe. Spika, kwamba imefika pahala kuna upungufu wa madaktari, wauguzi ndio wamegeuka madaktari. Kila mtu na kazi yake. Hivyo, tukija tukifika pahala tukisema wananchi wengine pengine wanapoteza maisha kwa sababu wanaowahudumia sio fani zao, tutakuwa tunakosea.

Mhe. Spika, kwa hali hii inasikitisha sana. Nimesema Mhe. Spika, katika Wizara ya Elimu muda umekwenda, lakini nilizungumza katika bajeti kwenye idara mbali mbali zile, tumezungumza sana, maana yake ufanisi wa jambo unatizamwa katika *out put, in put ina-reflect out.* Leo wanafunzi wakifeli kwa korija, maana imekuwa kama fito, ikiwa hali ndio hii ya bajeti Mhe.Spika, tutegemee nini.

Taasisi ya Elimu inayotuandalia mitaala haingiziwi bajeti, tutegemee tutazalisha kitu gani. Mhe. Spika, kwa hali hii ninasikitika sana kusema kwamba au kwa lugha ya Mji Mkongwe ninastaafu kusema kwamba hali hii Mhe. Spika, bado kazi kubwa kweli kweli. Na ninasema tena naomba na Mhe. Waziri wa Fedha, ninafikiri nitamsubiri kwa hamu aje atwambie, hii mapato yanayoongezeka yanakwenda wapi, ikiwa kila kamati ikirudi hapa inakuja kututhibitishia kwamba ni ishirini na tano. Mapato yamekwenda wapi.

Mhe. Spika, ninaiunga mkono ripoti ya kamati, ninaziunga mkono ripoti za mawaziri kwa sababu tu kasema maelezo yake yamejitosheleza katika kamati, kwamba hawaingiziwi fedha tutegemee nini. Mhe. Spika, unachopanda ndio unachovuna. Mhe.Aboud Jumbe alikuwa akisema sana ukipanda mbigili utavuna bingili na hapa tunapanda kuangusha elimu ya watoto wetu, tunapanda kuangusha afya za wananchi wetu kutowaingizia fedha za bajeti za wizara hizi ndio matokeo yake haya yaliyokuwepo.

Mhe. Spika, ninasikitika sana na kwa majonzi makubwa ninasema ninaunga mkono ripoti ya kamati, lakini ninasikitika sana na *Acting Government* inavyotufanyia nchi hii. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

(Saa 7.00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika. Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kufika hapa jioni hii. Pili nikushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, pia nitoe pongezi kwa Waheshimiwa Mawaziri wa wizara tatu, kwa kutuwasilishia taarifa yao nzuri, pamoja na watendaji wao wote katika wizara zao. Mhe. Spika, mimi nitaanza kuchangia katika ufinyu wa bajeti na uingizaji mbaya wa fedha.

Mhe. Spika, wakati tulipokuwa tunatembea na kamati. Kwanza nikupe taarifa kwamba mimi ni Mjumbe wa kamati hiyo, kwa hivyo sitokuwa na mengi lakini nataka mule mulimochangiwa na mimi nizidi kuongeza nguvu.

Mhe. Spika, kuhusu uingizaji wa fedha katika mawizara tulipokuwa tunazipitia, kulikuwa kuna taarifa tulipewa za utekelezaji, kwamba taarifa zile hazijatekelezwa. Tukitaka kuuliza majibu yake tunapata kuwa utekelezaji haujatekelezeka kutokana na uingizaji mbaya wa fedha. Kwa hivyo, mimi naiomba Wizara ya Fedha ijitahidi kama vile tunapokuwa tunapitisha bajeti zetu wakati wa bajeti na tukasema kwamba wizara fulani iingiziwe fedha kiasi fulani, kwa taratibu walizojipangia, kwa hivyo Wizara ya Fedha ijitahidi kuwaingizia fedha kama vile tulivyopata taarifa katika Baraza hili.

Vile vile Mhe. Spika, katika uingizaji wa fedha hizi tumepata taarifa kwamba kama kipindi kimepita cha kuingizwa zile fedha, basi kipindi kijacho ina maana zile fedha wanasema zimeruka, ina maana hazirejeshwi tena kuingizwa. Kwa hivyo hili ni tatizo na yale malengo yaliyokuwa yamepangwa na wizara ina maana yameshindikana, kwa sababu inapofika wakati wa bajeti, tunapoletewa bajeti na Wizara ya Fedha na sisi tukaipokea, na tukaona utaratibu huu ndio utakaotumika, lakini katika kipindi hiki cha mwaka mzima kuanzia mwaka 2013 kuingia 2014 tumeshafika nusu ya mwaka, lakini utaratibu kutoka Wizara ya Fedha, fedha zinaingia vibaya, haziingii kama vile zilivyokuwa zimepangwa.

Mhe. Spika, mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri wa Fedha kwamba hii taarifa ya kuwa mwaka huu tunaokwenda nao kwamba fedha zinaingia kidogo kidogo sana tofauti na miaka mingine, taarifa hiyo anayo?

Jengine Mhe. Spika, kwenye Wizara ya Afya. Wakati Mhe. Waziri anatueleza taarifa zake kuhusu *incinerator*, alisema kwamba iko tayari na imebakia kazi kidogo tu ili iweze kufanya kazi. Mimi namuomba mara hii ajitahidi kwa sababu katika kipindi kilichopita cha bajeti Mhe. Naibu Waziri alituambia kwamba kila kitu kuhusu *incinerator* kimeshakuwa tayari. Lakini tangu kipindi kile sasa hivi ni mwezi wa sita bado haijakamilika, lakini Mhe. Waziri leo katwambia kila kitu tayari yamebaki mambo madogo madogo tu itakuwa tayari, kwa sababu pia Hospitali ya Mwembeladu taka zake pia zinakwenda kuchomwa katika hospitali ya Mnazi Mmoja na huko *incinerator* hawana. Kwa hivyo, itakuwa ni hatari, naiomba wizara ijitahidi ili tukija tena kwenye kikao chengine cha bajeti tuhakikishe *incinerator* imekuwa tayari.

Mhe. Spika, kuhusu Hospitali ya Wagonjwa wa Akili. Mhe. Spika, katika hospitali ile wakati tunaipitia kwenye kamati, kwanza haipo vizuri, inatakiwa ikarabatiwe. Pia hospitali ile kuna tatizo, unapotoka katika kitengo kimoja kwenda kwenye kitengo chengine njiani kuna majani, maana yake wewe mwenyewe utaogopa kupita. Kwa hivyo, napendekeza pale kama kuna upungufu wa mfanyakazi wa usafi basi wizara ijitahidi ili itafute mfanyakazi, ili ile hospitali ikae vizuri, kwa sababu wale wagonjwa na wao wana haki.

Vile vile Mhe. Spika, nije kuhusu Dawa. Katika hospitali ile dawa ni hafifu na dawa zake ni za bei ya juu. Kwa hivyo, naiomba wizara iwatizame kuhusu dawa wanazotumia wagonjwa wa akili.

Mhe. Spika, nije katika Hospitali ya Mwembeladu. Kama Wajumbe waliopita waliweza kuchangia kwamba Hospitali ya Wagonjwa wa Akili kuhusu chakula na Hospitali ya Mwembeladu na wao pia wana tatizo hilo hilo, lakini kwa taarifa tulizopata tunarudi tena pale pale kuhusu uingizaji mbaya wa fedha, kwa sababu Mkurugenzi anayeshughulikia hospitali hizi tatu, fedha anazoingiziwa pale ni kidogo, kwa hivyo katika kupangilia mipango yake anaangalia kila pahala ili aweze kupata kidogo kidogo. Kwa hivyo hizo fedha zinazotolewa hazikidhi haja.

Mhe. Spika, pia niipongeze wizara kwa kuipatia gari Hospitali hii ya Mwembeladu. Kwa sababu pale tulipomalizia kamati hospitali walitwambia wana tatizo la gari, kwa sababu gari iliyokuwepo Mnazi Mmoja wakiwa na tatizo ndio waiombe ije pale Mwembeladu ichukue mgonjwa na ichukue taka au saa nyengine wanakwenda kukodi *taxi* ili kumchukua mgonjwa kumpeleka

Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ametwambia kwamba gari imepatikana kwa hivyo ninampongeza sana.

Mhe. Spika, vile vile nije katika Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. Mhe. Spika, mimi nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kamati yetu na Wizara ya Fedha, kukaa pamoja kulishughulikia suala hili la fidia. Kusema kweli Mhe. Spika, suala hili limekaliwa kwa pamoja na hatua zimechukuliwa na mpaka sasa hivi kwa taarifa tulizopata kwamba deni hilo litamalizika mwezi Machi, 2014. Kwa hivyo, nawapa hongera wizara pamoja na Wizara ya Fedha kwa kuhakikisha kuwa deni hili linamalizika.

Mhe. Spika, pia nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kusimamia vizuri ukarabati katika nyumba za Wazee Sebleni. Nampa hongera zile nyumba zimekarabatiwa vizuri, zinapendeza na katika sherehe zetu zile zilikwenda kufunguliwa rasmi. Kusema kweli nyumba ni nzuri tena sana. Mhe. Waziri hongera pamoja na watendaji wako.

Mhe. Spika, hapa hapa kuhusu hizi nyumba ili zibakie vile vile kuwa safi panahitaji paongezwe wafanyakazi, kwa sababu pale katika zile nyumba kuna wafanyakazi kidogo hawatoshi kuweza kutunza nyumba zile.

Mhe. Spika, nikiendelea nije katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ambapo niwapongeze katika utendaji wao wa kazi, lakini pia na wao wana tatizo hilo hilo la fedha, uingizaji wake wa fedha sio mzuri, yaani katika wizara tatu hizi tulizokuwa tumezitembelea katika kamati yetu basi kila tunapofika kutaka taarifa zao basi kazi haziendi kama walivyokuwa wamezipanga kutokana na tatizo la fedha.

Katika Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Spika, niende katika hati miliki za maendeleo ya skuli. Mhe. Spika, katika migogoro hii ya uvamizi wa maeneo ya skuli bado ni changamoto. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali wakae pamoja na Mhe. Waziri anayehusika na ardhi, ili kuona wanapanga mipangilio mizuri ya kuweza kumaliza matatizo haya ya uvamizi na migogoro. Kwa sababu kila tukienda katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuna taarifa kwamba kuna baadhi ya maeneo ya skuli yanavamiwa. Kwa hivyo, naomba suala hili ili limalizike Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na Waziri anayehusika na ardhi basi wakae pamoja ili kuona hili suala linamalizika.

Mhe. Spika, baada ya mchango wangu huo mdogo, nikiwa Mjumbe wa kamati. Mengi yameelezwa katika taarifa yetu iliyowasilishwa hapa asubuhi.

Kwa hivyo, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi, naunga mkono kwa asilimia mia. *(Makofi).*

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia kuja hapa tukiwa wazima wa afya. Pia nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia machache katika ripoti iliyotolewa na Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, pamoja na taarifa za utekelezaji zilizotolewa na wizara zilizohusika.

Mhe. Spika, mimi kama Mwenyekiti wa kamati hii, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru sana Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, (Mjumbe wa kamati hii) ambaye leo aliisoma ripoti hii ya kamati, kwa kweli aliisoma vizuri na ufasaha mkubwa.

Mhe. Spika, mimi nisingetaka kusema mengi sana kwa sababu mengi ambayo tumeyafanyia kazi na tumeyaeleza katika ripoti, basi ndio yale yale ambayo yanaweza kujitokeza katika mchango wangu.

Mhe. Spika, la kwanza kabisa ninalotaka kulizungumza ambalo limejitokeza hapa Mhe. Ismail Jussa Ladhu, alisema kwamba kuna taarifa kuhusu matokeo ya mitihani na akasema kwamba inawezekana kuwa taarifa ile au ripoti ile haikuonesha suala la matokeo ya mitihani. Kwa kweli Mhe. Ismail Jussa alikuwa ana kila haki ya kujua kuwa suala hili limefikia wapi.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013 kulikuwa na changamoto hiyo iliyojitokeza katika matokeo ya mitihani ya kidato cha nne. Kwa bahati nzuri kulikuwa na Tume Maalum ambayo iliundwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa bahati nzuri mmoja kati ya wanakamati wa kamati hii hii iliyopita alikuwa ni Mjumbe wa tume hiyo, ingawa kamati yenyewe hasa haikuhusishwa moja kwa moja. Lakini hata hivyo Mhe. Spika, nakumbuka hapa Barazani, kuna baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe akiwemo Mhe. Hija Hassan Hija walitaka kupata taarifa ya uchunguzi wa tume hiyo, lakini kwa bahati mbaya sana haikufika Barazani.

Mhe. Spika, sisi kama kamati pia wakati wa kazi zetu za kamati tuliliulizia suala hili kwa Mhe. Waziri na yeye aliahidi kulileta Barazani, lakini mpala leo hii bado taarifa hiyo haijafika. Mimi ningeomba sana wizara, kwa bahati mbaya sana waziri hayupo, lakini kuna mwengine ambaye anakaimu na ninaamini kuwa na watendaji wake pia wapo, uwezekano wa kuletwa ripoti hiyo upo. Kwa hivyo, ningeomba sana tupatiwe ripoti hiyo ili iweze kuwasilishwa kwa Waheshimiwa Wajumbe.

Jengine Mhe. Spika, ambalo nafikiri ilikuwa ni vizuri kulitolea ufafanuzi ni taarifa ya matokeo ya darasa la kumi ambayo yamepita. Kwa bahati mbaya sana Mhe. Spika, hii tumeshindwa kutoa kwa sababu kipindi ambacho matokeo yale yametoka, sisi tayari tumeshamaliza kamati. Kwa hivyo, tunaahidi kwamba ripoti nyengine itakayofuata kutakuwa na ripoti kamili ya matokeo hayo.

Mhe. Spika, labda kidogo tu nizungumzie kuhusu Wizara ya Afya. Mhe. Spika, kama walivyotangulia kusema Wajumbe wenzangu, kwamba tatizo kubwa linalojitokeza katika Wizara ya Afya ni ukosefu wa vifaa pamoja na ubovu wa maeneo, ufinyu wa ofisi na mengi mengineyo, lakini yote haya yanasababishwa na nini, yanasababishwa na uhaba wa fedha ambazo wanapatiwa na kwa bahati mbaya sana Mhe. Spika, fedha ambazo zinatolewa hazitolewi kwa wakati, mara nyingi sana fedha ambazo zinatolewa zinachelewa na hii ni sababu kubwa ambayo inasababisha huduma za afya ziwe huduma ambazo zinadhorota.

Mhe. Spika, Mhe. Ismail Jussa hapa alisema kwamba huduma ni muhimu kwa sababu watu wanalipa kodi ili wapate huduma, lakini kwa bahati mbaya sana leo watu hawajui hizo kodi zao zinakwenda wapi. Hili ni tatizo kubwa na sote tunajua kwamba tunapotoneshwa pahala kidogo tu basi tunakimbilia hospitali, tunakimbilia kwa madaktari, lakini madaktari hawana nyenzo za kufanyia kazi.

Suala hili sio kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja tu, lakini Mhe. Spika, tumekuwa tukifanya kazi na Maafisa wa Wilaya katika hospitali zilizokuwemo wilayani, malalamiko yao ni yale yale, na kwa bahati mbaya sana Mhe. Spika, tunapofika kule mpira tunatupiwa sisi Wawakilishi, tunaambiwa Wawakilishi na Wabunge kama serikali haiwezi kufanya kazi, basi na nyinyi msaidie kufanya kazi. Kweli iko sababu na kweli kwa hakika kama kuna uwezo ni sawa Waheshimiwa Wajumbe na Waheshimiwa Wabunge wanaweza kusaidia, lakini kuna pahala ambapo uwezo huo haupo, kwa hivyo hili ni jukumu la serikali.

Mhe. Spika, utakuta vifaa muhimu. Mhe. Mwanaidi Kassim alisema pale *incinerator*. Mhe. Spika, tulipokwenda kule tulipiga na picha, tungekuwa na wasaa au tungekuwa na *screen* hapa tungeweza kuonesha. Hali ni mbaya kabisa ya utupwaji wa uchafu wa hospitali ambayo inaweza kusababisha maradhi, mpaka hii leo *incinerator* haijaweza kupatikana. Tuliambiwa kwamba fedha zipo, labda tunatarajia kwa sababu hii ni nyimbo ambayo tumekuwa tukiisikia siku nyingi, tunatarajia kwamba itakuwepo, lakini kuna vifaa vyengine vidogo vidogo, kama vifaa vya maabara, vifaa vya meno, zote hizo hazina vifaa vya kutosha na ni kwa sababu ya fedha.

Mhe. Spika, vile vile kuna changamoto nyengine, kuna baadhi ya hospitali katika wilaya zina madeni makubwa ya umeme, hawana fedha za kulipa, kuna madeni ambayo saa yoyote wanaweza kukatiwa umeme. Kwa kweli Mhe. Spika, changamoto ni nyingi kwa wizara hii.

Kwa hivyo, ningemuomba sana Waziri yeye ndiye anayejua ufumbuzi wa tatizo hili, sio Wizara ya Afya, tutawakamata sana Wizara ya Afya, lakini mimi ninajua kwa uhakika, kwa sababu Mhe. Spika, nikwambie ukweli tulipokwenda niliwaonea huruma sana wafanyakazi wa Wizara ya Afya, kwa sababu saa nyengine tunashindwa hata kuwashauri kitu. Wanasema hatuna fedha tufanye nini? Hali ndio hii muione.

Mhe. Waziri wa Fedha tunakuomba sana huduma ya afya ni muhimu sana kwa wananchi, kama hii wizara tukiidharau tukawaingizia fedha kidogo au tukawagaia kidogo tu, basi Mhe. Spika, vifo vitaongezeka na wananchi tutawavunja moyo. Kwa hivyo, naomba sana suala hili.

Jengine Mhe. Spika, mimi niwapongeze sana watu wa Wizara ya Afya wako katika mpango wa kuanzisha Bima ya Afya. Hii inaweza kusaidia sana hasa kwa wale wanyonge itawasaidia kwa sababu watakuwa na uwezo wa kudunduliza fedha zao ambazo zitawasaidia pale inapotokea haja ya kupata matibabu.

Kwa hivyo, mimi ningeiomba sana wizara na wamesema kwamba kunatakiwa kufanywe *research* nyingi ili kuangalia uwezekano wa kuwa na hiyo Bima, lakini najua kwamba uwezekano upo, hivyo ningewaomba sana waharakishe ili angalau wanusuru sekta hii ya afya.

Mhe. Spika, changamoto katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni ile ile. Mhe. Spika, uingizwaji wa fedha ni mbaya na ni mdogo mno. Kutokana na bajeti yake wanayoipata asilimia ndogo mno ambayo inaingia katika wizara hii. Mhe. Spika, kuna baadhi ya maskuli yameshaanguka na bado wanafunzi wamo ndani, yakija masika hapa sijui tutawapeleka wapi.

Mhe. Spika, kuna baadhi ya maskuli darasa moja wanakaa wanafunzi 200 au 300, ni katika Skuli ya Mtopepo Mhe. Spika, usishangae, lakini tukiwauliza watendaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wanasema na sisi Waheshimiwa tuna hamu kubwa ya kutekeleza haya. Laiti mngejua, kwa sababu sisi tunayaona kila siku, nyinyi mnakuja mara moja tu hapa, lakini sisi tunayaona kila siku yanatuuma. Ninaamini yanawauma, kwa sababu wengi wa watendaji wale ni walimu, wengine nimesomesha nao wana uchungu na Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali, wanataka kuinusuru sekta ya elimu, lakini wanashindwa hawana nyenzo.

Namuomba tena Mhe. Waziri wa Fedha, hubu tuzipe vipaumbele hizi wizara mbili sasa hivi. Tusizungumze tu, tutende. Madawati bado watoto wanaendelea kukaa chini Mhe. Spika, hali ni mbaya.

Mhe. Spika, nataka nimalizie kwa Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. Mhe. Spika, katika wizara ambayo inanisuuza roho, basi hii ni moja. Wizara hii naweza kusema nikimaliza wizara nyengine na mara nyingi sana inakuwa ni wizara ya mwisho ambayo tunakwenda, napata faraja kubwa. Naamini mimi moja ni kwa sababu ya uongozi, uongozi uliokuwepo madhubuti, watendaji madhubuti. Sisemi kama wengine sio madhubuti, hapana, lakini hata uingizwaji wake wa fedha basi ni mzuri na ni afadhali sana. Lakini na utendaji.

Mhe. Spika, Mhe. Mwanaidi Kassim alisema ujenzi wa nyumba za wazee. Mhe. Spika, kama hujafika nenda ukajionee, kwa kweli nyumba zimejengwa vizuri na wazee walioko pale wanakaa vizuri, mimi naipongeza sana wizara.

Mhe. Spika, jambo moja nataka kuiomba wizara ambalo linahusu nyumba ya kulelea watoto Mazizini. Mhe. Spika, nyumba ile mimi nilipokwenda niliridhika sana, kwa sababu mimi naijua nyumba ile na niliwahi kufanya kazi katika *NGO*, *ZAYADESA* ambayo ilisimamia na ilijenga nyumba ile. Kwa kweli *ZAYADESA* iliijenga nyumba ile kwa mapenzi yote. Mimi hawezi kunihadithia mtu kwa sababu nilikuwepo, kwa mapenzi yote ya kuwapenda wale watoto ilijengwa nyumba ile. Mhe. Spika, tunashukuru kwamba mpaka leo imebakia kuwa vile vile, bado inapendeza ndani ya taswira ya macho ya watu, nashukuru sana.

Jengine Mhe. Spika, kuna matatizo ya mambo madogo madogo ambayo mimi naamini kwamba wizara inaweza kuyashughulikia. Tumeona kwamba kwanza kuna upungufu wa wafanyakazi pale, kwa hivyo tunaiomba sana wizara ilisimamie hili kwa sababu yule ambaye yupo ule mzigo aliobebeshwa ni mkubwa.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu walezi wa watoto. Mhe. Spika, tulipokwenda pale tumegundua nafikiri kuna mtoto mmoja mgonjwa ana mahitaji maalumu, lakini uwezo wa walimu au wazee waliokuwepo pale hawana uwezo wa kumlea mtoto kama yule. Kwa hivyo, ningeiomba sana wizara kwa sababu hatujui ni lini watapatikana na wengine, na sio kwamba atakapotokea mtoto ambaye ni mlemavu wa aina yoyote akashindwa kulelewa ndani ya nyumba ile. Kwa hivyo, ningeomba sana wizara ijitayarishe kwa hilo, iwape elimu ya ulezi wale walezi wa pale, elimu ambayo itaweza kuwanufaisha hata wale ambao wana mahitaji maalumu.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, muda.

Mhe. Spika, na mimi ninamalizia, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Ninawaomba na Waheshimiwa Wajumbe wachangie, vile vile waipitishe ripoti hii, tunatarajia sana kupitishwa leo au kesho. Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mgeni Hassan Juma. Waheshimiwa Wajumbe, tujitahidini tuwe tunaokoa muda, wachangiaji ni wengi na tunakusudia baadae tukamilishe ripoti hizi na kuzipitisha rasmi. Tumkaribishe basi Mhe. Farida Amour Mohammed na baadae Mhe. Abdi Mossi Kombo.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi jioni hii kuchangia machache katika hotuba ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, na mimi nataka nianze ndani ya Wizara ya Afya, sina lengo la kurudia rudia Mhe. Spika, lakini jambo ambalo linaathiri katika Wizara zetu hizi mbili tunazozisimamia kamati hii mtihani wake mkubwa Mhe. Spika, ni kuhusu uingizaji wa fedha za bajeti. Kwa hivyo nina imani kama kila atakayesimama hapa katika kuziboresha wizara zetu hizi ataligusia suala hili la fedha.

Mhe. Spika, Wizara hii ya Afya ni Wizara mama kwa sababu kila mmoja anahitaji afya, kila mmoja anahitaji matibabu kuanzia mtu wa ngazi ya chini mpaka wa ngazi za juu, na sio wengi walio na uwezo wa kwenda katika hospitali za nje au hospitali za pesa. Hospitali zetu tunazozitegemea ni hizi hizi za serikali.

Mhe. Spika, nataka nianze katika hospitali ya Muembeladu. Sitaki niseme wenzangu waliokuwa tayari wameshayazungumza, lakini kuna suala pale ambalo tumeliona halipendezi ni eneo la *clinic* ya waathirika, lile eneo la wanaofanyia *clinic* wale waathirika wetu Mhe. Spika, liko wazi sana ni nje kukiwa na mvua, mvua kukiwa na jua, na isitoshe mbali na matatizo yote haya, matatizo haya yanatakiwa yawe siri. Kwa sababu kila mmoja hajijui katika hali hii atafika na mtihani wakati gani, sasa kuwaanika wenzetu pale kila mmoja akajua kama wale wanakuja *clinic* kwa sababu ya tatizo la uathirika haipendezi Mhe. Spika.

Kwa hivyo ninaiomba sana Wizara iwafanyie mpangilio wa aina yoyote juu ya kuwa bajeti ni ndogo uingizwaji wa pesa haupo lakini watumie hekima zao zote watakazozijua wale wenzetu pale angalau wapatiwe eneo la stara, katika

hali ile Mhe. Spika, ni ngumu kiukweli. Kila mmoja akiwaona pale wanaingia wanajua yule fulani yule kaathirika, yule kaathirika haipendezi.

Halafu Mhe. Spika, katika hiyo hiyo hospitali ya Muembeladu tulikuta pale kuna changamoto nyingi; uingizwaji wa fedha ni mdogo lakini hata yale mambo madogo madogo lakini ambayo ni makubwa na ni ya msingi pia yanakosekana. Mhe. Spika, katika vituo vyote vya afya hospitali kama zile zinakuwa na kazi ya kufua zile nguo zilizomo mule ndani ya hospitali, lakini kwa bahati hata sabuni wanayopewa pale kwa mwezi basi haiwatoshi ni kidogo mno. Kwa hivyo ninaiomba Wizara katika hili ilisimamie Mheshimiwa. Suala la usafiri tayari hapa ninaambiwa kama usafiri umepatikana, kwa hivyo sina haja ya kulizungumzia tena.

Nikitoka hapo nije kwenye Kitengo cha Afya kilichopo Kwamtipura. Mhe. Spika, Kitengo cha Macho kilichopo Kwamtipura Jimbo la Mwakilishi makini Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa bahati njema kuna vifaa vingi mno vilivyoko pale lakini tatizo lililokabili eneo lile ni lile eneo la kufungia vile vyombo vilivyopo pale. Kuna mambo mawili sehemu nyengine utakuta vifaa hamna wataalamu hamna lakini cha kufurahisha pale kuna vifaa vingi wataalamu wapo lakini kwa bahati mbaya sana havina eneo la kuhifadhiwa vifaa vile.

Vifaa vya gharama kubwa kwa sababu chombo kimoja kwa maelezo tuliyoyapata pale au kifaa kimoja kina gharama kubwa mno lakini kwa bahati mbaya viko katika maeneo yaliyokuwa si ya kuridhisha, na vyengine havitakiwi vipate muangaza, vyengine vinatakiwa sehemu nyengine ziwe na mapazia meusi ili ule muangaza usiingie lakini pia vinakosekana.

Sasa Mhe. Spika, watu wanatafuta vifaa sisi vifaa tunavyo tunashindwa na pahali za kuvifunga. Ninaiomba Wizara ilitizame hili kwa upeo mkubwa na kama alivyozungumza Mhe. Jussa hapa na suala la dereva kitengo kile cha macho hakina dereva, pale pana daktari kwa sababu wagonjwa wanaofanyiwa *operation* wanafanyiwa Mnazi Mmoja, baada ya masaa wanatakiwa wakawachukue wawalete pale. Sasa yeye pale hata kama ana kazi muhimu namna gani atoke aende akamchukuwe mgonjwa amlete pale sasa ni tatizo, wizara ihangaike kumtafutia dereva katika kitu kile.

Mhe. Spika, nije kwenye hospitali ya wagonjwa wa akili. Hospitali ya wagonjwa wa akili pia bajeti yake hapa imezungumzwa ni milioni mbili inayopatikana wakati wao mahitaji yao ni karibu milioni sita. Kulinganisha na wagonjwa walioko pale wagonjwa wa akili walivyo wengi Mhe. Spika, tuwaangalieni milioni mbili zitawafanyaje. Mtu mwenye akili yake kila

mmoja ana nguvu yake ya kula sikwambii mtu aliyekuwa akili hana mlo mmoja kwa siku.

Mhe. Spika, suala hili ni gumu na tutalalamika kila siku mpaka Wizara ya Fedha itusaidie kuwaongezea vile vitengo muhimu kama chakula, ni lazima kwa sababu Mhe. Spika, hospitali nyengine kama Mnazi Mmoja wakilazwa watu, watu wao wanakwenda pale kuwaangalia na kuwapelekea chakula, lakini pale Kidongochekundu watu wanaona kama ile ni sehemu iliyokuwa haifai hata kwenda binaadamu. Sasa mtu akishamtupa mgonjwa pale hampitii hamuulizi. Sasa kama hawakupata huduma kutoka pale pale ni mtihani Mhe. Spika.

Jengine kuhusu usafi. Mhe. Spika, tulipokwenda pale na Kamati yetu kutizama sisi wenyewe tulioingia dakika moja kila mmoja alirudi pale mwili unamuwasha, hata ule usafi mle ndani ni mtihani. Tunajua waliomo mule ndani ni wagonjwa wanafanya kila aina ya maajabu lakini angalau pawe na utaratibu maalumu wa kupigwa dawa kila baada ya muda kwa sababu mna kunguni wanaweza wakakubeba hata wakakupeleka mjini!

Mhe. Spika, naomba nije katika kitengo cha takwimu cha Mnazi Mmoja. Vile vile kitengo kile nacho kina umuhimu wake kwa sababu nyaraka zote za mafaili ya wagonjwa ziko pale, lakini kutafuta hilo faili la mgonjwa pale pana kazi kubwa kwa sababu hayapangiki, tumekwenda mengine yamechawanyika chini hayana nafasi ya kukaa, mchana kuna kiza sikwambii usiku, na zile taa zilizoko haziwezi kuona ule mwangaza wake tukayaona yale mafaili pale yalipo. Kwa hivyo Mhe. Spika, nalo hili pia tuangalie sana wizara litafute eneo jengine la kuhifadhi mambo yale kwa sababu mgonjwa anapotokezea pale kutaka waraka wake ukawa haupo inakuwa ni tatizo Mheshimiwa.

Halafu pia mbali ya kuwatafutia eneo kitengo kile cha takwimu pia na wale wanaofanya kazi pale na wao ukiingia ile dakika moja tu basi *flue* tayari, macho yataanza kuwasha kwa sababu ya lile vumbi ya kuwa yale mabuku mengi pale na hayana pahala maalumu pa kuhifadhiwa vizuri.

Mhe. Spika, nitoke kwenye Wizara ya Afya nije kwenye Wizara ya Uwezeshaji. Wizara ya Uwezeshaji naomba nitoe pongezi za dhati kabisa kwa utendaji wao mzuri wanajitahidi sana katika kufanya shughuli zao. Na pia sitakuwa mwizi wa fadhila naomba niipongeze sana Wizara ya Fedha kupitia Katibu wao Mkuu kwa kukubali kukutana na kamati kwa kutafuta suluhisho la wale watu wanaodai fidia, tatizo ambalo lilikuwa la muda mrefu sana. Fidia ya wafanyakazi wanaoumia katika mazingira ya kazi, lakini kwa bahati njema Wizara ya Fedha imekubali kukaa pamoja na kamati, pamoja na Wizara ya

Uwezeshaji Wananchi na imelikubali hili na imetoa ahadi kama itamaliza tatizo hili kwa muda mfupi.

Mhe. Spika, naomba nije katika Wizara hii ya Uwezeshaji katika Idara ya Ushirika. Idara ya Ushirika ni hakika wamepatiwa jengo lile liliopo Migombani. Lile jengo ni kubwa na ni zuri lakini linahitaji gharama kubwa mno mpaka kufika kukaliwa lile jengo, hasa katika miundombinu ya maji. Mhe. Spika, lile jengo linatakiwa lifanyiwe ukarabati wa hali ya juu kwa sababu zile *pipe* baadhi yake zimeng'olewa kwa sababu jengo lilikuwa halikaliwi kwa muda mrefu.

Jengine katika hapa naomba niwambie tu watu wa Idara ya Ushirika watoe elimu zaidi kwa sababu watu wengine hawana elimu juu ya dhana nzima ya ushirika. Hawajui nini maana ya ushirika, hawajui chochote kile, na hasa kuna upande wa usajili kwa hivi vyama vya ushirika unaleta matatizo na usumbufu mkubwa kiasi fulani hasa katika kisiwa chetu cha Pemba. Kwa hivyo ninaiomba Wizara kupitia Idara hii ya Ushirika walishughulikie sana suala hili watu wetu vijana wengine waliokuwa tayari wameshakuwa na muamko wa kuunda vikundi vyao, wanapata tabu kwa suala la usajili. Kwa hivyo naomba sana suala hili walifuatilie na walichukulie hatua za haraka ili azma ile ya serikali ya kuwasaidia vijana wetu kuwawezesha kiuchumi lifanikiwe.

Mhe. Spika, katika eneo hili hili la uwezeshaji niko katika Idara ya Mikopo naomba waendelee na kutoa elimu zaidi kwa sababu kuna baadhi ya watu wanaokwenda pale kwa ajili ya kuchukua mikopo, vichwa vyao vinavyowaelekeza ni kuwa pesa ya serikali hata ukikopa hailipwi. Lengo la pesa ile ni kuwawezesha wao halafu warejeshe na wengine wapate kuchukua. Kwa hivyo ninaiomba sana Wizara kupitia Idara hii wasichoke kutoa elimu katika vyombo tofauti ili mtu akope atumie kisha arejeshe, anaweza akakopa tena yeye mwenyewe na wengine wapate nguvu ya kukopa.

Mhe. Spika, kwa hayo machache, kwa niaba ya wanawake wa Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba ninaunga mkono asilimia mia moja.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na mimi naomba kwanza nimpongeze Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Uwezeshaji kwa kusimamia kazi nzuri mpaka tumemaliza kazi yetu na mpaka tumeleta ripoti yetu, na niwapongeze makatibu na nimpongeze Mhe. Mohammed Mbwana kwa kuwasilisha vizuri sana ripoti yetu, na kama ingekuwa mimi natoa nishani kama wale maaskari leo ningempa cheo cha ukanali.

Mhe. Spika, nikianza mchango wangu kwanza ninakwenda katika hospitali ya Mnazi Mmoja, kitengo kile cha kinamama waliokuwa wameathirika na VVU.

Mhe. Spika, kitengo hiki ni muhimu sana lakini kuna ukosefu wa kifaa kinachoitwa DNA, kifaa hiki na kinachanganya kifaa cha PCR ambavyo vifaa hivi huwa vinapima damu za wale akinamama walioathirika na ukimwi wakati wanapojifungua. Lakini ukosefu wa kifaa hiki inabidi damu ipelekwe Dar es Salaam Muhimbili. Sasa kwa bahati kule damu inakawia ikikaa kule miezi mingi, hata ikifika hapa inakuwa inachelewa na inakuwa athari sana kwa wazazi ambao waliokuwa wameathirika. Kwa hivyo ijapokuwa kifaa hiki ni ghali lakini ninaiomba Wizara ijitahidi na serikali iweke fedha kipatikane kifaa hiki ili waokolewe akinamama wetu ambao ni wazazi.

Mhe. Spika, na mimi nitatilia mkazo hospitali ya macho ya Kwamtipura. Kama walivyozungumza Wajumbe wenzangu kwamba hospitali ile ina tatizo kubwa la dereva, dereva inabidi afanye kazi daktari wa macho, akipata mgonjwa amchukue ampeleke hospitali ya Mnazi Mmoja. Mhe. Spika, ninamuomba Mhe. Waziri alitizame sana jambo hii kuhusu hospitali ya Kwamtipura ina tatizo la dereva. Daktari ndio afanye kazi ya udereva, daktari afanye kazi ya macho, hii itakuwa ni usumbufu sana. Kwa hivyo Mhe. Waziri alifikirie sana jambo hili katika hospitali ya Kwamtipura ya ugonjwa wa macho.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia wakati ninakwenda katika Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, Wizara hii imechukua kinamama wengi sana na kinamama wetu wa hivi sasa wengi ni wajasiriamali. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri ahakikishe kinamama hivi sasa anawawezesha na ile benki ya akinamama inayotarajiwa kufunguliwa ili wapate mikopo kinamama. Ninamuomba Mhe. Waziri aiharakishe ili kinamama na watoto wasipate tabu. Kwa sababu nchi yetu sasa hivi naona asilimia kubwa ya kinamama ndio wafanyabiashara, kwa hivyo kinamama lazima wawezeshwe kwa hali ya juu.

Mhe. Spika, ili wapate wenzangu nao wachangie naishia hapa. Ahsante.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii kuchangia machache katika ripoti hii ya Ustawi wa jamii. Nianze kwa kuipongeza kamati; nimpongeze msomaji wa ripoti kwa niaba ya Mwenyekiti kaka yangu Mhe. Mohammed Mbwana Hamad kwa kuisoma ile kwa ufasaha.

Mhe. Spika, kamati hii ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ina jukumu la kufuatilia Wizara tatu kama nilivyoeleza na Wizara zote hizi ni muhimu sana. Wizara hizi tatu; Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na

Wizara ya Uwezeshaji Ustawi wa Jamii Vijana Wanawake na Watoto na zote Wizara hizi zina majukumu mazito.

Mhe. Spika, nikianza na ukurasa namba 66 ya ripoti hii niende kwenye kitengo cha kupambana na maradhi yasiyopewa kipaumbele. Hivi kwanza niulize kuna maradhi ambayo hayana kipaumbele. Kwa sababu ninaamini mimi kwamba maradhi ni maradhi, unaweza ukasema maradhi hukuyapa kipaumbele basi pengine yakawa ndio sababu ya kuja kukufanya wewe ukaaga dunia kwa yale maradhi ambayo hayakupewa kipaumbele. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri anambie kwamba kuna maradhi ambayo hayakupewa kipaumbele haya ni maradhi gani?

Mhe. Spika, nikienda ukurasa wa 66 wa ripoti hii kuna kitengo cha huduma za matibabu ya macho. Na nikitizama kuna namba 3 hapa katika changamoto anasema kukosekana kwa gari ya wagonjwa na dereva. Kamati ilibaini gari inayotumika kusafirishia wagonjwa kutoka hospitali ya macho iliyopo Kwamtipura mpaka hospitali ya Mnazi Mmoja ni gari ya mradi, na kutokana na kukosekana dereva wa gari hiyo, daktari anayetibu wagonjwa wa macho analazimika pia kuwa dereva wa gari hiyo. Mhe. Spika, kwa kweli kuna vijana wetu huko wengi tu ambao wanahitaji ajira lakini bado tunapata changamoto kama hizi kwa kweli tujitahidi kama serikali kuwapa watoto wetu hawa ajira.

Mhe. Spika, nikienda kwenye hospitali ya Mnazi Mmoja wenzangu wameshasema na sina haja ya kuyasema tena lakini kuna mambo muhimu Mhe. Spika.

Karibuni hivi nilikuwepo pale hospitali baada ya kulazwa na mtoto wangu lakini inasikitisha sana hospitali pale kusema kweli, mimi ninashukuru sijui kama ni madaktari au ni wauguzi na nilipata msaada mkubwa kutoka kwa Dr. Sira hapa kila mara lakini kwa kweli inanitisha. Na waswahili tunasema mtu akiumwa na nyoka basi akiona ung'ong'o anakimbia, kwa kweli inasikitisha sana sana.

Nimekwenda na mgonjwa wangu pale baada ya kuwa mimi nilazwe hospitali niseme wala sitaki kumkufuru Mwenyezi Mungu, lakini ninafikiria baada ya kufika hospitali basi nipate matibabu na nione ule uendelevu wa yule mgonjwa, lakini kadiri nilivyofika pale kila siku zilivyokuwa zinaendelea baada ya kuwa mgonjwa kapanda kwa miguu yake lakini mwisho wa siku kashuka pale kwa vitanga vya mkono kwa kweli hii inasikitisha. Na haya yote nasema mimi ninamwachia mwenyewe *Allah Subhana Wataala*, lakini kusema kweli baada ya kutiwa damu pale ndio ilikuwa ndio mauti, ile damu ilikuwa ni matatizo, kwamba hakuwa nayo mwilini mwake, lakini baada ya

kutiwa ile damu kumbe ile damu ilikuwa ndio tatizo ya kutoka kwa roho ya binaadamu.

Kwa kweli baada ya kupata ile damu tu akaanza kupata mshtuko ule na baadae kuja kupigwa sindano ya kwanza, ya pili, ya tatu, nikaambiwa ni *valium* lakini kutoka Alkhamis aliyopigwa mpaka ninafikiri kenda kufumbua macho akhera. Kwa kweli hii inanitisha mimi hata tena kwenda na mgonjwa katika hospitali ya Mnazi Mmoja.

Kwanza vifaa, ni bora basi twende hospitali zile za binafsi moja kwa moja kwa sababu kila unachokitaka pale unaambiwa wewe nenda Al Rahma, nenda wapi ukatafute vipimo kweli? Hii ni hospitali ambayo sisi tunasema itakuwa ni hospitali ya rufaa. Kwa kweli Mhe. Spika, inasikitisha sana na kwa kweli tutaogopa hata kwenda hospitali, na wala sisemi tena kwamba nimpeleke mgonjwa wangu leo pale niambiwe atiwe damu. Kwa sababu mimi mwenyewe ile damu nilikuwa ninaiogopa vile namna inavyodondoka inatoka kama urimbo, mimi nasema ile damu pia ilikuwa ni tatizo.

Mhe. Spika, hayo katika Wizara ya Afya kwa kweli bado tujitahidi sana, kuna wananchi wengine hawana pa kwenda, hospitali tunayoitegemea ni hospitali ya Mnazi Mmoja, hakuna kwengine katu. Kwa hivyo tujitahidi sana sana, na hasa ninaogopa kusikia madaktari wengi wamekwenda kusoma na waliokuwepo pale wengi ni wanafunzi. Kwa hivyo suala hili kwa kweli mimi linanishtusha sana.

Mhe. Spika, nikienda kwenye Idara hii ya U stawi wa Jamii kuna changamoto inazozikabili kamati za Shehia zinazoshughulikia masuala ya kuzuia vitendo vya udhalilishaji. Hivyo Mhe. Spika, kama kuna changamoto hizi kwa kweli tunategemea nini katika Wizara yetu hii ya Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto ambao tunasema watoto ndio viongozi wa baadae, kama hata hapa kunakosekana na ushahidi wa kesi zinazoripotiwa na Polisi, kweli tuko *serious* na hili jambo kweli? Mheshimiwa kwa kweli changamoto hizi ni nyingi.

Nikiendelea kwenye ukurasa 77 unasema kwamba kuwepo changamoto kwenye Idara hii ya Ustawi wa Jamii kwa deni la fidia kwa wafanyakazi 71 walioumia kazini lenye thamani ya shilingi milioni 92,844,586 kwa Unguja na Pemba. Unguja shilingi 32,560,064 na Pemba shilingi 60,284,522. Nimuulize Mheshimiwa hizi pesa hizi ambazo ni fidia ya wafanyakazi walioumia lini zitalipwa? Hapa siku zote tunasema changamoto, changamoto ni ufinyu wa bajeti, hebu serikali iwe *serious* na kuzitafuta hizi pesa, kuna pesa nyingi sisi tunaweza tukazikusanya kupitia ardhi tu na wala sina haja ya

kuyasema. Hivyo hizi pesa tunapokaa tukapanga bajeti na halafu kukawa na fedha ambazo haziingii kama zinavyotakiwa au kama zinavyoombwa.

Tunajua tu kuna *ceiling* ya hizi pesa lakini *still* kunakuwa na ufinyu wa bajeti na kuna Wizara mimi nimeshapita katika kamati yangu PAC au kuna maeneo wanapata *hundred percent* (100%) ya bajeti lakini bado unakuta kwamba wizara nyengine au hivi vipaumembele tunasema vipaumbele, kwa nini hivi vipaumbele basi tusiweke mbele zaidi kwenye haya maeneo? Mhe. Spika, kwa kweli haya ni matatizo.

Nikienda kwenye Idara ya Ushirika changamoto zinazoikabili Idara ya Ushirika iko hapa, kamati iligundua kuwa Idara Ushirika inakabiliwa na tatizo la uhaba wa wafanyakazi wenye taaluma hasa kwenye fani ya ukaguzi. Hivyo kweli tunataka tufanikiwe kweli kwenye Idara hii ya Ushirika kumbe hata pale Idarani kwenyewe kuna mapungufu, kweli tutawasomesha nini wananchi wetu, na kama tunataka tuwafahamishe kweli na nimeona kuna sehemu hapa sijui kama ni Wizara ya Afya ile hata zile nafasi za kawaida zilizokuwa si za usomi za usafishaji tu basi wafanyakazi hamna. Kwa kweli Mhe. Spika, hili ni tatizo.

Nikienda na Wizara ya Elimu niwashukuru sana lakini kuna matatizo vile vile, lakini haya si ya Wizara kama hili la utoro wa wanafunzi. Kamati imebaini kuwa tatizo la utoro bado ni changamoto kubwa katika skuli zetu za Unguja na Pemba. Hili ninafikiri ni sisi wenyewe wazazi ni kwamba hatuna mashirikiano, hatuna ule utaratibu wa kuwakagua watoto wetu namna gani wanakwenda skuli, tunawaachia tu halafu tunakuja kulaumu serikali na kuwalaumu walimu.

Vile vile kuna majengo haya ya skuli ambazo zimejengwa mimi ndio kwanza nimeipata hapa kwamba skuli ile iliyokuwa kwenye eneo la Kwamtipura, lakini nilivyosikia huko nyuma ilikuwa katika eneo langu katika shehia ya Kilimahewa kule na sasa hivi ndio nimesikia kwamba inaitwa Faraja. Basi faraja iwe faraja ya kweli tufarijike sote.

Haya maeneo kwa kusema kweli hizi skuli zijengewe uzio kwa sababu maeneo yenyewe tunayajua ni ya hatari, kwa sababu wanaingia tu watu yapo ndani ya makaazi ya watu, watu wanachimba mchanga. Kwa hivyo ningeomba kwamba Wizara ya Elimu ilishughulikie suala hili ijenge uzio. Ile Skuli ni nzuri na imejengwa juzi tu skuli hiyo ya Faraja na ya Mpendae, kwa hivyo ningeomba Wizara ya Elimu basi iyashughulikie majengo haya kwa kuyatilia uzio.

Baada ya hayo Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa hii na kwa niaba ya wananchi wangu wa Amani naunga mkono.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kuna wachangiaji wanane waliobaki na nategemea kwa muda tulionao tunaweza kumudu kupata wachangiaji wanne, ambao ni Mhe. Hamad Masoud Hamad, Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Abdalla Mohammed Ali na mwisho kwa sababu amezungumzwa sana Mhe. Waziri wa Fedha. Basi naomba sasa nimkaribishe haraka haraka Mhe. Hamad Masoud Hamad baadae Mhe. Salim Abdalla Hamad.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo kuwa miongoni mwa wachangiaji wa taarifa hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, ambayo inajumuisha wizara tatu. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, kwanza niende kwenye elimu. Mwaka juzi nilikuwa nachangia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika hotuba ya bajeti, nikasema kwamba hivyo sisi Zanzibar tuna kitu gani ambacho hatujakijua hadi tukafikia hali hii. Nilitoa mifano kwamba kulikuwa na matokeo ya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita. Nikasema kwamba Zanzibar ina Wizara ya Elimu kuna waziri, naibu waziri, kulikuwa na makamishna, wakurugenzi wanakaribia kama 15 wizara moja hiyo, lakini matokeo ya uchaguzi...

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, lakini matokeo ya mtihani wa Kidato cha Nne na cha Sita kwa wakati huo…

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mnajua humu tulimo kwamba kuna uchaguzi keshokutwa, ndio maana kateleza hivyo. Mheshimiwa endelea. *(Vicheko)*

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mheshimiwa keshokutwa tuna uchaguzi sio uongo, na *Inshaallah* tarehe tatu utamuapisha Mwakilishi wa *CUF* katika Baraza hili.*(Makofi)*

Mhe. Spika, niendelee, nilisema kwamba Zanzibar nzima ilikuwa na *first division* ya *Form VI*, wanafunzi ambao hawazidi 10, hiyo ni wizara nzima, serikali nzima, nchi nzima. Wizara ambayo ilikuwa na waziri, naibu waziri, makamishna, katibu mkuu, manaibu katibu wakuu kama 15 hivi ukiwajumlisha. Lakini nikasema kwamba kuna skuli ya serikali Kibaha ilikuwa na *first division* 56, nikataja baadhi ya skuli nyengine zina *first division* 40, 25, sisi nchi nzima, serikali nzima, wizara nzima tulikuwa na *first division* hazizidi 10, tatizo ni nini? Tukajibiwa hivi hivi tu.

Mhe. Spika, katika elimu bado tuna tatizo. Mimi nafikiri bado serikali haijafanya elimu na afya kuwa ni kipaumbele. Katika hili ningeshauri sana tena sana kabisa, kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwanza katika kutekeleza sera ya kupunguza umasikini maana umasikini hauondoki kiyama kitafika hapa, hauondoki hata Marekani umasikini upo. Lakini angalau kuupunguza kwa kiasi kikubwa, basi iondoe mzigo kwa Wazanzibari wanyonge, mizigo miwili hii waiondoe, wa kwanza ni elimu.

Mhe. Spika, Mapinduzi ya mwaka 1964 yaliweka elimu bure na kweli ilikuwa ni elimu bure. Kwa sababu kipindi kile na mpaka hivi karibuni miaka 15 nyuma, ilikuwa mwanafunzi akipasi ile familia ilikuwa na sherehe, furaha, mtoto wao kapasi anakwenda *Fidel-Castro*. Anakwenda Tumekuja, Ben-Bella au Lumumba. Leo mtoto akipasi ni msiba, huzuni, vilio, ni harusi isiyokuwa na kitu! Mtoto huyo achukue ndoo, apate godoro au mkeka. Sasa angalia masikini ya Mungu, aliyekuwa na watoto wawili au watatu! Kipato cha Mzanzibari kinajulikana. Katika jambo ambalo sasa hivi ni mzigo kwa Wazanzibari basi ni elimu. Mimi mtu akinambia elimu ni bure namtizama mara tatu usoni.

Juzi nilikuwa jimboni kwangu kule, wamenijia wanafunzi na wazee wao wanataka kutoka darasa moja kuingia jengine. Wengine shilingi 7,000, mwengine 10,000, 5,000 na kama huna walimu wanakwambia kabisa uso tusiuone. Kwa hivyo, mwakilishi gani atakayekuwa na fedha za kuwatolea wanafunzi wengi katika jimbo wa namna hiyo. Kwa sababu ukishakuwa mzee una watoto wanne au watano walipe shilingi elfu tano tano tu ni 25,000; ziko wapi?

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali hapa hayupo lakini kaimu wake yupo, watoto wale hawaendi skuli kwa sababu hawana shilingi 5,000 au 7,000 za kutoka darasa moja kuingia jengine. Mtoto anakuwa haendi skuli, *child labour* inamchukua anakwenda kufanya matofali huyo ndio hasomi tena.

Kwa hivyo, shughuli hii Waheshimiwa ya kutoza pesa mimi sikatai kuchangia lakini uwezo uko wapi wa kuchangia. Nilikuwa nafanya mahesabu hapa mimi nina hakika kama serikali itakuwa na kipaumbele cha elimu *twelve billion shillings* zinatosha kwa wanafunzi wasinunue mabuku, wasitoe *fees*, wasinunue kiti, wasitoe michango ya kujenga skuli. Tumuache mzee na sare za watoto tu, fedha atakazopata ashughulikie mambo mengine madogo madogo. Hilo ni moja.

Kwenye afya vile vile ni mzigo wa pili Mhe. Spika. Utamkuta mtu ana mgonjwa wake hospitali, mtu anatoka Nungwi hata chakula kile cha hospitali ubebe kutoka Nungwi. Huku ana chupa ya maji ya moto, huku ya uji, huku

ana koba la kisamvu, Mheshimiwa aibu, kwani tuna wagonjwa wangapi kiasi ambacho hatuwezi kuwalisha.

Zamani ilikuwa marufuku mtu kupeleka chakula hospitali kwa sababu kulikuwa na chakula cha wagonjwa. Leo mgonjwa anaandikiwa mchicha, maharage yote hayapatikani, anapelekewa pande la muhogo ndilo alilonalo mtu, nani atapona maradhi hayo.

Kwa hivyo, mimi naishauri serikali, bajeti inayokuja tukubaliane hapa jamani kipaumbele iwe kwenye elimu na kwenye afya, ili Mzanzibari hii mizigo miwili asaidiwe. Watu washughulikie mambo mengine.

Mhe. Spika, nchi yoyote bila ya elimu hiyo haiwezi kuendelea na elimu kwetu sisi ni ngumu haiendelei kwa sababu gani? Amesema hapa Mhe. Mgeni Hassan Juma, darasa lina wanafunzi 200 kwa hivyo mwalimu hapo hatoi *home work* wala *class work.* Kwa sababu *home work* na *class work* mwalimu lazima apate daftari aangalie la mwanafunzi. Hesabu alizotoa hakuna kusahihisha Mhe. Spika. Mwalimu anayejitahidi kusahihisha wanabadilishana wanafunzi mabuku, huyu anachukua la huyu na huyu anachukua la huyu anasema huyo, 'hesabu nambari tatu, saba na saba ni kumi na nne' aliyepata anamtilia mwenzake, hakuna jengine, yaani ni ucheza, ucheza, ucheza!

Mimi nashauri sana bila ya elimu hakuna nchi inayoweza kuendelea. Bbila ya wananchi wenye afya hilo taifa ni *acting*. Kwa hivyo nashauri kabisa kabisa Mheshimiwa mimi sina mchango mkubwa katika hili. Lakini nashauri katika vipaumbele vya serikali basi elimu na afya tuweke nambari moja bajeti zake, tuhakikishe kwamba wanafunzi wanasoma.

Mhe. Spika, juzi nilikuwa na walimu walinifuata wana madai ya *areas*, walimu wa Skuli ya Kiponda, Skuli ya Darajani na Skuli ya Kisiwandui. Hawa ni walimu ambao wamesoma, wamepata vyeti vyao wanatakiwa walipwe tofauti ya mishahara ya sasa na hiyo ishathibitishwa, huu ni mwezi wa tisa. Sasa mwalimu gani atakuwa na *interest*?

Kuna skuli Mhe. Spika, maana wakati mwengine Wizara ya Elimu mimi inanishangaza hasa hivyo vigezo vyao ni vipi. Kule Skuli ya Kangagani naitaja *specific,* ile ni skuli ina mpaka *Form IV*. Kuna walimu pale wenye uzoefu wana *first degree* ya *education,* wana wanafunzi wao wanasomesha nao pamoja, basi Mwalimu Mkuu ilichukua karibu miezi mitatu watu wanabishana awe nani. Amewekwa Mwalimu Mkuu ambaye ni mwanafunzi wa wale walimu.Walimu wenye *experience*, wana digirii ya kwanza hawana sifa ya kuwa mwalimu mkuu. Amewekwa pale jamaa ambae ana *Form IV,* ni mambo ya kuchekesha.

Hivyo kweli skuli hiyo itakwenda? Ni mwalimu gani atakayekuwa na *interest* ya kumuona mwanafunzi wake ambae ana elimu ndogo kuliko yeye anakuwa ni bosi wake, ni ngumu na huo ndio mfumo. Kwa hivyo, kwanza hili nalizungumza ili lifuatiliwe tuone.

Mhe. Spika, na mabadiliko yasifanywe pale tu, Mjini Kiuyu kuna madarasa saba walimu watano, hebu nambieni, kuna madarasa mawili saa zote hayo hayasomi. Unaangalia *attendance* anasema sisi tulikwenda jana hatukusoma, darasa hilo utakuta siku ya pili lina wanafunzi saba katika wanafunzi 50, waliobaki wote wamekwendazao pwani, hawasomi. Kwa hivyo, baadhi ya wakati ni upotezaji wa muda tu. Mimi nasema Wizara ya Elimu inahitaji *measure overhaul*, sio kutia girisi na kupaka rangi.

Mhe. Spika, Bodi ya Mikopo. Kuna malalamiko Bodi ya Mikopo, kuna upendeleo na ubaguzi mkubwa, inasemekana hivyo. Kwa sababu wanaopewa mikopo na wale ambao wanakosa walio na sifa wengi ndio ambao wamekoseshwa mikopo kuliko ambao wamepewa.

Sasa hili kamati sijui kama waliliona, mimi nafikiri kuna haja hasa ya kuwekwa wazi hili kuletewa orodha hapa. Shilingi 18 bilioni zimetumikaje, nani kapata na nani hakupata kakoseshwa. Vyenginevyo Mheshimiwa, kila siku watu watakuwa na manung'uniko. Bodi ya Mikopo hii imewekwa ili kurahisisha mambo haya lakini badala yake inakuwa magumu zaidi.

La mwisho kabisa Mhe. Spika, huduma za afya. Huduma za afya zinasikitisha na yote si kwamba watu hawana uwezo wa kufanya kazi, lakini bajeti. Mishahara asilimia mia moja, *other charges* asilimia 33, *development* asilimia 2, maana yake hapo ni kwamba hapafanywi kazi watu wanalipwa tu.

Sasa pesa zenyewe hazipo, kazi haifanywi, mtu unamlipa, jamani hii ni serikali. Haya ni mambo hata mtoto mdogo anayaona, achiliambali mtu mkubwa, ni aibu na kesho itakuwa kashfa hii. Mimi naona aibu.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, kama ulivyosema muda ni mdogo lakini nasisitiza serikali iwe na vipaumbele. Elimu na afya iwe *number one*. Tuwatue Wazanzibari mizigo hii miwili twika ya maisha tuwaache wafanye shughuli nyengine za maisha. Lakini afya iwe kama ni bure basi iwe bure kweli, elimu kama ni bure iwe bure kweli isiwe ni bure jina lakini ni ghali kuliko ile bure.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kupata nafasi hii na nashukuru zaidi kwa sababu nina dakika kumi na *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nitazitumia hizo hizo kumi.

Mhe. Spika, kwa kuanza nitoe shukurani za dhati kabisa kwa Kamati hii ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa ripoti nzuri waliyoitoa inayohusiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto na Wizara ya Afya.

Vile vile nitoe pongezi kwa msomaji nae kajitahidi sana kusoma kwa namna ya ualimu anavyoujua yeye kaisoma na kuifahamu bila ya kuiangalia hiyo karatasi yenyewe. Mwisho natoa shukurani kwa wenzangu waliochangia.

Mhe. Spika, kwa sababu ya wakati nianze moja kwa moja na Wizara ya Afya. Wizara hii nitaanza na Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwanza kabla sijaanza nimpongeze Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuwa ni Mwakilishi wa aina yake kwa kufuatilia hospitali hii kwa huruma sana, ili kuona kuwa wagonjwa wanapata huduma ipasavyo.

Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja imeelezewa kuwa ina changamoto nyingi, lakini mimi nazungumza tatu tu kutokana na wakati. Kwanza Mheshimiwa kuna kukosekana kwa kifaa hiki kinachoitwa *DNAPCR*, ambacho ni kifaa kinatumika kwa kupimia damu ya watoto waliozaliwa na mama ambao tayari walikwishaambukizwa na virusi vya UKIMWI.

Mhe. Spika, watoto hawa wanahitaji uangalizi wa aina yake kutokana na mazingira yao yaliyojitokeza, lakini kwa bahati mbaya ili kuweza kujua mtoto huyu yukoje wakati wa kupimwa hii damu yake na kwa kukosekana kwa kifaa hiki ni jambo la kusikitisha sana. Inasikitisha zaidi kwa kuwa hata huko Muhimbili kunakopelekwa hiyo damu inapohitajika matokeo huchelewa, na naamini matokeo yanapochelewa kutolewa kuna athari zitajitokeza kutokana na matokeo hayo. Namshauri Mhe. Waziri wa Fedha atoe uzito mkubwa kwa suala hili, aone kuwa katika hospitali yetu hii ambayo tunaiita ya rufaa kifaa hiki cha *DNAPCR* kinapatikana kwa maslahi ya watoto wetu waliozaliwa katika mazingira hayo.

Mhe. Spika, la pili katika hospitali hii, tunajua popote panapokuwa na kituo cha afya na hospitali na kadhalika na mambo mengine yanayohusiana na hayo kunakuwa na taka taka za aina yake, na ndio ikawa ni lazima katika sehemu kama hizi kuweko na matanuri ya kuchomea taka taka hizo. Lakini kutokana na ripoti kwa kukosekana tanuri hili hiziz taka taka zinachomwa pembeni kwa hospitali kwenye ufukwe wa bahari.

Mhe. Spika, hata Hospitali ya Mwembeladu nayo vile vile, kumbe haina tanuri hili na riipoti imeeleza kuwa wakati mwengine zinaleta harufu mbaya na zinachukuliwa zinachanganyishwa huko Mnazi Mmoja. Mimi nahisi uchomaji huu wa taka hizi katika sehemu iliyo na hewa ni hatari kubwa sana. Kunaweza kukatokea *air pollution*, *land pollution*, *water pollution* ikiwa maji ya bahari yanafika pale kutokana na aina ya taka zile zilivyo. Namuomba Mhe. Waziri anifahamishe kwa kukosekana kwa tanuri hili na kusababisha taka taka zichomwe huko je, hakuna athari yoyote kwa viumbe?

Jengine Mhe. Spika, katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kuna kitengo maalum kinachojadili wagonjwa ambao maradhi yao ni makubwa na hayatibiki na huhitajika kupelekwa nje ya nchi kwa matibabu zaidi, sana hapa wagonjjwa wetu tunapeleka India.

Wagonjwa wanaojitokeza ni wengi lakini kwa bahati mbaya na naamini ni kwa sababu ya ukosefu wa fedha, ni wagonjwa wachache wanaopata nafasi ile ya kwenda kutibiwa. Kuna wengine hawapati na mpaka daktari akizungumza kuwa huyu asafirishwe maana yake ni kuwa asafirishwe, kwa bahati mbaya wanapoteza maisha yao bure.

Naomba kwa vile ile ni hospitali ya rufaa suala la maradhi likiwa ni la kwenda nje ya nchi tuone kuwa wakati bodi imeamua huyu asafirishwe basi asafirishwe. Kwa sababu hakuna kitu muhimu kama kulinda maisha ya binadamu.

Halafu katika Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Mhe. Spika, hii inasikitisha sana. Mheshimiwa Mgonjwa wa akili kwa miezi minane hii anapata mlo wa mara moja tu. Hospitali ilikuwa katika makisio yake inahitaji shilingi milioni sita zimepatikana mbili tu. Hawa ni wagonjwa wa akili na kwa sababu fedha haikupatikana ndio tena na wagonjwa wanakaa na njaa. Namuomba Mhe. Waziri tena Waziri wa Fedha aone kuwa wagonjwa hawa ni wakuhudumiwa, kwa hivyo yale maombi yanayotoka kwenye wizara kwa ajili ya wagonjwa hawa yapewe kipaumbele. Jamani kuumwa ni jambo zito sana na mtu kufa hivi hivi na njaa ni hatari.

Halafu katika hospitali hii vile vile inasikitisha sana kuona kuwa kumbe hii hospitali ina upungufu wa wafanyakazi wengi, katika ngazi ya madaktari, ngazi ya wauguzi, ngazi ya walinzi, wasafishaji na wengineo na hivyo waliopo wanafanya kazi ya ziada ili kufidia wasiokuepo. Ningeliomba idara inayohusika na uajiri ikiwa wale vijana wetu wanaosoma kule Mbweni wana utaalamu wa kuendesha shughuli hizi, basi haja ya dharura ifanywe ili waajiriwe waweze kuzifanya kazi zao ilivyo kwa maslahi ya wagonjwa wetu wa akili.

Wagonjwa wa akili hawa nawasikitikia zaidi kuwa katika hiki kitabu wameelezwa wanakosa hata dawa muhimu. Humu imeandikwa kuna upungufu wa dawa muhimu. Suala hili hupelekewa wagonjwa hawa kukosa kuendeleza *dose* zao kama inavyohitajika.

Mhe. Spika, huyu ni mgonjwa wa akili, daktari katoa dawa hizi apewe zimsaidie na ikiwa hazipatikani ni hatari. Nikisema tunawauwa kwa makusudi wagonjwa wetu nafikiri sitakosea sana. Kwa hivyo, tuone kuwa na hizi dawa kwa gharama zozote zile, lakini zinapatikana kwa maslahi ya wagonjwa wetu.

Mhe. Spika, kwa ufupi sana naomba kuzungumza machache kuhusu Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Mhe. Spika, hii ni wizara inayohusiana na utoaji wa fidia kwa wale wafanyakazi wanaopata ajali kazini na wako wengi sana. Mhe. Spika, kama tulivyoona katika ripoti kwa Unguja tu katika bajeti ya mwaka 2012/2013 waliomba shilingi za kitanzania 50 milioni na wakapewa shilingi milioni mbili tu.

Pemba huko hakuna chochote kilichotolewa na sijui waliomba ngapi. Hii inasikitisha kwa sababu wako wengi na Mheshimiwa mimi najua Pemba kuna wagonjwa wa tangu mwaka 2008, hawajaulizwa chochote. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha ahadi yake ya kuipatia wizara hii jumla ya shilingi 92,844,586 kama ndio fedha inayohitajika kwa kulipwa watu wote fidia hiyo kwa mwezi wa Machi, 2014 zipatikane ili kero hii iondoke.

Mwisho Mhe. Spika, naomba dakika moja tu kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Wizara hii Mheshimiwa ndio taasisi tunayoitegemea kwa maendeleo ya nchi yetu. Ripoti imeeleza mengi kuhusu wizara hii. Upungufu wa walimu hasa wa sayansi, vikalio, meza na kadhalika. Kutokana na kuwa ripoti imeeleza hali ya masomo imeshuka na kutokana na hali hii mimi nilikuwa nizungumze sana, lakini kwa sababu ya wakati basi naishauri sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Spika, ikae kitako na iangalie hii fomula inayotumia kuona kuwa kwa nini maendeleo hayapatikani vilivyo.

Hii ni hatari. Sasa hivi ukiangalia watoto wetu wengi tu wanasoma lakini masomo wanayofaulu kuendelea mbele ni masomo ya *art*, ambayo wizara yenyewe haikuweka kipaumbele kwa kuwapa mikopo na wao hawana kosa. Kosa ni wizara yenyewe kwa kutokuwa na walimu wa sayansi ili na wao wakaingia katika sehemu hiyo.

Kwa hivyo, ni wajibu wa wizara sasa kukaa kitako na kufanya utafiti, kwa vile wanacho kitengo hiki kuona kuwa ifanye vipi ili hali ikae sawa. Mhe. Spika, nashukuru.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nataka niseme machache ili nikuokolee muda. Mhe. Spika, mimi kidogo nataka niingie katika Wizara ya Afya. Hapa kuna agizo nambari tano na agizo hili limetolewa ufafanuzi kwamba kutakuwa na utanuzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee iliyopo Mkoani kisiwani Pemba. Huu ni uamuzi wa busara na wa kupigiwa mfano, kwamba serikali imeona ipo haja sasa ya kuweka hospitali ya kisasa katika Wilaya ile ya Mkoani ambayo itasaidia wagojwa kutoka sehemu zote za kisiwa hiki.

Kwa ujumla wananchi wa sehemu zile walitakiwa kuondoka na kupitisha upanuzi wa Hospitali hiyo. Kwa ujumla wananchi hawakuwa na pingamizi kwa suala hilo, ni moja kati ya masuala ya maendeleo katika kisiwa chetu isipokuwa tu Mhe. Spika, katika suala hili wananchi bila shaka walitakiwa kupatiwa fidia zao. Nashukuru kwamba kati ya wengi wa wananchi hao wamepatiwa fidia na wengine walikubaliana na fidia hiyo, lakini kinachojitokeza kuna baadhi ya watu ambao wamehisi kwamba fidia hiyo haikukidhi nyumba zao ambazo zitapisha utanuzi huo na kwa ujumla watu hao hawakuchukua fidia hiyo.

Sasa ningemuomba Mhe. Waziri akanieleza kwamba zile fedha ambazo walitakiwa wazichukuwe ziwe kama fidia ziko wapi na kuna utaratibu gani utakaotumika hata watu wale waridhike kuzichukuwa fedha hizo.
Mhe. Spika, jengine ni kuwa kuna baadhi ya wananchi wawili ambao wao mpaka siku ya mwisho ya malipo walikuwa wakionekana katika orodha ya watu ambao watalipwa, lakini la kushangaza ni kwamba watu hao siku ya mwisho waliambiwa wao hawatakuwamo katika orodha hiyo ya malipo. Sasa kwa maelezo yaliopo ni kwamba walitakiwa wao waonane na Mkuu wa Wilaya, kwa sababu wao mambo yao yalikuwa bado.

Sasa ningeomba Mhe. Waziri, akatuwekea wazi, je, wale wao watakuwa wamo kwenye mpango huu wa malipo au hawamo na kama hawamo ni kwa sababu gani na mwazo waliorodheshwa.

Jengine Mhe.Spika, maelezo haya yanasema kwamba kuna ujenzi wa msikiti. Bila shaka kwa taarifa hii ni kwa ujenzi ule uliotakiwa pesa zake ziwe zimeshapatikana. Hadi nazungumza suala hili Mhe. Spika, hadi jana baada ya kufuatilia, Katibu wa Wizara ya Afya nasikia alifika katikaWilaya ya Mkoani na kueleza kwamba yeye amekuja na *cheque,* lakini kuna mabadiliko kidogo kwamba hivi sasa ametokea mfadhili ambaye yeye atafadhili ujenzi kwa kujenga *foundation* ya msikiti ambayo itaruhusu ujenzi wa ghorofa. Kwa hivyo, *cheque* ile hawakukabidhiwa wananchi.

Sasa mimi nilitaka kujua zaidi, je, kuna ukweli gani kuhusu suala hili. Wale wananchi watapewa fedha zile kama zilivyotengwa au mfadhili atatokea kwa ajili ya ujenzi wa hiyo *foundation* ya ghorofa na je hayo ndio makubaliano ya mwanzo. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri akatoa ufafanuzi, kabla ya suala hili kuchafuka katika sehemu hiyo ya utanuzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee.

Lakini jengine Mhe. Spika, hapo hapo Abdalla Mzee, nashangaa sana kwamba wale madaktari waliopo hivi sasa, sijui wana utaalamu wa kiasi gani? Kwa sababu wanachotumia nahisi ni kiini macho. Imani yangu ni kwamba ili umtibu vizuri mgonjwa, basi unatakiwa ujue tatizo linalomsibu mgonjwa, lakini hivi sasa Mhe. Spika, ninachokijua huu unafika mwezi wa nne Hospitali ile haina *X-ray*, ingawaje kuna upungufu wa *OC* kwa wizara zote, lakini kama walivyokwisha sema wenzangu, kwamba wizara hii ni muhimu sana. Kwa hiyo, ile *O* sasa tuibadilishe, kwa sababu *O* kwa lugha nyengine ina maana nyingi, maana mpaka mwisho itakuwa *OC* hakuna na *O* ni *Nill* kwa lugha nyengine.

Huu si uamuzi wa busara. Ningeomba kwamba hili kama tatizo ni fedha, basi Wizara ya Fedha ikajiandaa, kwa karne tunayokwenda isifikie wakati tena ikawa *X-ray* ikawa tena ndio nyimbo, hakuna.

Nashangaa kwamba leo tunaingia katika ujenzi wa Hospitali kama hii ambayo itakuwa ni ya kisasa kabisa, lakini matayarisho yake sijui yakoje, kwa sababu hata *X-ray* hakuna . Sijui hawa wataalamu ambao watatakiwa kuhudumia hiyo Hospitali watakuwaje? Kwa sababu hakuna hata madaktari ambao wamekwisha andaliwa kwa ajili ya kuja kuhudumia hiyo Hospitali. Ningeomba Mhe. Waziri, haya akayazingatia kabla ya kufika hiyo hatua.

Mhe. Spika, labda niende kidogo kwenye Sekta ya Elimu kwa vile na mimi nilitokea kwenye sekta hiyo. Hivi sasa kuna utaratibu wa kufanya mitihani kwa madarasa ya saba na madarasa ya 10 na mara nyingi tunaposubiri matokeo huwa tunapewa tathmini mwanzo wa yale matokeo, kwamba mara hii yamekuwa hivi. Pia, huwa wanatwambia kwamba wilaya fulani imefanya vizuri na wilaya fulani imefanya vibaya. Sasa ningeomba wizara ikatwambia, labda wakati wakigundua kwamba wilaya fulani ndio ambayo imefanya vibaya, huwa wanachukuwa taratibu gani ili kuweka skuli ile ikafikia lengo wanalolitaka?

Jengine Mhe. Spika, ni kwamba wakati wa kufanya tathmini ya mitihani au kupasisha wanafunzi kunakuwa na vigezo kila mwaka. Mwaka huu tumeweka kiwango hiki, uwe umepasi na mwaka huu kiwango hiki. Nafikiria huwa mara nyingi tunakwenda kisiasa zaidi.

Sasa sijui wizara haioni kwamba hii ndio inayoathiri matokeo ya darasa la saba na darasa la kumi, inakuwa zaidi ni kwenda mbele si kupasi, lakini matokeo ya darasa la 12 ambao mtihani hauko katika umiliki wetu inakuwa tunafeli. Sasa sijui wizara haioni ile kwamba kujaalia tu kwamba mara hii tufanye asilimia 75% wapasi, husababisha wale wanafunzi wetu watakapofika darasa la 12 wakawa hawana uwezo na matokeo yake yakawa ni ile zero. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, naomba na mimi nichangie angalau kwa machache tu katika taarifa hii iliyowasilishwa na Kamati. Kwanza nataka na mimi nichukuwe nafasi hii Mhe. Spika, kuipongeza sana Kamati kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na kwa kweli wanastahili sifa na mimi naunga mkono taarifa ya Kamati.

Mhe. Spika, kwa sababu Kamati hii ndio tumeanza shughuli zile ambazo zinazotekelezwa na wananchi kuzikataa moja kwa moja, nimeona ni vyema na mimi nikatoa ufafanuzi kidogo hasa pale ambapo ilipokuwa inazungumziwa kuhusu habari ya Bajeti na upatikanaji wa fedha na hii itasaidia sana kwa Kamati zinazokuja ili kuweza kufahamu hali halisi.

Mhe. Spika, naomba kidogo nilikumbushe Baraza lako tukufu, wakati wa kupitisha Bajeti mwezi wa sita nililiarifu Baraza lako tukufu kama ifuatavyo:-

Serikali inatarajia kukusanya mapato ya ndani bilioni mia nne na ishirini na tatu halafu nikaendelea kufafanua, *ZRB* watakusanya bilioni mia moja na hamsini na tano nukta tatu . *TRA* watakusanya bilioni mia moja na arubaini na saba nukta sita na nyengine zitatokana na mkopo wa ndani; bilioni ishirini na tano. Fedha ambazo zilibakia mwaka jana, tukazileta mwaka huu bilioni tano, *JBC* bilioni arubaini na *NDRI* bilioni mbili. Ukizijumlisha hizo utapata bilioni mia nne na ishirini na saba. Katika kipindi cha miezi sita, *ZRB* tulipanga wakusanye bilioni sabini na tano nukta moja. Kwa bahati nzuri *ZRB* wamekusanya bilioni sabiini na saba nukta mbili, asilimia 103%.

TRA tulipanga wakusanye bilioni sabiini na mbili nukta saba, wamekusanya bilioni sitini na tano nukta tatu. Mkopo wa ndani hatujachukua, bilioni ishirini na tano na *MDRI* bado hatujaziweka kama tumeshazitumia. *JBC* imepatikana 100%. Ukitazama kwa ujumla wake Mhe. Spika, tumeweza kufanikisha kukusanya asilimia 95% ya miezi sita tulioipanga, yaani, bilioni mia moja na thamanini na moja nukta saba, tumeweza kukusanya bilioni mia moja na sabiini na mbili nukta tano sawa na 95%, tumeweza kukusanya kwa zile tulizozipanga kukusanya miezi sita.

Hebu tuangalie matumizi basi, hapa ndipo ambapo kila mmoja alikuwa anapaulizia. Mhe. Spika, kwanza tumepanga kulitoa suala la mishahara, mwaka jana tumeboresha mishahara kwa sababu tulikuwa na matatizo ya wataalamu wetu kuondoka nchini. Tukasema ni dhahiri kwamba tuboreshe mishahara ili kuwasaidia wataalamu wetu wabakie na wananchi wetu vilevile kupata matumizi mazuri.Tumepanga kutumia shilingi milioni mia moja na hamsini na tano nukta tano bilioni kwa mwaka, maana yake mapato yote yanayokusanywa na *ZRB*, tunatumia kwenye mishahara.*ZRB* ndio wanaokusanya sehemu kubwa ya mapato ambayo nimeyaeleza. Wao wanakusanya mia na hamsini na tano nukta tatu, wakati wenzao *TRA* wanakusanya mia moja na arubaini na saba nukta tisa.

Kwa hivyo, mapato yetu yote ya *ZRB* tunayapeleka kwenye mishahara na huu ulikuwa uamuzi wetu na wala sio uamuzi mbaya kuwasaidia wataalamu na wafanyakazi wetu na wao wajisikie kuwa wanapata angalau mishahara iliyokuwa afueni.

Mhe. Spika, katika miezi sita tumepanga tutumie bilioni sabiini na sita nukta nne tano kwa ajili ya mishahara. Tulichotumia ni bilioni sabiini na saba. Tumepanga kutumia sabiini na sita nutka tano, tumetumia sabiini na saba nukta nne nne. Hapa ni dhahiri Mhe. Spika, kwamba lazima kuna pahala tutazitoa pesa zile tuzipeke kwenye mishahara, kwa sababu ndio *first charge* katika serikali yoyote ile kuendesha shughuli za serikali na hakuna pengine tulipozitoa, tumezitoa kwenye *OC* na tumezitoa kwenye *Development Fund* ili kukidhi mishahara.

Mhe. Spika, lakini nataka niseme tu kwa sababu ule mkopo wa bilioni ishirini na tano hatujauchukuwa na huwezi tu ukaingia kwenye Bajeti ukasema unataka kuanza kuchukuwa mkopo, huko mbele unapokwenda ukishindwa huna sehemu ya kwenda. Ule mkopo tumeuwacha na tulipoiona hii hali ya *OC* zetu kuwa ndogo na *Development Fund* zetu kuwa kidogo, alisema pale Mhe. Hamad Masoud Hamad rafiki yangu, swahibu wangu, tulikuwa nae huku huku. Nashukuru angalau kidogo na yeye anapata kusema.Hivyo, alisema *OC* iko 33%, ni kweli na yeye akasema kwamba *Development Fund* iko 2%, ni 16%. Mpango wetu wa kuchukua bilioni ishirini na tano ambao tunataka tuchukuwe katika kipindi hiki cha mwezi wa Febuari na Machi, utasaidia kwa kiwango fulani kukuza hii hali ya *OC* pamoja na *Development Fund*.

Mhe. Spika, ninachotaka kusema ni kwamba matumizi yetu yote kwa mwaka nilisema bilioni mia nne na ishirini na tatu kutokana na mapato yetu ya ndani. Miezi sita tulipanga kutumia bilioni mia moja na thamanini nukta nne. Katika matumizi ya miezi sita yote tumetumia bilioni mia moja na sabini na tano, ni

97% ya matumizi tuliojipangia kutumia miezi sita, lakini ukitizama kwa mwaka ni 41% ya mwaka.

Mhe. Spika, kwa hivyo, nataka nilieleze Baraza lako tukufu serikali sio kwamba haitaki kutumia wala kupeleka pesa kwenye sekta fulani, ndani ya serikali sekta zote zina umuhimu. Leo hapa tunazungumzia Afya na Elimu. Mimi nawashukuru sana Wajumbe wanazungumiza afya na Elimu, lakini tukija kwenye Bajeti, watazungumzia na maji.Watazungimzia Ole, Kengeja na barabara, vyote hivyo ndani ya serikali ni muhimu.

Mimi nakubaliana nao kwamba tutoe umuhimu maalum au wa pekee kwa Sekta ya Afya na Sekta ya Elimu. Mimi mwenzao, Waziri wa Fedha niliepewa dhamana nimelichukuwa na nitawashawishi wenzangu hawa ambao tumelisikia kwa pamoja, ili tulione hili ni kweli. Mwanachi anahitajia elimu na afya, lakini anaehitaji afya ni yule mgonjwa na anaehitaji elimu ni yule anaetaka kusoma, lakini maji tunahitaji sote.Kwa hivyo, ukizungumza kwamba kama kuna sekta hii na hii kwenye serikali, Mhe. Spika, kweli sisi sote tunapa umuhimu wa pekee, lakini nasema kwamba tumelipokea suala hili na mimi nataka niwashukuru wale wote ambao wameichangia hii ripoti na kusema kwamba ipawe kipaumbele.

Kuna mambo ambayo wameyazungumza nadhani Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Waziri wa Elimu watayatolea ufafanuzi. Msauala haya ya jiko la kuchomea taka tayari serikali imeshafanya maamuzi, wao watayatolea maelezo. Mimi langu ilikuwa nitoe hizo *figures* mzione, mapato yetu yanaongezeka sana.

Tulipoingia mwezi wa Novemba mwaka 2010, tulikuwa tunakusanya *TRA* na *ZRB* kwa pamoja kwa mwezi bilioni kumi na tatu, lakini leo tunakusanya kati ya bilioni ishirini na saba na ishirini na nane kwa mwezi. Mapato yetu yameongezeka, lakini na sisi tumepanua matumizi, tunafikiria jinsi ya kubana kidogo matumizi, ili tuende kulingana na hali halisi ya mapato yetu.

Kila siku asubuhi Katibu Mkuu na watalamu wangu wanafanya mzunguko kuangalia mapato yetu yanayoingia kila siku asubuhi na kila mwezi kuna Kamati ya Makatibu Wakuu wanagawana *OC*.

Mimi nadhani Mhe. Spika, nisiseme mengi, nataka niwaambie Waheshimiwa Wajumbe kwamba mimi naunga mkono na mawaziri wenzangu hapa katika Bajeti inayokuja tutaziangalia vizuri zaidi sekta ya Elimu na sekta ya Afya, ili ziwe ni kichecheo, lakini Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wasitulazimishe au wasitutake tukaziacha sekta nyengine, nazo ni muhimu pia.Tunaweza tukafanya maongezi ya sekta hizi hata kilimo 44% ya pato letu

la Taifa linachangiwa na kilimo. Asilimia 70 ya watu wetu wako kwenye sekta ya kilimo. Huwezi ukasema sekta hii tuiwache lazima tuipe kipaumbele nayo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo namalizia kwa kukubaliana na hoja ya Kamati na mimi naiunga mkono mia kwa mia. Ahsante sana.(*Makofi*)

Mhe. Spika: Nakushukuru Mhe. Waziri wa Fedha kwa ufafanuzi huo, niendelee kuwaomba radhi Waheshimiwa Wajumbe wale ambao hamkupata nafasi. Wako wengine walinambia niwaingize katika orodha, na niwape dakika tatu, wengine walinambia mbili tu, lakini huo muda wenyewe sinao, naomba radhi sana. Sasa Waheshimiwa Wajumbe twende kwenye hatua nyengine. Nimkaribishe basi Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawakae na Watoto.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawakae na Watoto: Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima wa afya. Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika pamoja na ...

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunakwenda kusali, tukisha sali tukumbuke kurudi ili tuendelee na shughuli yetu na kumaliza kazi hii. Mheshimiwa endelea.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawakae na Watoto: Mhe. Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yao mbalimbali wanayotupa katika kutelekeza na kutuelekeza majukumu ya wizara.
Mhe. Spika, naomba uniruhusu nitoe pongezi maalum kwa Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa taarifa yake nzuri na safi inayoeleweka, naomba niseme hongera sana, lakini pia, nitakuwa si mwingi wa fadhila kama sitampongeza nae Mhe. Mwenyekiti mwenyewe kwa kazi nzuri anayoifanya wakati tukiwa pamoja.

Nachukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wote waliochangia katika maagizo yangu niliyokuwa nayo hapa, ambayo niliagizwa na Kamati hii ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, aidha pongezi zote tulizopewa tumezipokea vizuri na kwa umakini sana. Wajumbe hapo walikuwa wanatupa pongezi kuhusu Sebleni, kwa namna tunavyoshirikiana na tunavyofanya kazi kwa ufanisi.

Mashirikiano makubwa wanapata Kamati ndio maana wakatupa pongezi hizi, si za bure.

Nachukuwa fursa hii sasa kuwashukuru Wajumbe wote waliochangia na naomba niwataje;

Mhe. Hassan Hamad Omari
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
Mhe. Mgeni Hassan Juma
Mhe. Farida Amour
Mhe. Abdi Mosi Kombo
Mhe. Fatma Mbarouk Said
Mhe. Hamad Masoud Hamad
Mhe. Salum Abdalla Hamad
Mhe. Abdalla Moh'd Ali
Mhe.Waziri wa Fedha.

Mhe. Spika, yale mengi ambayo yameelezwa na Kamati, Mwenyetiki nimeshayatolea ufafanuzi katika taarifa ambayo nimewasilisha na yale ambayo hayajajitokeza kwenye taarifa hiyo, ndio ambayo nitakayoyatolea ufafanuzi. Kwanza yote nayaunga mkono, nayakubali na nitayafanyia kazi.

Mhe. Spika, sina nia ya kumjibu mmoja mmoja, lakini nataka nianze na Mwenyekiti wa Kamati. Mhe. Spika, nikianza, kulikuwa na suala kuhusu kushajihisha jamii kutoa ushahidi katika kesi za udhalilishaji. Wizara ikishirikiana na wadau mbalimbali vikiwemo vyombo vya habari, inaendelea na kampeni ya kupinga vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia, ikiwemo umihimu wa kutoa ushahidi.

Mhe. Spika, Wizara kwa kushirikiana na Kamati za kupinga udhalilishaji za shehia, zinafanya juhudi kubwa za kuelimisha jamii juu ya kutoa ushahidi, lakini napende kusisitiza na kutoa pendekezo kwa Mahakama zetu kwamba kesi hizi ziharakwishwe utoaji wake wa hukumu. Kwani kuna urasimu mkubwa wa utoaji wa haki na watoaji ushahidi huchoka nao kwenda Mahakamani kwa ajili ya kutoa ushahidi.

Mhe. Spika, nakubaliana na Kamati kuwa wafanyakazi wa nyumba za watoto hawana taaluma ya kutosha ya kuhudumia watoto wenye mahitaji maalum. Wizara katika mwaka wa fedha ujao 2014/15 itahakikisha kwamba wanapatiwa mafunzo hayo ili wafanyakazi hao waweze kuhudumia vyema watoto kwa imani, upole na unyenyekevu hasa kwa wale wenye mahitaji maalum.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kuongeza wahudumu kwenye nyumba za wazee Sebleni. Wizara hii italifanyikazi na maombi ya wahudumu wanaohitaji kuongezwa tutayazingatia katika *nominal roll* ya mwaka 2014/15. Hivi sasa pia wizara imeshapeleka maombi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa ajili ya kujaza nafasi zilizoachwa wazi na wahudumu waliostaafu.

Mhe. Spika, kuhusu matengenezo ya jengo la Idara ya Ushirika. Hatua za kuwapata wataalamu wa kufanya tathmini ya gharama za matengenezo zimefanywa na wataalamu wameshalikagua na kulipitia jengo hilo. Sasa tunasubiri ripoti yao ya mchanganuo wa gharama kwa kuombewa fedha.

Mhe. Spika, kuhusu utoaji wa elimu ya mikopo. Wizara imeimarisha taratibu za utoaji na urejeshaji mikopo kupitia mfuko wa uwezeshaji. Wizara inatoa taaluma ya awali kwa wakopaji kabla ya kupewa mikopo ili watumie mikopo kwa ufanisi na wapate tija na faida. Aidha, wizara huwa inatoa taaluma kwa wakopaji juu ya kuendesha vizuri baishara zao ili waweze kurejesha mikopo.

Kuhusu malipo ya fidia. Wizara italisimamia suala hili la fidia kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha. Kwa maelekezo au meelezo yake aliyoyatoa sasa hivi hapa, tuna imani kwamba jambo hili litatekelezwa.

Kuhusu suala la ununuzi wa Jenereta. Wizara itazingatia katika Bajeti ya mwaka ujao 2014/15 kwani nasi tunaona umuhimu wake katika kuleta ustawi mwema wa watoto walioko katika nyumba ya watoto, Mazizini.

Mhe. Spika, wizara inaendelea kushirikiana na vijana wa Skauti kwa kuwapatia mafunzo na ushauri juu ya kuendeleza Skauti Zanzibar. Hata hivyo, suala la sare za Skauti ni jukumu la Skauti na Mhe. Mwakilishi pamoja na Mhe. Waziri, tukishirikiana kwa pamoja ili watoto waweze kupata kivazi hicho.

Mhe. Spika, wizara bado haijaanzisha Benki wa Wanawake. Kwa sababu uanzishwaji wa benki unahitaji maandalizi ya kutosha. Katika kufanya maandalizi hayo, wizara imeshafanya upembuzi yakinifu pamoja na mpango wa biashara wa benki hiyo na hatua za kitaalamu zinaendelea. Aidha, wizara ina mpango wa kuunganisha nguvu ili benki hiyo itakayoundwa iweze kuwahudumia wanawake na Vyama vya Ushirika.

Mhe. Spika, kuhusu suala la ajira. Wizara imekuwa ikitekeleza shughuli mbalimbali kwa lengo la kukuza ajira kwa wanawake na vijana, hii ni pamoja na utoaji wa mikopo kwa wananchi ili waweze kujiajiri kupitia shughuli za Ujasiri amali.

Mhe. Spika, pia, wizara huwa inaandaa mafunzo maalum juu ya Ujasiri amali kwa vijana na wanawake, ili waweze kuimarisha bidhaa zao na kujiongezea kipato. Mhe. Spika, wizara itafanya tathmini ya mahitaji ya wafanyakazi na walezi na kujaza nafasi zinazohitajika. Aidha, wizara hivi sasa iko katika mpango wa kuwaajiri wafanyakazi wapya ili kujaza nafasi za wafanyakazi waliostaafu.

Mhe. Spika, hivi sasa wizara kupitia Idara ya Ushirika, inatoa taaluma kwa viongozi na wanachama wa Vyama vya Ushirika ili wajue haki na wajibu katika kuendeleza Vyama vya Ushirika. Wizara itaendelea kutoa taaluma hii ili wananchi waelewe zaidi zana ya ushirika na umuhimu wake. Mhe. Spika, suala la kuwawezesha wanawake na vijana lina mpango maalum na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaalia tutalifanyia kazi.

Mwisho, nataka nimalizie kwa kusema kwamba nashukuru sana kwa mchango mkubwa alioutoa Mhe. Omar Yussuf Mzee (Waziri wa Fedha). Hii nadhani itasaidia kujibu hoja na matatizo mbali mbali yaliyopo mbele yetu. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa na mimi nafasi hii ili niweze kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya masuala ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wawakilishi, ili waweze kufahamu hali halisi ilivyo katika Wizara yetu.

Napenda pia niwashukuru Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa jinsi walivyotupa mashirikiano na wanavyoendelea kutupa mashirikiano, kwa kuiona hali yetu ilivyo na kutambua uhalisia wa mambo baada ya wao kufika pale na kujua nini kinachotusibu mpaka tunashindwa kukamilisha mambo haya. Lakini pia, napenda niwashukuru wale wote waliochangia na ambao hawakupata nafasi kwa kuwa najua kwamba walikuwa na nia njema isipokuwa muda haukutosha.

Mhe. Spika, nitajibu baadhi ya vipengele ambavyo kidogo nahisi kwamba hivi vinahitaji utaalamu na mengine atajibu Mhe. Waziri. Na zile ambazo si za kitaalamu, lakini zinanihusu moja kwa moja naweza kuzitolea ufafanuzi.

Tumezungumza kuhusu suala la Bajeti ya Wizara ya Afya. Bajeti ya Wizara ya Afya tunapangiwa na tunatakiwa tupewe, tunapewa tunachokipata na tunatumia hicho. Mhe. Spika, bajeti ya Afya tunayoipanga kama tutapanga kweli uhalisia wa bajeti ya Afya tutachanga Bajeti ya serikali nzima ili tuweze kununua vitu na madawa na ndio maana wanapoingia wafadhili kuweza kutusaidia. Shirika la Afya linapotoa maelekezo linakuwa na vipengele maalum vya misaada kulingana na lile ambalo linatakiwa lifanyike.

Mhe. Spika, Kwa hiyo, pale tunaposema mfadhili kachangia kiasi hiki na serikali imechangia kiasi hiki, sio tu kwamba tunasema kama ni suala la utegemezi, lakini ndizo taratibu za Wizara yetu zilivyo. Wizara ya Afya kokote hata Bara wanachangiwa sana tena kwa mamilioni ya mapesa. Kwa hiyo, huo ndio utaratibu. Sasa tusione kwamba serikali haifanyi kazi au haitoi pesa, lakini ili Wizara iweze kwenda. Kwa sababu katika Wizara ya Afya hakuna kitu kidogo ukilinganisha na pesa zake utashangaa mwenyewe.

Mhe. Spika, Kwa hiyo, wafadhili wataendelea kuwepo na misaada itaendelea kutolewa kwa sababu ni haki yetu kupata misaada ile na tunaihitaji na mingine tunaandika sisi kuomba kwa sababu hata kama tutataka serikali ifanye haitoweza kufanya hivyo kulingana na yale mapato ya serikali na kile tunachopewa. Kwa hiyo, ni wajibu wetu sisi kuhakikisha tunaandika, tunaomba, ili kukidhi haja ya serikali yetu kutoa huduma kwa wananchi wake.

Jambo jengine ambalo ningependa kulitolea ufafanuzi ni suala la Kitengo cha Macho, kimezungumzwa na wengi. Kitengo cha Macho kilikuwepo Hospitali ya Mnazi Mmoja kilifanyiwa matengenezo, baada ya muda si mrefu sana kikapata matatizo, kutokana na ufundi uliotengenezwa tukaambiwa kwamba kilichotengenezwa kulikuwa kuna matatizo na utengenezaji wake ulikifanya kitengo hichi kisiwe imara kwa sababu kimeziba zile njia za asili za kupitisha hewa. Ikabidi Wawakilishi wakalalamika tuhame na tukahamia Kibweni. Kibweni wenyewe walipotaka kufungua Hospitali yao ikabidi tuhame, tukahamia Kwamtipura.

Mhe. Spika, Sasa kitengo ukikitizama jengo lake ni kubwa kulikuwa na juu na chini, lakini Kwamtipura kuna nafasi ndogo mno. Kwa hivyo, vyombo tulivyokuwa navyo ni vingi hatukatai ni kweli, lakini nafasi ya Kwamtipura kama tunavyoiona hakuna jinsi ya kuviweka vyombo vile mpaka vikaenea. Kwa hiyo, kama hatukuweza kupata lile jengo ambalo kwa mwaka huu haitowezekana kwa sababu halikuwemo kwenye bajeti, tutashindwa kuvipanga vile vyombo vikaenea.

Kwa hiyo, vimewekwa vyengine, haviwezi kutumika kwa sababu ya nafasi. Kwa hiyo, sio kwamba tunavibadhiri isipokuwa ndio hali halisi. Mwakani tukijaaliwa tutaweka kwenye bajeti, tukipatiwa bajeti na tukipata pesa, tutalitengeneza jengo la macho na watu watarudi pale wafanye kazi kwa nafasi. Suala hilo ndilo lililojitokeza.

Kitu kingine ambacho nataka kukitolea ufafanuzi ni suala la *X-ray*. Wamezungumza hapa *CT Scan na X-ray*. Kwa hivyo, *CT Scan* nafikiri imetolewa ufafanuzi wake, kukubali na kutokukubali hayo ni mengine. Lakini ukweli utabaki ule ule kwamba *CT Scan* inatakiwa kufanyiwa *service*,

ikifanyiwa *service* kuna vitu vinatakiwa vibadilishwe na kama vitu vinatakiwa kubadilishwa ina maana vinatakiwa kununuliwa. Kuna watu wanatakiwa waje wafanye hiyo kazi na gharama hiyo sio ndogo. Kwa hiyo, wakati ule wa Bajeti unapofika na kama sisi pale hatuna, kama na Wizara ya Fedha tunaomba kwa kipindi kile wakishindwa kutupatia fedha zile na ambazo zinakuwa nyingi itabidi tusubiri taratibu zinafanyika mpaka muda tunaopata pesa vifaa vinanunuliwa, saa nyengine wanatukopesha baadae tunakuja tunalipa taratibu.

Kuhusu *X-ray*, nataka niseme hivi. *X-ray machine* ina sehemu mbili muhimu, kuna sehemu ya kwanza ambayo inapiga picha, unakwenda kama mkono umevunjika unaweka mkono wako na unapigwa picha tunaona kama ndani kumevunjika ama la. Kama ni kifua unakwenda unasimama na kupiga picha na tunaona kilichoko ndani, lakini sehemu ya pili ya *X-ray* ile ni sehemu ambayo inatizama viungo vya ndani na kwa kutumia dawa maalum inaitwa *Fluoroscope*.

Sehemu hiyo ndio ambayo ina matatizo. *X-ray* ya kawaida inayopiga mifupa na picha za kifua, hiyo inafanya kazi na hiyo ndio inayotumika asilimia zaidi ya 90 ya kufanya kazi ya *X-ray machine.* Kwa hiyo, mtu anaposema *X-ray* haifanyi kazi, ni hao wanaowaambia na nataka waambiwe vizuri ili wafahamu, badala tu ya kusema tu hazifanyi kazi. Huyo mgonjwa wa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kapigwa *X-ray* hiyo hiyo wakati huo alipopata ajali. Kwa hiyo, *X-ray* kwa upande huo inafanya kazi, Fluoroscopy inatizama watu wasiopata ujauzito.

Kwa hiyo, lazima tutie dawa katika mafigo na vitu vyote vya ndani kama hivyo ambavyo vinahitaji dawa upande huo haufanyi kazi, lakini wameshakuja mafundi walipokuja kutizama *CT Scan* na ile wameitizama. Kwa hiyo, wametuletea *invoice* ikabidi tupeleke iweze kurekebishwa.

Mhe. Spika, kitu kingine ninachopenda kukizungumzia hapa ni kuhusu wagonjwa wanaopelekwa nje. Mhe. Mwakilishi, mmoja hapa alisema kwamba Wizara yetu inapeleka zaidi ya mara tatu ya kile kinachotakiwa kulipwa kule. Hilo labda lina hisia nyengine ambayo anaifikiria yeye labda rushwa, labda sisi tunafanya ubadhirifu na mengineyo. Sina uhakika alikuwa anakusudia nini na akasema kuna mtu kaenda huko, lakini kilicholipwa ni kidogo mno karibu mara tatu ambacho kile Wizara ya Afya inapeleka.

Mimi kama nataka kuiangalia kesi hiyo niwe mkweli, huyo mtu alikuja akaenda kwa madaktari wetu wakamwambia hichi kinaweza kikafanyika hapa Zanzibar, yeye hakutaka, ni kitu kidogo sana kwa madaktari wetu kumudu kukifanya, lakini akaondoka akenda India akafanyiwa na kweli kilichukua

pesa kidogo kwa sababu ni kitu kidogo. Sisi tunapopeleka wagonjwa India *Miot Hospital* kwanza hatulipi pesa, tunapeleka tunachofanya, tunafanya makadirio ya nauli ya msindikizaji na mgonjwa mwenyewe na makadirio ya malipo ya matibabu yatakayofanyika kule. Wao kule wanafanya hiyo kazi, wakifanya kazi yao, wakifanya vipimo, wakifanya dawa na pengine inabidi tutoe dawa labda za mgonjwa wa miezi sita baadae, hapo ndipo wanapotuletea gharama kusema kwamba kiasi hichi ndicho kilichotumika kwa ugonjwa huu.

Siku nyengine kile tulichokadiria kinatosha, siku nyengine kinazidi gharama ile inategemea mgonjwa gani kapelekwa kule. Tunapeleka wale wagonjwa walioshindikana Zanzibar na mgonjwa aliyeshindikana hata akenda kule ujue kwamba gharama itakuwa kubwa, tofauti na huyo mgonjwa wake yeye aliyekwenda akenda akatolewa kitu kwa dakika tano, gharama zitabadilika. Kwa hiyo, kinachopelekwa kule na kinachosemwa ni cha kweli wala watendaji hawajawahi kufanya ubadhirifu kwa hilo. Kwa sababu baada ya matibabu, ndipo tunapoletewa bili na serikali ndipo inapolipa.

Mhe. Spika, kitu kingine ambacho nataka nikitolee ufafanuzi naona hapa kama Wawakilishi kidogo wanajichanganya labda kwa kuwa hawaelewi utaalamu ukoje. Wamama wajawazito, wanapokuja hospitali wanapimwa ukimwi na hichi hakihitaji *DNA,* anapimwa pale ni kipimo cha dakika tano, anao ukimwi au hana. Kama anao anasajiliwa anapewa dawa za kumkinga mtoto na mtoto anapozaliwa, anapewa dawa za kumkinga ukimwi. Mtoto baada ya miezi 18 anapimwa tena kujulikana kama ana ukimwi au hana. Kwa hiyo, hapa suala la *DNA* halina mahusiano. Kwa hiyo, tutafute *DNA* ilisemwa wapi? Lakini hapa si pahala pake.

Mengine hapa kuna suala lilizungumziwa kuhusu maradhi yaliyokuwa hayakupewa kipaumbele. Anataka kufahamu hayo maradhi yasiyopewa kipaumbele ni yepi. Maradhi yote ni maradhi, lakini katika ulimwengu kuna vipimo vya maradhi na vile ambavyo vinaua haraka vinakuwa vinapewa kipaumbele kwa sababu vinaua sana, vinaua watu wengi na kwa muda mfupi. Kuna maradhi mengine yanachukua muda mrefu na yapo katika nchi kidogo tu. Kwa hiyo, hayo yalikuwa huko nyuma hayatizamwi sana. Tulikuwa tunashughulikia kifua kikuu, ukimwi, *cholera* na vitu kama hivyo ambavyo vinaua watu kwa mara moja.

Sasa baada ya hayo maradhi kuteremka chini, kuna maradhi mengine ambayo zamani yalikuwa hayakupa nafasi, lakini hayaui haraka. Kwa mfano kichocho, ukoma, *trachoma* maradhi ya macho, hayo hayaui. Kwa hiyo, kwa kipindi hicho yalikuwa hayana nafasi mbele ya maradhi yanayoua. Sasa hivi tumepata nafasi maradhi hayo nayo yanashughulikiwa. Kwa hiyo, kitengo

maalum kimeundwa cha maradhi ambayo hayakupewa kipaumbele, sio kwa sababu sio maradhi, isipokuwa kwa umuhimu wa wakati ule na sasa hivi ndio tumepata nafasi ya kuyashughulikia hayo. Kwa hiyo, hilo ni jina la maradhi yaliyokuwa hayakupewa kipaumbele hapo nyuma, leo hii yameshapewa nafasi na yanashughulikiwa. Kwa hiyo, naomba ifahamike hivyo.

Suala jengine hapa linazungumzia mgonjwa wa Mhe. Fatma Mbarouk Said. Kwa kweli nimehangaika sana mimi kama binadamu, kama Mwakilishi mwenzangu, kama daktari kuhakikisha kwamba tunaponya na kuhakikisha kwamba mgonjwa yule katoka salama. Ninachotaka kusema Mhe. Fatma Mbarouk Said, asikate tamaa kwa sababu kilichotokea si uzembe wa madaktari, wala daktari aliyemhudumia mgonjwa si mwanafunzi, ni *specialist* aliyepo kwenye kitengo kile.

Mgonjwa kaingia na tatizo jengine, lakini katika matatizo aliyokutwa nayo na upungufu wa damu ulikuwepo. Kilichotokea kama mgonjwa katiwa damu kujaribu kupandishwa damu kiwango kilichokuwa kimepungua. Katika kutia damu kama tunachukua suala la kutia damu, kumtia damu mgonjwa yeyote yule chochote kinaweza kikatokea, lakini kama damu iliyo salama akitiwa mgonjwa ni asilimia ndogo sana ya binadamu ambao wanapata matatizo ya damu, lakini nao ni binadamu. Kwa hiyo, hata kama ni asilimia 0.00 ina maana kuna mtu au kuna watu. Asilimia 0.0 ya mia utakuja ukakuta kwamba ni mtu mmoja, wawili, watatu, kitu kama hicho.

Kwa bahati mbaya mgonjwa wa Mhe. Fatma Mbarouk Said, nae ni katika hiyo asilimia 0.00, lakini wamo wanatokea na si wa kwake tu wa kwanza. Katiwa damu siku ile, lakini bahati mbaya kapata *reaction*, na *reaction* ya damu ndio hilo tatizo ambalo wagonjwa wanapata. Sio kwa sababu damu ilikuwa mbaya, sio kwa sababu damu haikupimwa, isipokuwa ni katika hao ambao wenye bahati mbaya katika maisha wanaoweza kupata tatizo hili. Ukipata *reaction* unachomwa sindano ili kupunguza *reaction.* Mgonjwa kachomwa sindano ili apumzike alale kwa sababu alikuwa kama kachanganyikiwa. Alipolala hakuja tena juu, hii haina maana kwamba ni uzembe, ni vitu ambavyo vinatokea.

Unapotibu *reaction* moja katika mawili, aidha mgonjwa atapona au atakufa. Tulijitahidi sana mimi na kundi la madaktari. Nilikuwa nakwenda nimepitia *case note* tangu mwanzo mpaka mwisho na sikuona uzembe uliotokea. Kwa hiyo, hili Mhe. Fatma Mbarouk Said, naomba utuamini kwamba tulijitahidi, lakini siku ilikuwa imeshafika.

Kitu kingine ambacho ningeweza kukisema hapa labda ni cha mwisho kuhusu uajiri wa madaktari na kada nyengine za afya. Mimi kila siku hapa

nikizungumza nazungumza kuhusu upungufu wa wafanyakazi katika Wizara ya Afya. Tuna vitengo vingi, tuna idara nyingi, tuna hospitali nyingi, tuna vituo vingi. Katika Wizara ambazo inahitaji wafanyakazi wengi baada ya Wizara ya Elimu ni Wizara ya Afya na ndio maana tunakataa jamani tena kujenga vituo basi.

Mheshimiwa, aliyezungumza kwenye wilaya yake kuna hospitali kubwa moja na vituo 19. Kwenye Jimbo lake kuna vituo vinne na kimoja tumekifungua juzi tu, kote huko kunataka wafanyakazi. Na sisi madaktari wetu tunaowasomesha wengine wanarudi, wengine hawarudi. Wanaosomeshwa Chuo cha Afya Mbweni, wengine wanakuja hospitali, wengine wanakuja Wizarani wanaajiriwa, wengine hawaji. Wakitoka Chuo cha Afya Mbweni wote tunawapa ajira, lakini sio wote wanaokuja. Kuna wanaokwenda Polisi, kuna wanaokwenda *private*, kuna wanaokwenda Tanzania Bara na kwengineko. Hatuna uwezo wa kuwazuia kwa sababu ni khiari yao kuja kuajiriwa serikalini.

Kwa hiyo, bado tutabakiwa na upungufu wa wafanyakazi na hili ni suala sugu, baada ya hili linakuja madawa na vifaa. Kwa hiyo, tutajitahidi kuajiri kila atakayekuja mpaka tutakapokuwa na uwezo wa kuweza kuhudumia vituo vyote, lakini pengo bado ni kubwa.

Juzi nilisema Pemba ina asilimia 78 ya upungufu na Unguja asilimia 48. Hiyo ni asilimia, lakini ukihesabu watu ni wengi mno. Kwa hiyo, naomba mtuelewe kwamba huduma tunataka kutoa, lakini wafanyakazi wametupungukia na hilo mlifahamu, hatuna jinsi nyengine ya kuweza kufanya. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba na mimi kueleza baadhi ya masuala yaliyojitokeza katika mjadala, lakini kabla sijaanza, lazima nitoe pongezi za dhati kwa Wajumbe wote pamoja na Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa jinsi walivyochangia tena kwa hamasa na kutuonea huruma Wizara ya Afya tulivyojaaliwa na changamoto zisizo ufumbuzi wa papo kwa papo.

Mhe. Spika, lazima nikiri kwamba tuna uhaba wa fedha, lakini uhaba huo Mhe. Waziri wa Fedha, ameeleza hali halisi ilivyo, pamoja na matatizo yote hayo mengi yamefanyika na mengine yamefanyika kwa ufanisi zaidi kuliko hata tulivyotegemea na kwa kiasi fulani lazima tuwashukuru wafadhili kwa michango yao mikubwa, mara nyengine huja ule wakati ambapo tuko hali mbaya, lakini kwa kawaida Mhe. Spika, huwa tunawafuata ili tushirikiane nao kusaidia huduma hizi na ni moja katika wajibu wa dunia ulivyo.

Mhe. Spika, baada ya kueleza utangulizi huo wa shukrani, naomba vilevile, nishukuru na kwa bahati nzuri wale aliowataja Mhe. Zainab Omar Moh'd, ni wale wale takriban waliochangia kwenye Wizara yetu. Ni vizuri muwatambue. Wa kwanza alikuwa Kaimu Mwenyekiti wa Kamati, wa pili Mhe. Jaku Hashim Ayoub, wa tatu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, wa nne Mhe. Ismail Jussa Ladhu, wa tano Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, Mhe. Mgeni Hassan Juma, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati hii, Mhe. Farida Amour Mohammed, Mhe. Abdi Mosi Kombo, Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Hamad Masoud Hamad, Mhe. Waziri wa Fedha, na Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, alituletea kwa maandishi.

Mhe. Spika, Naibu Waziri amejaribu kusaidia kupunguza baadhi ya mambo ambayo mengine ni ya kitaalamu ya kidaktari na mimi bahati mbaya sijui zaidi ya a, b, c ya hali halisi, lakini kwa jumla masuala mengi yaliyosemwa ni masuala ambayo unaweza ukayaweka makundi. Kwa hivyo, nitaeleza katika msingi huo na kuweza kutaja baadhi ya yale mambo ili nisichukue muda zaidi tumalize.

Kulitajwa suala la Hospitali ya Wagonjwa wa Akili, chakula, dawa, hali halisi ya mazingira na usafi wake na mengine. Tumeyasikia, tumeyazingatia na tumeyachukua, lakini baadhi ya mambo yanahitaji ufumbuzi wa muda mrefu na mengine yanahitaji ufumbuzi wa muda mdogo. Moja ambalo limewaumiza Wajumbe kuhusu hospitali ni suala la chakula.

Mhe. Spika, bajeti yetu ya chakula ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa jumla ilikuwa shilingi milioni 81 na kwa wastani ni milioni 6.7 kwa mwezi kwa Hospitali tatu, Mnazi Mmoja, Mwembeladu na Hospitali ya Wagonjwa wa Akili. Hospitali ya Mnazi Mmoja tunawanyima, ya Wagonjwa wa Akili tunahakikisha angalau inapata milioni 2. Sasa hizo milioni 6.7 kwa wastani kwa mwezi 6 iliyopita tumekuwa tukipata milioni 4, lakini hizo milioni 4 tunahakikisha milioni 2 zinakwenda kwenye Hospitali ya Wagonjwa wa Akili.

Kitu kinachotofautisha kidogo Hospitali ya Wagonjwa wa Akili na Hospitali ya Mnazi Mmoja ni kwamba unaweza ukawa na mgonjwa Hospitali ya Mnazi Mmoja, mara nyingi akiwa mzee wako utampelekea uji mchana, usiku na asubuhi utampelekea chai kwa kutegemea baada ya wiki moja, mbili anatoka. Wagonjwa wa akili wengi wao ni wagonjwa wa muda mrefu na moja katika tatizo lililopata katika jamii ni kutelekeza. Ni kwamba wengine husema sisi hatuna haja nae tena huyu. Kwa hiyo, anakuwepo pale ni *Laila haila Llahu Muhammada Rasulullah* wanangojea kudra ya serikali, wengine wanawaacha, hilo moja.

Pili, idadi ya wagonjwa wa akili imeongezeka hivi sasa wapo hawapungui mia, ni wengi na ni suala la kutisha. Na moja katika sababu hiyo ni kutokana na tatizo la kijamii tulilonalo la haya madawa ya kulevya, bila shaka na mazingira mengine. Kwa hivyo, si suala la kulitizama katika sura ya kupata chakula tu tukasema chakula hawapati. Tunakubali hilo na tuna wajibu, lakini ukweli ni kwamba na tatizo lenyewe ni kubwa.

Kwa taarifa ya Wajumbe kesho tuna Kamati Tendaji agenda hiyo tu juu ya suala la Hospitali ya Wagonjwa wa Akili. Tumetafuta wataalamu wetu pale wametuandikia ripoti kamili ya hali halisi ilivyo. Na baada ya kuisoma nimeshauriana na Naibu wangu na Katibu Mkuu kwamba tulijadili suala hilo halafu tulipitishe serikalini kueleza hali halisi.

Mhe. Spika, ili wagonjwa wote wa Hospitali ya Mwembeladu, Mnazi Mmoja na Hospitali ya Wagonjwa wa Akili wale kwa utulivu, milo mitatu kwa mwezi tunahitaji milioni 24, lakini Bajeti yetu tuliyonayo milioni 7.7. Kwa hivyo, si suala la kwamba hatutaki au hatuoni huruma. Kwa mwaka milioni 280, tumepewa milioni 81 ndio hali halisi. Kwa hivyo, si suala la hujambo shkamoo, ni suala la kukaa tukazingatia hasa nini cha kufanya. Hali hiyo hiyo ni hali kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja na Mwembeladu.

Suala la *CT Scan* ni kwamba kuna taratibu za sheria ya *Procurement*, inatulazimisha hatuwezi tukatoka tu tukenda tukanunua kitu moja kwa moja. Nadhani Naibu ameeleza kwamba *CT Scan* ni kweli ilikuwa mbovu, lakini utaratibu wa kununua *spares* umeshakamilika, nilivyoambiwa na watu wangu tunategemea wiki hii wale mafundi watakuja kumaliza kuvifunga vile vifaa, wapo Dar-es-Salaam, lakini hizo *spares* ilikuwa inabidi ziagizwe kutoka Ulaya na ndio hali ya umaskini.

Suala la *incenerator* sina hakika kwamba Waziri wa Fedha alilisema, lakini nalo vilevile, tumeshamaliza taratibu za ununuzi, yaani *tendering* hivi sasa tunataka kutiliana mkataba baina ya sisi na yule anayetuuzia. Kwa sababu kifaa chenyewe cha bei ghali zisizopungua milioni 300 na kitu, hatuwezi tu kama tunaokwenda kununua boflo pale Darajani. Lazima tutiliane mkataba kujua masharti ya utengenezaji *maintenance services* zitakuwaje na *spares* zitapatikanaje, lakini nalo limo njiani.

Sasa ile hali tunayoiona pale pwani ya kutupwa taka si nzuri na miaka miwili, hivi sasa inasemwa hiyo hakuna anayependa hilo, lakini na ule utaratibu wa kupata hicho kifaa ni lazima tufuate taratibu za serikali.

Nadhani jengo la macho amelizungumza Mhe. Naibu Waziri.

Suala la usafi wa hospitali nimeambiwa chafu ni kweli, kwa mwaka tumepewa milioni 78 kusafisha hospitali ile ambayo kwa mwezi Hospitali ya Mnazi Mmoja ili iwe ina sura, inahitaji milioni 15. Sasa milioni 78 ukizigawa kwa 12 utaona ni kiasi gani. Tulikuwa moja ya tatizo letu ni kwamba hatuna wafanyakazi ma-*orderly*, lakini bahati nzuri tumeajiri wa kutosha sasa ma-*orderly*, lakini mtaji wenyewe ndio lile lile suala la fedha.

Suala la mafaili na takwimu lilizungumzwa hapa kwamba mafaili yale yapo gizani na nini, ni kweli hivi sasa tunaanza kuyaingiza kwenye kompyuta ili tarakimu zile badala ya kuwa kwenye faili moja moja, iwe tunaweza kuzipata kwenye mtandao, lakini kuna tatizo vilevile na jamaa hawa tunaokwenda hospitali. Mimi mara moja mbili nimeshakwenda Dar-es-Salaam, ukifika hospitali uliyokwenda mara ya kwanza kuji-*register* unapewa kadi, ukishapewa ile kadi unaambiwa kila ukenda pale hospitali unakwenda nayo.

Ukifika pale unakwenda kwenye *reception* ukitoa ile kadi jamaa anazunguka hivi au anakwenda ndani anavuta faili anakuletea. Hapa tulikuwa na utaratibu huo, lakini kwa sababu ya mazoea na dharau, mtu kadi anaiacha nyumbani akifika pale anafunguliwa faili jengine, akija tena mara ya tatu anafunguliwa. Kwa hivyo, yale mafaili wengine ni mawili au matatu ya mtu mmoja kwa sababu ule utaratibu wa kulinda yale haukuwa mzuri. Tunajitahidi kubadilisha utaratibu huo na Mungu akijaalia, lakini itachukua muda kidogo, si suala la muda mdogo kwa sababu ni kubwa.

Suala la pili, Mhe. Spika, ni madawa. Nilipoingia Wizara ya Afya, fedha za madawa ilizokuwa ikipangiwa ilikuwa ni kama milioni 350 na milioni 400, mwaka wa pili nikaongezewa zikafika kama milioni 700 ingawa hatuzipati zote, lakini *allocation* ikawa inaongezeka. Mwaka jana nikaongezewa nikapata bilioni 1.5 ile tuliyoisema 37, lakini *allocation* imeongezewa. Mwaka huu tunaoendelea nao tumepangiwa bilioni 2.1 na nakumbuka katika maamuzi ya serikali aliambiwa Waziri wa Afya kwamba jitahidi suala hili la dawa liwe halina muhali kwamba tukenda tukitaka pesa za dawa, basi kama mambo mengine tutakosa, lakini za dawa tupate.

Kwa kiasi fulani namshukuru Waziri wa Fedha kwamba hilo nalo amelizingatia hadi sasa tumeshapewa milioni 811 kwa miezi mitatu ya kwanza, miezi hii iliyobaki hatujapewa, lakini wameturuhusu kukopa dawa za milioni 600. Bila shaka maana yake ni wana *commitment* kwamba watatulipia pesa hizo. Kwa hivyo, hali ya dawa si mbaya sana na hata katika mjadala wote huu yamezungumzwa mengi Hospitali ya Wagonjwa wa Akili, lakini dawa kwa jumla iliguswa sana mara hii, kuliko lilivyokuwa likizungumzwa kwa sababu hali ya dawa si mbaya sana, *infact* kuna dawa tumepata nyengine

za wafadhili, *four billions* tumepata kwa jamaa wengine kuchangia. Suala la dawa linaanza kuwa sio tatizo baada ya muda.

Mhe. Spika, suala jengine lililozungumzwa ni uchakavu wa majengo. Mhe. Naibu Waziri, aliligusia lile la macho, lakini uchakavu wa majengo ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ni suala la tangu mimi sijazaliwa, Karne ya 18 ile, ninadhani imejengwa ile 1928 ninaambiwa, sijui pengine hata udongo ulikuwa haupo. Sasa limechakaa jengo lile ni kubwa linahitaji *over whole*.

Matengenezo tunayofanya ni madogo madogo, yanahitajika matengenezo makubwa. Watu wa *BADEA* shirika lile la misaada la Uarabuni limeweza kutupatia msaada, limefanya utafiti ripoti yake tayari tunabembeleza watupatie hizo pesa tufanye *overwhole*, yaani tulitengeneze lote kwa pamoja. Pale tunapopata matatizo, hivi sasa kuna matengenezo fulani pale yanaendelea, lakini ni madogo madogo. Hili jengo la macho amelieleza uzuri.

Kuna suala la vituo vya macho vya mashamba. Vituo vya mashamba kuna wafadhili wa aina tatu au nne wanatusaidia. Kuna mradi wa Orael umesema utasaidia kutengeneza baadhi ya vituo vya mashamba, kuna SMZ yenyewe, *DANIDA*, *ADB*, wote hawa kwa kiasi fulani wamegawana wataendelea kutengeneza vituo vya mashamba ili vile vilivyochakaa vipate kuwa vizuri.

Suala la msingi amelisema Mhe. Naibu Waziri, hapa kwamba karibuni tumepata agizo kutoka serikalini na limetangazwa sana, ninadhani alitangaza yeye mimi nilikuwa kwenye likizo, kwamba hakuna ruhusa, tena hapa ni nafasi nzuri Waheshimiwa Wawakilishi kama munataka turufu ya kura, isiwe kwa kujenga kituo cha afya, jengeni nyumba za wafanyakazi, tusaidieni vifaa na matengenezo angalau tulipieni huo umeme.

Kila mmoja kama vile tunafyatua matofali, kila mmoja anaona hapati kura kama hajajenga kituo cha afya. Ikifika pahali dawa, wafanyakazi. Matokeo yake Mhe. Spika, tunaelemewa. Kwa hivyo, tunawaomba tubadili mbinu sasa, tutafute kura kwa kutusaidia madawa, kujenga nyumba za wafanyakazi au tulipieni huo umeme. Limetajwa hapa suala la umeme Mhe. Spika, katika watu wanaodaiwa kwenye serikali hii na Shirika la Umeme, deni kubwa ninadhani sisi ni nambari mbili, namba moja ni Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) hiyo.

Hili si la jana wala juzi, ni la miaka mingi na dunia nzima hospitali ni kawaida, hospitali haikatiwi umeme kwa sababu ni pahali ambapo hata huko kwenye vita watu wakikimbia, wanakimbilia Hospitali kwa sababu wakifika wanajua wapo salama.

Sasa hizi taratibu zilizotokea juzi kidogo, lakini ninadhani walizinduka wakaona tunalipa tunapoweza na vile vituo vya mashamba hivyo hivyo navyo, kwa kila siku sasa tumekubaliana kila idara, tutakapoipa pesa zake, ikate angalau shilingi milioni moja au laki tano, kila mwezi wawe wanalipa kidogo kidogo, lakini itachukua muda mrefu.

Mhe. Spika, kuhusu suala la wagonjwa wa India limezungumzwa. Mama Sira amesema hapa kidogo, lakini hatuna hospitali moja kule India tunazopeleka wagonjwa na hiyo ilikuwa ni ushauri wa hapa hapa kwamba tusitegemee Hospitali moja. Ninavyozijua mimi kuna Hospitali ya *Appolo* ambayo imesemwa kidogo hapa, kuna Hospitali ya *Apuna* ambapo huku ni maradhi ya mifupa tu, kuna hospitali ya Miot imetajwa hapa. Sasa hivi tumekubaliana na *Ras El Khaimaa* kule Uarabuni tunaweza kupeleka wagonjwa.

Hivi sasa tunapeleka wagonjwa Hospitali ya Muhimbili kwa mkataba. Zamani ilikuwa Muhimbili *general*, lakini na sasa hata ile hospitali ya mifupa itabidi nayo tukubaliane. Halafu kuna na hospitali nyengine inaitwa *Escot*, zote hizi huwa tunapeleka wagonjwa na moja katika kitu kinachotumaliza Mhe. Spika, kwenye bajeti yetu ni gharama za kupeleka wagonjwa India na kwengineko.

Gharama ni kubwa, lakini Mhe.Rais alisema hakuna bei ya uhai, haijawahi hata siku moja kuambiwa maisha ya Juma Duni shilingi kumi na ya fulani shilingi kumi na tano. Uhai ni uhai, anapoumwa mgonjwa inabidi apelekwe.

Tatizo tulililonalo Mhe.Spika, wagonjwa ni wengi kuliko uwezo na hatuwezi kuwapeleka kwa pamoja. Kwa hivyo, tumeweka utaratibu pale. Daktari akishamuona mgonjwa akiona hatibiki ana-*refer* kwenye *Medical Board*, *Medical Board* ikimaliza inamletea mkurugenzi mkuu wa makao makuu, mkurugenzi mkuu akikutana na Katibu Mkuu wakisha-*approve*, wanamletea Waziri, Waziri anaambiwa huyu tunaruhusu anaweza kupelekwa nje kutibiwa. Mimi ninasaini inakwenda kwa Mhe. Waziri wa Fedha na mgonjwa anakwenda.

Na kwa wastani mgonjwa anayekwenda India mara nyingi ni wale wanaokuwa na maradhi ya muda mrefu na yanayohitaji kutunzwa kwa muda mrefu. Kila mgonjwa si chini ya dola elfu saba na mia nne na mara nyengine inabidi tumpeleke na mtu afuatane naye. Kwa hivyo, bill yetu ya malipo ya wagonjwa nje ni kubwa kidogo Mhe.Spika, na tunaomba wazee wafahamu hivyo.

Suala la magari. Lazima nikubali Mhe.Spika, magari mengi ni machakavu na hapa imetajwa Wilaya zile hazina gari, macho hawana gari, Mwembeladu hawana gari, wagonjwa wa akili hawana akili, wafanyakazi hawana gari, kila

mmoja hana gari. Ni gari nyingi na uwezo hatuna. Lakini nilipokuwa ninawasilisha maagizo mwaka jana nilisema kwamba kama kuna ma-*ambulances* matatu manne yanakuja yatasaidia, moja litakuwa Hospitali ya Mwembeladu, likiwemo Mwembeladu linaweza ku-*save* na kule kwa Mhe. Hamza Hassan Juma, mental kule. Lakini yanategemewa kuja hayo, yapo njiani kwa msaada wa *UNFPA.*

Uhaba wa fedha umetajwa Mhe.Spika, na kwa jumla nilikuwa na shauri moja tu nilieleze Mhe. Waziri wa Fedha amesema. Lakini kila mwaka tunasema Wizara ya Afya ina tatizo la fedha, wananchi tunawachangisha. Kwa miaka miwili sasa, mimi na wenzangu wizarani tunatafuta ufumbuzi wa suala hili. Suala hili litafumbuka, tutakapopata bima ya afya, tuki-*solve* tatizo la bima ya afya, itakuwa mwananchi analipa kabla ya mchango wake.

Kwa hivyo, atakuwa na haki kudai kwamba lazima apate matibabu kwa sababu analipia. Hivi sasa wananchi bado wananchi wanachangishwa kinyume nyume kwa sababu ndio hali halisi, lakini suala hili limeshafika mbali, ilikuwa ni tatizo kuwapata wataalamu.

Wataalamu wa kufanya bima ya afya ni wataalamu maalum Mhe. Spika, na lazima ujue gharama zake. Sasa nimeshawapata na hivi sasa tunaendelea nao, tulikuwa na ukosefu wa fedha, pengine mwisho wake nitafika kwa Ba. Omar, lakini Ba. Omar akinipa fedha zile zitamnusuru baadae kudaiwa fedha kwa sababu itakuwa sasa kwa kiasi fulani fedha zinachangiwa.

Hili ninategemea lipata ufumbuzi Mwenyezi Mungu akijaalia baada ya mwaka mmoja ujao kwa sababu tunahitaji kupata hiyo gharama, kuthibitisha ni kiasi gani, kutayarisha mfumo na kuandikwa sheria. Ni matatizo ya muda mrefu.

Mhe. Spika, la mwisho ni Hospitali ya Mkoani. Mhe. Abdalla Mohamed Ali nani pale alizungumza mambo mengi kuhusu...

Mhe. Spika: Mhe. Abdalla Mohamed Ali.

Mhe. Waziri wa Afya: Ardhi pale tumeshalipa. Nimesema asubuhi. Watu wote wameshalipwa. Kuna watu kama wawili hawajalipwa, lakini sababu si zetu, sababu ni zao. Kwa sababu ile *estimation* au tathmini ya zile nyumba hakufanya Jidawi wala Juma Duni, wala Sira, wamefanya wataalamu wanaostahiki.

Kuna mrembo mmoja baada ya kwisha kufanywa makisio anatuletea na ramani, anasema mimi ningekuwa nimejenga nyumba yangu ingekuwa na

thamani hii. Sisi hatuthamini ramani. Tumethamini nyumba tulichokiona na baada ya hapo ukishalipwa hizo pesa, wamesaidiwa na kiwanja ambapo ilikuwa si wajibu wetu, wameambiwa na vitu vyao wachukue, lakini bado bibi anatuletea ramani na *bill of quantity* kwamba thamani yangu ningekuwa na nyumba hii.

Bado tunavutana, tunamshauri kwamba hii ni hali halisi wenzake wote wamepokea michango yao, yeye bado hajachukua na amelitaja suala la Msikiti. Msikiti kuna fedha zake zipo na kila mara ninamuuliza Katibu Mkuu kwamba hizi haziwezi kutoka, lazima kuwe na utaratibu maalum. Kuna mfadhili mmoja ametaka kujenga Msikiti kusaidia katika kutoa sadaka, nikasema kama anataka kutoa sadaka, aje tukubaliane kwa mkataba, tujue anachangia nini na sisi tunachangia nini, itolewe *contract*, wajenge huyo anayejenga, tujue sisi tunatoa nini na yeye anatoa nini ili kesho tukiulizwa na mwenye fedha ajulikane amefanya nini na sisi tumetumiaje.

Mhe. Spika, la mwisho naomba nimshukuru Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwamba tumefahamu tuliyofanya na amesema yaishe, hatuna haja ya kuvutana katika suala hili. Na mimi ninashukuru hivyo na hakuna haja ya kuendelea, maana ilikuwa sijui iende kwenye Kamati ya Maadili na nini, mwenyewe amesema yameisha. Tumefahamu yaliyotokea.

Kaja kaniambia ananisamehe na mimi nimemsamehe ndio katika kufanya kazi mambo haya ni lazima yanatokea, hakuna haja ya kuliendeleza, lakini ukweli kulitokeza, vipi ilivyokuwa na mimi niliona vipi nilieleza. Ninadhani tufunge buku, tuanze upya. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Ninakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, shughuli hii ilikuwa imalizike jana, lakini kwa sababu ya shughuli ambazo zimetangulia zilichukua muda mrefu kidogo, tunakusudia imalizike leo ili kesho tuendelee na shughuli nyengine ambayo inahusu pamoja na Wizara ya Fedha ambazo baadhi ya hoja zake tayari zimeshatolewa, tunategemea majibu yatakuja kutoka. Hivyo, ili tuweze kumudu na kuwahi na shughuli nyengine kubwa katika nchi yetu. Niwaombe basi tukubaliane kwamba Mhe.Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili, akuombeni tuongeze muda si mkubwa sana ili kumaliza shughuli hii, ili kesho tuendelee na ratiba nyengine.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe.Spika, kwa kuwa shughuli zilizo mbele yetu bado kumalizika na kuwa muda kwa mujibu

wa Kanuni zetu zinatarajiwa kumalizika. Kwa hivyo, ninaliomba Baraza lako tukufu tuweke kando Kanuni ya muda ili tuweze kuendelea kumaliza shughuli zilizo mbele yetu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Mimi ninakushukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe kukubali kwamba tuendelee na shughuli hii. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, naomba kumshukuru sana Mhe. Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake ya Baraza lako tukufu kwa kuwasilisha kwa ufasaha ripoti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Pia, ninawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza waliochangia ripoti hiyo. Naomba niwataje wote:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
3. Mhe. Hamad Masoud Hamad
4. Mhe. Salim Abdalla Hamad
5. Mhe. Mgeni Hassan Juma - kwa maandishi
6. Mhe. Mwanaidi Kassim - kwa maandishi
7. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - kwa maandishi

Na maandishi kwa bahati nzuri ninayo haya hapa Mhe. Spika.

Mhe. Spika, naomba sasa kutoa ufafanuzi kuhusu hoja zilizotolewa na Wajumbe. Wa kwanza nikianza na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, alikuwa na hoja zifuatazo. Je, sera ya kumaliza majengo ya skuli yaliyoanzishwa na wananchi bado ipo. Jibu lake ni kwamba bado sera, bado ipo na wizara inajitahidi kukamilisha majengo ya skuli hasa katika maeneo yenye idadi kubwa ya wanafunzi. Kwa mwaka 2012/2013 wizara imekamilisha madarasa 185 na kwa mwaka 2013/2014 wizara inaendelea na ukamilishaji wa madarasa 480.

Pili, michezo irejeshwe maskulini hasa ya riadha. Mhe. Spika, michezo imo katika skuli zetu pamoja na riadha, ndio maana vijana wetu wameweza katika mashindano ya Umoja wa Michezo wa Shule za Sekondari Tanzania (*UMISETA*) yanayofanyika kila mwaka Kibaha Tanzania Bara.
Mwaka 2013 timu ya riadha ilikuwa nafasi ya tano kati ya kanda 12. Vilevile, wizara imeanza kuendesha mashindano ya *cross country* kwa wanafunzi wa skuli ya msingi na sekondari mwaka 2013 na mwaka huu mashindano hayo yatafanyika mwezi Machi mwaka huu 2014. Pamoja na hayo imeundwa kamati maalum ya wizara pamoja na Wizara inayoshughulikia masuala ya michezo kuangalia namna ya kuimarisha michezo maskulini.

Mhe. Spika, ardhi iliyojengwa skuli ya Regezamwendo, eneo lililobaki apewe aliyekuwa akimiliki ardhi hiyo atafutiwe sehemu nyengine. Mrithi wake ni Bwana Ramadhan Khatib. Mhe. Spika, wizara inaahidi kulifuatilia suala hili na kulipatia ufumbuzi kwa mashirikiano na Wizara inayohusika na masuala ya ardhi.

Mhe. Spika, sasa ninakuja kwa Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Mhe. Spika, alishangazwa na utaratibu wa serikali wa mawaziri kukaimu wizara nyengine na hata Naibu Waziri hayupo Barazani hasa katika Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba nimueleze kwamba Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, yupo likizo na utaratibu wa serikali ni kuwa waziri mwengine kukaimu na ninayemkaimu ni mimi hapa, naye Naibu Waziri kwa leo ni mgonjwa, tangu jana ni mgonjwa.

Mhe. Spika, ninamshukuru Mhe. Jussa Jussa Ladhu, kwa kuliona suala la ufinyu wa Bajeti ya wizara na namna inavyokwamisha utekelezaji wa malengo ya wizara. Ninapenda kumjibu suala lake Mhe. Hamad Masoud Hamad, kuhusu sifa ya mwalimu mkuu wa Skuli ya Darajani ambaye yeye anasema ni mwalimu wa cheti. Baada ya kukamilika Skuli ya Forodhani, Skuli ya Darajani iligaiwa sehemu mbili; skuli ya sekondari ikahamia skuli ya Forodhani na Darajani ikabaki ni skuli msingi.

Mwalimu Mkuu Skuli ya Darajani msingi ni mwalimu mzoefu na ana sifa ya cheti cha ualimu. Katika Skuli ya Darajani msingi hakuna mwalimu mwenye *degree.* Kwa Skuli ya Forodhani ambayo sasa ni sekondari, Mwalimu Mkuu ana *degree* na ni mwalimu mwenye uzoefu wa muda mrefu na hiyo ndio sifa ya Mwalimu Mkuu wa sekondari.

Mhe. Spika, kuhusu Bodi ya Mikopo. Ninapenda kumuhakikishia Mheshimiwa, kuwa hakuna ubaguzi wowote katika utoaji wa mikopo. Katika

Wajumbe wa Bodi wa Mikopo miongoni mwao ni kiongozi wa shughuli za serikali, wanafunzi na Mjumbe mmoja wa Baraza. Jumla ya wawakilishi ambao wanashiriki katika kikundi...

UTARATIBU

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, hebu tulia kidogo kuhusu utaratibu Mhe. Hamad Masoud Hamad.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, ninafikiri ni vyema kuweka *Hansard* sawa, mimi sikusema Skuli ya Darajani, nilisema Skuli ya Kangagani. Sasa akisema kwamba Skuli ya Darajani mwalimu hivihivi, mimi sikutaja Darajani. Naomba Mhe. Waziri, aiweke vizuri hii ili *Hansard* isijekuwa ninamtia mtu mwengine makosa au mimi sifahamu jambo ikaonekana kwamba anavyosema yeye ni sawa, ni Skuli ya Kangagani na si Darajani.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Spika, nashukuru kwamba amefanya masahihisho na mimi ninakubali masahihisho yake. Kuhusu Bodi ya Mikopo. Ninapenda kumuhakikishia Mheshimiwa, hakuna ubaguzi wowote katika utoaji wa mikopo. Katika wajumbe wa Bodi wa Mikopo, miongoni mwao ni kiongozi wa serikali, wanafunzi na Mjumbe mmoja wa Baraza lako tukufu la Wawakilishi ambaye wanashiriki katika vikao vya bodi vinavyotoa maamuzi ya kutoa mikopo.Katika uteuzi wa wanafunzi wa kupata mikopo. Bodi inapokea maeneo ya vipaumbele ambavyo vimeekwa na Tume ya Mipango. Maeneo hayo ya vipaumbele ni hayo yafuatayo:-

- Sayansi
- Uchimbaji wa mafuta
- Udaktari
- Uhandisi
- Kompyuta
- Uchumi
- Ualimu wa sayansi

Waombaji wa mikopo wa maeneo, ndio wanaochaguliwa kwanza, yaani hawa ndio wanaopewa nafasi ya mwanzo. Maeneo ambayo mara nyingi huwa hawapati mikopo ni wale wanaosomea sheria, sanaa, dini na kiarabu kwa sababu hata kwenye ajira waliosomea maeneo haya, wengi wao wanashindwa kupata kazi na hatimaye wanashindwa kurejesha mikopo.

Hata hivyo, waombaji wa mikopo ni wengi kuliko uwezo wetu wa kuwapa mikopo. Fedha ambazo Mhe. Mwakilishi, amezitaja ni chache mno ukilinganisha na maombi yanayopokelewa.

Mhe. Spika, sasa naomba nimjibu Mhe. Salim Abdalla Hamad. Kuhusiana na matokeo ya mtihani wa darasa la saba na kidato cha pili, ninapenda kumuhakikishia Mheshimiwa, kwamba matokeo hayapangwi kisiasa, bali yanategemea na vigezo vilivyoekwa vya ufaulu wa wanafunzi na ndio maana katika baadhi ya miaka matokeo yanashuka na miaka mengine matokeo yanapanda. Kwa misingi hiyo hiyo, ndio maana utakuta kwamba baadhi ya skuli zinapasisha wanafunzi wengi na baadhi ya skuli wanapasisha wanafunzi wachache, alama zilizoekwa za ufaulu wa wanafunzi hazijabadilishwa ni zile zile zinazotumika katika miaka yote.

Hivyo, ni wale wanafunzi walioweza kufika alama zinazotakiwa, ndio wanaochaguliwa kuendelea na masomo. Sera yetu ya elimu ya 2006 inaagiza kwamba elimu ya lazima kwa Zanzibar itakuwa hadi kidato cha nne, lakini utekelezaji wa sera hiyo unakwenda sambamba na kuongezeka ufaulu wa wanafunzi.

Hivyo, wizara haikimbilii kuwapeleka wanafunzi wote hadi kidato cha nne kama hawafaulu mitihani yao. Wizara inafanya jitihada ya kuimarisha ubora wa elimu kwa kuzipatia skuli nyenzo za kufundishia ikiwemo vitabu na vifaa vya maabara na pia kuhimiza mafunzo ya walimu na mambo hayo ndio yanayochangia katika kuwafanya wanafanya wanafunzi wafanye vizuri zaidi.
Mhe. Spika, naomba sasa nimuelezee Mhe. Mgeni Hassan Juma, ambaye yeye amechangia kwa maandishi. Naomba niyasome maandishi kwa sababu ni muhimu.

Mhe. Spika, Mheshimiwa, anasema taarifa ya uchunguzi kuhusu matokeo ya mitihani ya *Form IV* mwaka 2012 haikuwasilishwa Barazani. Mhe. Spika, taarifa kuhusu matokeo ya mitihani ya *Form VI* ilitolewa katika kongamano lililofanyika mwezi wa Oktoba, 2013 na Wajumbe wa Baraza hili walialikwa...

Mhe. Spika: Mhe. Mgeni Hassan Juma, alizungumza kwa kusema, sijui hii *note* alikuja kuleta na maandishi mengine au pengine.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Spika, naomba nikwambie kwamba Mheshimiwa, aliposimama alizungumzia kuhusu Wizara ya Uwezeshaji na nini, sasa hii ni Wizara ya Elimu.

Mhe. Spika: Haya tuendelee.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Mhe. Spika, taarifa kuhusu matokeo ya mitihani ya *Form VI* ilitolewa katika kongamano lililofanyika mwezi wa Oktoba, 2013 na Wajumbe wa Baraza hili walialikwa, lakini kwa bahati mbaya hakuna hata mmoja aliyeshiriki.

Hata hivyo, nitamkumbusha Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amai, kuhusu suala hili na mimi akirejea tu Mheshimiwa, nitamkumbusha kuhusu suala hili na nitamkabidhi maandishi haya. (*Makofi*)

Mhe.Spika, nikiendelea naomba sasa nieleze kuhusu maelezo ya Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, ambayo naona yana umuhimu wake, anasema changamoto zinazowakabili Idara ya Elimu na Maandalizi ya Msingi kukosekana kwa posho kwa walimu hawa. Mhe. Waziri, kama tunavyoelewa skuli hizi wengi ni wanawake wanaofundisha na wanawake hawa hufanya kazi ya kuolea watoto, si mchezo kukaa na mtoto mdogo ukamuelimisha hadi kufikia elimu ya msingi ni kazi kubwa sana. Na Waswahili husema "Ndama ndama ndio ng'ombe". Kwa hivyo, naungana na mimi kwamba walimu hawa wa maandalizi waangaliwe kwa jicho la huruma.

Mhe. Spika, Skuli ya Ufundi Kengeja kuna ukosefu wa dakhalia hasa kwa wanafunzi wa kike. Mhe.Spika, hasa sisi wanawake tumekosa nini, huoni ni kuwarudisha nyuma wanawake. Leo wanawake wanakosa pahala pa kukaa pamoja ili kutafuta elimu kwa pamoja. Huu ni usumbufu. Mheshimiwa, naomba ulitilie mkazo zaidi ili nyumba za kukaa, lakini pia ukosefu wa vifaa uangaliwe kwani ikiwa hapana vifaa ndio hapana kusoma. Pengine nikuulize tena, naomba unijibu Mheshimiwa wangu hapana dereva, lakini gari ipo na ikiwa ipo kwa nini ikakosekana dereva.

Ahsante Mheshimiwa, nilitaka niyasome haya ili muyasikie Waheshimiwa na nitayachukua haya ili nimkabidhi mwenyewe Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, atakaporudi.

Mhe. Spika, nikiendelea kuhusu ripoti ya Tume ya Uchunguzi ya Matokeo ya Mtihani, ni kweli kwamba ripoti ya uchunguzi wa matokeo ya mitihani itawasilishwa kwa Baraza lako tukufu baada ya kukamilika. Ripoti na matokeo hayo wizara ilikusudia kuzungumza taarifa hiyo ya matokeo ya mitihani katika kongamano la elimu lililoandaliwa tarehe 6 mpaka 7 mwaka 2013, katika kongamano la kimataifa ambapo Wajumbe wako walipewa mualiko kwa bahati hawakushiriki.

Mhe. Spika, nalisema kwa mara ya pili kwa sababu suala hili ni muhimu na Wajumbe nawaomba wakati wowote tukipewa mualiko tujitahidi tushiriki, mambo haya ni muhimu na yana maana sana. Kongamano hilo kwa sababu mwasilisha mada alipata ajali ya kugongwa na gari na kulazwa hospitali siku mbili kabla ya kongamano. Hata hivyo, wizara inaahidi kuiwasilisha Barazani ripoti katika siku za karibuni.

Mhe. Spika, mwisho naomba sasa nizungumzie kuhusu Ndugu Mwanaidi Kassim alisema kwamba tunampongeza Mheshimiwa, kutokana na mchango wake suala la hatimiliki za maeneo ya skuli. Wizara imeshawasilisha skuli ambazo zinahitaji hatimiliki kwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na mazungumzo kati ya wizara mbili yamefanyika kuona jinsi gani maeneo hayo yanaweza kupewa na kupatiwa hatimiliki.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, naomba kuwasilisha.(*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Kaimu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, ila tu ile hoja ya Mhe. Hamad Masoud Hamad, kuhusu mwalimu mkuu wa skuli ya Kangagani ninadhani hilo mulichukue mukalifanyie kazi. Baada ya hayo sasa, naomba nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Mgeni Hassan Juma (Mhe. Mwenyekiti wa Maendeleo ya Wanawake na na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu leo kwa kunipa afya njema na kuweza kusimama hapa kwa ajili ya kufanya majumuisho.

Mhe. Spika, pia, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii adhimu ambayo kwa siku ya leo itakuwa ni mchangiaji wa mwisho katika kutoa majumuisho ya kadhia yetu hii ya leo.

Mhe. Spika, naomba muwatambue wachangiaji ambao wamechangia ripoti hii ambao ni 17, na Mjumbe mmoja amechangia kwa maandishi.

Wachangiaji wenyewe ni:-

1. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
2. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
3. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
4. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
5. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
6. Mhe. Farida Amour Mohammed

7. Mhe. Abdi Mossi Kombo
8. Mhe. Fatma Said Mbarouk
9. Mhe. Hamad Masoud Hamad
10. Mhe. Salim Abdalla Hamad
11. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
12. Mhe. Waziri wa Fedha
13. Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto
14. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
15. Mhe. Waziri wa Afya
16. Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: (Kaimu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali) na
17. Mhe. Nassor Salim Ali ambaye amechangia kwa maandishi.

Mhe. Spika, awali ya yote niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri pamoja na Naibu Waziri wa Afya, kwa kuweza kutoa taarifa ambazo zimeweza kwa kiasi kikubwa kusaidia katika michango au wasiwasi waliokuwa nao Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, kwanza nilizungumzia mimi mwenyewe katika ripoti suala zima la uhaba wa fedha. Mhe. Spika, uhaba wa fedha katika wizara mbili, Wizara ya Afya pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imekuwa ni changamoto kubwa ambayo imezungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi ambao wamechangia.

Pia nitoe shukrani nyingi kwa Mhe. Waziri wa Fedha ambapo hapa ameweza kidogo kutueleza kwamba uwezekano sasa wa fedha kupatikana ni mkubwa. Mhe. Spika, mengi ambayo yamezungumzwa na mengi ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali basi yamehusiana katika masuala ya ukosefu wa vifaa.

Kwa upande wa Wizara ya Afya Mhe. Spika, Wajumbe wamezungumzia suala zima la ukosefu wa vifaa, uhaba wa maeneo yaani ofisi na pia wamezungumzia changamoto za usafiri katika Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, kwa upande wa Wizara ya Afya Waheshimiwa wengi wamesisitiza kuhusu kifaa cha *incinerator* na *PCR*, ambapo wameona vifaa hivyo vina umuhimu mkubwa wa kuvipata.

Mhe. Spika, kamati yangu inasisitiza kwamba kwa kuwa tayari fedha zimepatikana, basi vifaa hivi na hasa kifaa cha *incinerator*, kwa kuonekana umuhimu wake mkubwa basi kipatikane katika kipindi cha robo inayokuja.

Mhe. Spika, vile vile kwenye suala zima la Hospitali ya Wagonjwa wa Akili, ambapo fedha zilizopatikana zilikuwa ni chache mno na hiyo imesababisha kwamba wagonjwa katika hospitali hiyo wamekuwa wakipata mlo mmoja kwa siku. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kamati inasisitiza kwamba tatizo hili kwa kweli uwezekano wa kuondoka upo, kwa hivyo tunaomba tatizo hili lifanyiwe kazi.

Mhe. Spika, tatizo hilo la kukosekana kwa chakula halijajitokeza tu katika Hospitali ya Wagonjwa wa Akili, lakini vile vile limejitokeza katika Hospitali ya Mwembeladu na Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, tumefarijika kuelewa kwamba sasa angalau Wizara ya Afya wana uwezo wa kununua dawa, ingawa bado ni changamoto. Tunamuomba Mhe. Waziri wa Fedha kuhakikisha kwamba fedha hizi zinapatikana, kwa sababu wengi wa wagonjwa wetu ni wanyonge na kwa kweli wanahitaji msaada katika kununua dawa.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo Waheshimiwa Wajumbe wengi waliochangia wamelizungumzia kuhusu Wizara ya Afya ni suala la ajira. Nashukuru kwamba Mhe. Naibu Waziri wa Afya ameweza kulitolea ufafanuzi. Kwa hivyo, tunatarajia kwamba suala hili pia litafanyiwa kazi kutokana na upatikanaji wa fedha.

Mhe. Spika, sasa naingia katika Wizara ya Elimu. Katika wizara hii pia tumeona ufinyu wa bajeti na uingizwaji wa bajeti unasababisha kukwaza shughuli nyingi za wizara hii. Mhe. Spika, ubovu wa majengo umedhihirika, ufinyu wa maskuli hasa katika madarasa, kukosekana kwa madawati, yote hayo yanasababishwa na ukosefu wa fedha za kutosha.

Mhe. Spika, suala la uhaba wa walimu hasa katika masomo ya Sayansi, Hesabati na Kiingereza yamezungumziwa sana na wachangiaji. Kwa hivyo, tunaiomba wizara suala hili ilishughulikie ili kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata taaluma katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, katika Wizara ya Elimu kuna mengi ambayo yamezungumzwa. Kwa mfano suala la usafiri, ofisi, vifaa mbali mbali ambavyo vinatumika katika kusomeshea watoto. Jengine ambalo Waheshimiwa Wajumbe wengi wamelizungumzia ni suala zima la kufeli na utoro wa wanafunzi.

Mhe. Spika, suala la kufeli kwa wanafunzi limekuwa ni changamoto kubwa katika taifa letu. Kwa bahati nzuri Wajumbe wengi ambao wamechangia wameligusia. Mhe. Spika, kuna hatua mbali mbali zimechukuliwa tunajua na

tunaona, lakini bado wizara ijipange ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu wanafaulu mitihani yao na waweze kuendelea na elimu ya juu.

Mhe. Spika, wizara ya mwisho ni Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto nayo ilikuwa na changamoto zake. Lakini nimshukuru sana Mhe. Waziri ameweza kutoa ufafanuzi wa changamoto hizo. Vile vile wizara hii inaonekana kwamba shughuli zake nyingi zinafanyika vizuri, lakini Mhe.Spika, kuna mambo ambayo yamezungumzwa, hivyo ningeomba sana wizara iyafanyie kazi.

Mhe. Spika, suala moja ambalo limezungumzwa ni suala la kuwa na jenereta ambalo litakuwa ni la dharura kwa nyumba ya watoto wa Mazizini. Vile vile Waheshimiwa Wajumbe wengi wamezungumzia suala zima la kutoa elimu ya ushirika kwa wajasiriamali wetu wengi, kwa sababu bado inaonekana tatizo kubwa hasa la wajasiriamali ni uwekaji wa fedha zao, suala hili ndilo linalosababisha hawa wajasiriamali wanavunjika moyo, wanaacha kufanya zile shughuli na wengine kupelekea kushindwa kulipa mikopo ambayo wanakopa katika wizara hii. Kwa hivyo, Wajumbe wengi wameomba kwamba elimu itolewe kwa upande wa vikundi hivi vya ushirika.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limezungumziwa sana katika wizara hii ni suala la kuanzisha benki ya wanawake. Mhe. Spika, Waziri ametuelezea na ameeleza changamoto zinazojitokeza katika kuanzisha benki hii. Lakini hata hivyo, kamati inasisitiza, kwa sababu hili ni suala ambalo tumekuwa tukilizungumza kwa muda mrefu, na Mhe. Rais ameonesha nia ya kuwepo kwa benki hiyo, hasa kwa sababu itawasaidia wanawake na vijana. Kwa hivyo, tungeomba sana Mhe. Spika. Kamati inaomba kwamba wizara na kwa sababu sasa hivi uwezeshaji wanayo wao, basi wafanye mikakati ya kusaidia kuwepo kwa benki hii.

Mhe. Spika, jengine ambalo limezungumzwa katika wizara hii na limezungumzwa sana ni suala lile la malipo ya fidia. Mhe. Spika, niishukuru sana Wizara ya Fedha, kwa sababu tumefanya kazi nao pamoja na wamekuwa tayari kuhakikisha kwamba fidia hii zinalipwa na wameahidi na ninaamini kwamba zitaweza kulipwa pale ambapo watakuwa na uwezo, lakini ninasisitiza kwamba fidia hizi hawa watu ni fedha za wanyonge, kwa hivyo wanastahiki kulipwa.

Mhe. Spika, mwisho kabisa niseme kwamba nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri ambao kwa kweli wametoa ufafanuzi mzuri, lakini nimshukuru zaidi Mhe. Waziri wa Fedha ambaye ameona changamoto ambazo zinazojitokeza katika wizara zetu, hususan Wizara ya Afya pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwa hivyo, ameahidi kuchukua hatua hizo,

hasa katika mafungu ya *OC* pamoja na mafungu ya miradi ya maendeleo. Mimi namuomba Mhe. Waziri kauli hiyo aiweke na tuione kwenye bajeti, ijitokeze kwenye bajeti, lakini kwa sasa tuhakikishe kwamba katika miezi sita hii basi fedha hizi ziingie na zisaidie katika mambo mbali mbali ya wizara hizi.

Vile vile nashukuru sana kwamba Waheshimiwa Mawaziri wa wizara zinazohusika wameweza kutupa ufafanuzi mzuri na kama kamati imeridhika, hasa kwa kutambua kwamba changamoto nyingi hazitokani na utendaji wao, bali zinatokana na matatizo ya kifedha.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti tunakushukuru kwa majumuisho na ufafanuzi huo wa ripoti ya Kamati yako. Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na ripoti za utekelezaji kwa wizara mbali mbali chini ya kamati hii, pamoja na kuipokea ripoti ya kamati wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nirudie kuwashukuru sana kwa mashirikiano makubwa tunayopeana katika kutekeleza shughuli zetu, mpaka kufikia leo katika shughuli hii ambayo ilikuwa ni nzito na refu kidogo, na tena tumeianza wakati wa dhiki kwenye kiasi cha saa 5:00, lakini hatimaye tunaimaliza sasa hivi kwanye saa 2:13.

Waheshimiwa Wajumbe, basi sasa tukapumzike na niakhirishe kikao hiki hadi kesho tarehe 30/01/2014, saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 2:13 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka
tarehe 30/01/2014 saa 3:00 asubuhi)